# KUCHUNGUZA MTINDO NA DHAMIRAKATIKA TAMTHILIYA YA MONDLANE NA SAMORA

**FATMA HASSAN ISMAIL**

**TASNIFU ILIYOWASILISHWA KUTIMIZA SEHEMU YA MASHARTI YA KUTUNUKIWA SHAHADA YA UZAMILI (M.A. KISWAHILI FASIHI) YA CHUO KIKUU HURIA CHA TANZANIA**

**2019**

## UTHIBITISHO

Aliyeweka saini hapa chini anathibitisha kuwaameisoma tasnifu hii yenye mada: **Kuchunguza Mtindo na Dhamira katika Tamthiliya ya *Mondlane na Samora***na kupendekeza ikubaliwe na Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kwa ajili ya kukamilisha masharti ya kupatiwa Shahada ya Uzamili ya Sayansi ya jamii katika Kiswahili Fasihi ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

**………………………………………..**

**Profesa Emmanuel Mbogo**

**…………………………………**

**Tarehe**

## HAKIMILIKI

Hairuhusiwi kuiga au kunakili kwa namna yoyote ile Tasnifu hii kwa ajili yoyotekama kwa njia ya Kieletroniki, Kurudufu nakala, Kurekodi au njia yoyote nyingine bilaya idhini ya Mwandishi au Chuo Kikuu Huria Kwa Niaba.

## IKIRARI

Mimi **Fatma Hassan Ismail**, nathibitisha kwamba tasnifu hii ni kazi yangu na haijawahi kuwasilishwa na haitawasilishwa katika Chuo Kikuu kingine kwa ajili ya Digrii yoyote.

**……………………………….**

**Saini**

**…………………………………..**

**Tarehe**

# TABARUKU

Tasnifu hii naitabaruku kwa Mume wangu mpenzi Bwana Khamis Salim Omar na watoto wetu Nassir, Amour, Asya, Sabra, Husna na Sahim na nawatakia dua kwa Mwenyezi Mungu awakuze na awape elimu yenye manufaa (Amin).

## SHUKURANI

Kwanza kabisa natoa shukurani kwa Mwenyezi Mungu (S.W) ambaye ameumba ulimwengu na vilivyomo ndani yake kwa kunijaalia uzima na afya njema na kufanikisha kazi hii ya utafiti hadi kukamilika. Kwa uchache wa shukurani ninasema Alhamdulillah.

Shukrani zangu za dhati zimfikie Msimamizi wangu Profesa Emmanuel Mbogo, Mwalimu Bakar Kombo Bakarkwa msaada wao wakutupa mwongozo na kuweza kufanikisha tasnifu hii, Wanafunzi wenzangu pamoja na uongozi wote wa Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (OUT) Mungu awalipe kheri ikiwa ni pamoja nakuwapa umri mrefu wenye manufaa kwao (Amiin).

Vile vile, shukrani zangu ziwaendee wazazi wangu ambao walinifunulia ufunuo huu kwa kunipeleka shule na hadi hii leo naendelea kutumia ufunuo huo. Sina zawadi ya kuwapa kwa vile wameshatangulia mbele ya haki ila namuomba Mwenyezi Mungu (S.W) azipumzishe roho zaopahala pema Peponi (Amiin).

Pia sina budi kuwashukuru Mwalimu Ali Mussa Faki, Mwalimu Mohd Ali Salim, Mwalimu Sharif Juma Fakih na Mwalimu Amour Rashid Ali kwa michango yao ambayo ilisaidia sana katika kufanikisha kazi hii. Nawale wote waliosaidia kwa njia moja au nyengine hadi leo hii kuweza kufanikisha tasnifu hii nao wote kwa pamoja Mungu awalipe jaza njema hapa duniani na akhera kwa msaada wao.

## ORODHA YA VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| BAKIZA | Baraza la Kiswahili Zanzibar |
| Dkt. | Daktarii |
| km. | kama |
| kv. | kama vile |
| ktj | Kashatajwa |
| OAU | Organization of African Union |
| Prof. | Profesa |
| S. W | Subhanahu Wataala |
| TATAKI | Taasisi ya Taaluma za Kiswahili |
| TUKI | Taasisi ya Uchunguuzi wa Kiswahili |

## IKISIRI

Lengo kuu la utafiti huu ni *Kuchunguza Mtindo na Dhamira katika tamthiliya ya Mondlane na Samora*. Utafiti huu ulikuwa na malengo mahsusi mawili ambayo ni, kubainisha vipengele vya mtindo katika tamthiliya ya *Mondlane na Samora*, na kubainisha dhamira katika tamthiliya ya *Mondlane na Samora*

Sampuli ya utafiti huu iliteuliwa kwa kutumia mbinu ya uteuzi wa madhumuni maalumu. Data zilikusanywa kwa kutumia mbinu ya maktabani kwa njia ya usomaji makini. Uchambuzi wa data ulifanyika kwa kutumia mbinu ya mkabala wa kimaelezo. Aidha, nadharia ya Umitindo ilitumika kwa lengo mahsusi la kwanza, sambamba na swali la utafiti la kwanza. Nadharia ya Mwitiko wa Msomaji ilitumika kwa lengo mahsusi la pili pamoja na swali la utafiti la pili. Nadharia zote hizo zilifanikisha vyema kazi yakukusanya, kuchambua na kuwasilisha data za utafiti.

Matokeo ya utafiti huu yameonyesha kuwatamthiliya ya *Mondlane na Samora* imetumia vipengele vya mtindo vinavyohusu matumizi ya lugha na vile vinavyohusu sajili mbali mbali kama vile barua, matangazo ya redio, mawasiliano ya simu na lugha ya shuleni na jeshini. Dhamira zilizojitokeza ni ukoloni, harakati za kupigania uhuru, umoja wa Bara la Afrika, umuhimu wa elimu, vita na mauaji, mapenzi na ndoa. Dhamira zote zililenga kusawiri uhalisia wa maisha ya bara la Afrika wakati wa ukoloni na wakati wa harakati za kutafuta uhuru kutoka kwa wakoloni. Mtafiti amegundua kuwa Emmanuel Mbogo amekuwa akichota matukio ya kihistoria katika jamii za Afrika kama msingi wa matumizi ya mitindo yake na dhamira zake katika tamthiliya anazozitunga.

# YALIYOMO

UTHIBITISHO ........ ii
HAKIMILIKI ........ iii
IKIRARI . ........ iv
TABARUKU ........ v
SHUKURANI ........ vi
ORODHA YA VIFUPISHO ........ vii
IKISIRI … ........ viii
YALIYOMO ........ ix
ORODHA YA MAJADWELI ........ xv

**SURA YA KWANZA: UTANGULIZI WA JUMLA ........ 1**

1.1 Utangulizi ........ 1
1.2 Usuli wa Mada ya Utafiti ........ 1
1.3 Tatizo la Utafiti ........ 3
1.4 Malengo ya Utafiti ........ 4
1.4.1 Lengo Kuu ........ 4
1.4.2 Malengo Mahsusi ........ 4
1.5 Maswali ya Utafiti ........ 5
1.6 Umuhimu wa Utafiti ........ 5
1.7 Mipaka ya Utafiti ........ 6
1.8 Muundo wa Tasnifu ........ 7
1.9 Hitimisho ........ 8

**SURA YA PILI: MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA MKABALA WA KINADHARIA .......... 9**
2.1 Utangulizi .......... 9
2.2 Ufafanuzi wa Istilahi Mbalimbali .......... 9
2.2.1 Dhana ya Mtindo katika Kazi za Fasihi .......... 9
2.2.2 Vipengele vya Kimtindo katika Fasihi .......... 12
2.2.2.1 Kiwango cha Maandishi au Grafolojia (Kiwango cha Utendaji) .......... 13
2.2.2.2 Kiwango cha Umbo .......... 14
2.2.2.3 Kiwango cha Kisarufi .......... 15
2.2.2.4 Kiwango cha Kisemantiki .......... 15
2.2.2.5 Mazungumzo na Mbinu za Uwasilishaji Usemi na Mawazo .......... 16
2.2.2.6 Usimulizi au Muundo wa Masimulizi .......... 16
2.2.2.7 Itikadi, Mtazamo na Mtindo .......... 17
2.2.2.8 Nadharia ya Umitindo .......... 17
2.2.3 Maana ya Dhamira .......... 20
2.3 Mapitio ya Kazi Tangulizi .......... 21
2.3.1 Mapitio ya Kazi Tangulizi kuhusu Mtindo na Dhamira katika Tamthiliya za Kiswahili .......... 22
2.3.2 Mapitio ya Kazi Tangulizi kuhusu Tamthiliya za Emmanuel Mbogo .......... 27
2.4 Pengo la Utafiti .......... 31
2.5 Mkabala wa Nadharia .......... 32
2.5.2 Nadharia ya Mwitiko wa Msomaji .......... 33
2.5.2.1 Waasisi wa Nadharia Mwitiko wa Msomaji .......... 33
2.5.2.2 Mihimili ya Nadharia ya Upokezi .......... 35

2.6 Hitimisho ........ 35

**SURA YA TATU: MBINU ZA UTAFITI ........ 37**

3.1 Utangulizi ........ 37

3.2 Eneo la Utafiti........ 37

3.3 Usanifu wa Utafiti ........ 38

3.4 Kundi Lengwa ........ 38

3.5 Sampuli na Usampulishaji........ 39

3.5.1 Sampuli na Mbinu ya Usampulishaji Lengwa........ 39

3.6 Aina za data zilizokusanywa ........ 40

3.6.1 Data za Awali ........ 40

3.6.2 Data za Upili........ 40

3.7 Mbinu za Ukusanyaji wa Data ........ 41

3.7.1 Mbinu ya Usomaji Makini Maktabani ........ 41

3.7.2 Mbinu ya Upitiaji wa Nyaraka ........ 42

3.8 Uchambuzi wa Data ........ 43

3.8.1 Mkabala wa Kimaelezo........ 43

3.9 Maadili ya Utafiti ........ 44

3.10 Vifaa vya Kukusanyia Data........ 45

3.10.1 Shajara na Kalamu........ 45

3.10.2 Kompyuta ........ 45

3.10.3 Vitabu, Tasnifu, Makala na Majarida........ 45

3.11 Hitimisho........ 46

**SURA YA NNE: UWASILISHAJI NA UCHAMBUZI WA DATA ZA UTAFITI ........ 47**

4.1 Utangulizi ........ 47

4.2 Usuli wa Mwandishi Emmanuel Mbogo ........ 47

4.3 Muhtasari wa Tamthiliya ya *Mondlane na Samora* ........ 50

4.4 Matumizi ya Mtindo katika Tamthiliya ya *Mondlane na Samora* ........ 51

4.4.1 Matumizi ya Lugha ........ 51

4.4.1.1 Matumizi ya Tamathali Semi ........ 52

4.4.1.1.1 Tashbiha ........ 52

4.4.1.1.2 Sitiari ........ 55

4.4.1.1.3 Tashihisi ........ 59

4.4.1.1.4 Taswira ........ 62

4.4.1.1.5 Takriri ........ 66

4.4.1.1.6 Tanakalisauti ........ 69

4.4.1.1.7 Mdokezo ........ 70

4.4.1.1.8 Nidaa ........ 73

4.4.1.1.9 Tafsida ........ 73

4.4.2 Vipengele vyengine vya Kimtindo katika Tamthiliya ya Mondlane na Samora ........ 75

4.4.2.1 Nyimbo ........ 76

4.4.2.2 Barua ........ 78

4.4.2.3 Hotuba ........ 79

4.4.2.4 Mawasiliano ya Simu ........ 80

4.4.2.5 Matangazo ya Redioni ........ 81

4.4.2.6 Rejista ya Jeshini ........ 82

4.4.2.7 Rejista ya Shuleni ........ 83

4.4.2.8 Misemo ........ 84

4.4.2.9 Kuchanganya ndimi/lugha ........ 85

4.4.3 Ubainishaji wa Dhamira katika Tamthiliya ya Mondlane na Samora ....... 88

4.4.3.1 Mauaji ........ 88

4.4.3.2 Ukoloni ........ 90

4.4.3.3 Ubepari na Ujamaa ........ 91

4.4.3.4 Usaliti ........ 93

4.4.3.5 Vita ........ 94

4.4.3.6 Umuhimu wa Elimu ........ 97

4.4.3.7 Umoja wa Bara la Afrika ........ 98

4.4.3.8 Mapenzi na Ndoa ........ 100

4.4.3.9 Ujasiri na Ushujaa ........ 103

4.4.3.1 Mawasiliano ........ 105

4.4.3.11 Uhuru ........ 106

4.5 Hitimisho ........ 111

**SURA YA TANO: MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO ....... 112**

5.1 Utangulizi ........ 112

5.2 Muhtasari ........ 112

5.2.1 Lengo Mahsusi la Kwanza ........ 114

5.2.2 Lengo Mahsusi la Pili ........ 115

5.3 Hitimisho ........ 115

5.4 Mapendekezo ........................................................................................ 116

5.4.1 Mapendekezo kwa Watafiti wengine ...................................................... 116

5.4.2 Mapendekezo kwa Viongozi .................................................................. 117

5.4.3 Mapendekezo kwa Jamii ........................................................................ 117

**MAREJELEO ............................................................................................. 118**

## ORODHA YA MAJADWELI

Jadweli 01: Muhtasari wa vipengele vya Lugha vilivyotumiwa kuwa Mtindo ..... 75

Jadweli 02: Vipengele vyengine vya Kimtindo katika Mondlane na Samora .. 86

Jadweli 03: Muhtasari wa Vipengele vya jumla vya Mtindo katika tamthiliya ya Mondlane na Samora ..... 87

Jadweli 04: Muhtasari wa Dhamira katika tamthiliya ya Mondlane na Samora ..... 111

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI WA JUMLA

## 1.1 Utangulizi

Sura hii imekusudia kubainisha mambo ya msingi katika utafiti huu usemao: *Kuchunguza Mtindo na Dhamira katika tamthiliya Mondlane na Samora*. Kwa kuzingatia mada hiyo ya utafiti, sura hii imejikita kufafanua vipengele vya msingi vifuatavyo: Usuli wa mada ya utafiti,tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, maswali yautafiti, umuhimu wa utafiti, vikwazo vya utafiti na utatuzi wake, maadili ya utafiti, mpango wa tasnifu na Hitimisho.

## 1.2 Usuli wa Mada ya Utafiti

Dhana ya mtindo katika kazi ya fasihi ni changamano miongoni mwa wahakiki wa fasihi. Wapo wanaouona mtindo kama ni upekee alionao mtunzi wa kazi ya fasihi. Wapo pia wanaoona kuwa mtindo ni namna ya kuwasilisha dhamira za mtunzi. Na wapo pia wenye mtazamo kwamba mtindo ni utafauti uliopo kati ya mtunzi mmoja na mtunzi mwingine katika kusanii kazi za fasihi.

Baadhi ya wataalamu kama vile Mohammed (2006), anamnukuu Kahigi (1997), akieleza mtazamo wa Leech na Short (1981), ambapo wawili hao wanautazama mtindo katika mitazamo miwili mikuu. Kwanza wanautazama mtindo kama uteuzi na pili wanauona mtindo kama tafauti. Mtindo kama uteuzi ni mtazamo unaosisitiza kuwa, mzungumzaji au mwandishi huteua vipengele maalumu miongoni mwa vipengele vya lugha na kuvitumia katika kazi yake.

Jilala (2016), katika kujadili dhana ya mtindo anashikilia kuwa kutokana na kila mtunzi kuwa na mtindo wake mahususi ndiko kunakopelekea kazi za mtunzi mmoja na mwengine kutafautiana japo kuwa kuna muathiriano wa kiwango kikubwa. Kwa misingi hiyo, Jilala (ktj) anaweka wazi kuwa mtindo ni tabia ya mtu binafsi ambayo inamtafautisha na mtu mwengine katika uzalishaji wa kazi za sanaa. Hii ni sifa ya pekee ambayo mtunzi huwa nayo hata kama mtu mmoja anaiga au kuathiriwa na mtunzi asilia.

Jilala (ktj), anamnukuu Enkvist (1973), akieleza kuwa mtindo ni kama nguo au vazi ambalo lipo kwa kuwa tu watu wanatakiwa kuliona kama ilivyo mazoea. Mjadala wa msingi hapa ni kwamba Je, mtindo ni kitu kinachoweza kuwepo ama kutokuwepo? Mantiki ya maelezo haya ni kwamba, mtindo unakuwepo tu pale unapohitajika. Kwa upande mwengine Enkvist (ktj), anasema mitazamo yote ya kiisimu kuhusu mtindo inaweza kujikita katika moja kati ya mitazamo mikuu mitatu. Kwanza mtindo ni ukiushi wa kaida zilizowekwa au zilizopo. Kutokana na mtazamo huu, uchambuzi wa mtindo hufanywa kwa kulinganisha vipengele vilivyomo katika matini inayoshughulikiwa na zile ambazo zitarejelewa kama kaida.

Katika mtazamo huu mtafiti ameweza kubaini tafauti iliyopo baina ya lugha na mtindo. Lugha ni jumla ya vipengele vyote anavyoweza kuvitumia mzungumzaji au mwandishi katika kufikisha ujumbe kwa jamii iliyokusudiwa, wakati mtindo ni vile vipengele vichache tu atakavyoviteua katika muktadha maalumu. Imani ya mtafiti juu ya dhana ya mtindo inakubaliana na Jilala (2016), kwamba mtindo katika kazi za fasihi hujibainisha katika sifa anuai kama vile; uteuzi wa msamiati wa mtunzi, miundo na mpangilio wa sentensi, uteuzi wa matumizi ya tamathali za usemi na

jazanda, usawiri wa wahusika, motifu na dhamira zinazokaririwa katika kazi za watunzi, usimulizi na mbinu za usimulizi wenyewe na sifa ya uakifishi.

Hivyo basi, mtafiti amesukumwa kufanya utafiti huu kwa sababu hadi sasa pamoja na kusoma kazi tangulizi mbalimbali hasa zilizohusiana na mitindo bado, mtafiti hajaona utafiti uliowahi kufanyika kwa lengo la kuchunguza mtindo na dhamira katika tamthiliya ya *Mondlane na Samora*. Pia, kutokana na umaarufu wa mtunzi huyu (Emmanuel Mbogo) katika fasihi ya Kiswahili, mtafiti ameona ipo haja ya kufanya utafiti huu, hasa kwa kuzingatia mitindo ambayo amekuwa akiibua mwandishi katika tamthiliya zake za hivi karibuni ikiwemo tamthiliya teule ya *Mondlane na Samora*.

Kwa sababu hizo, utafiti huu umeona bado pana pengo lililohitaji kufanyiwa uchunguzi. Kwa mantiki hiyo, katika kazi hii mtindo umetathminiwa kama ilivyojidhihirisha katika tamthiliya ya *Mondlane na Samora* ya Emmanuel Mbogo. Utafiti huu umeongozwa na nadharia ya Umitindo ili kuona namna mitindo ilivyodhihirika na nadharia ya Mwitiko wa Msomaji ili kuona dhamira ilivyojitokeza katika tamthiliya teule.

## 1.3 Tatizo la Utafiti

Watafiti kama vile Mlacha (1986), Bassnet (1993), Nyaosi (2008), Waliaula (2010), Onchangu (2013), Massoud (2013), Sibanda na Katemi (2014) na Jilala (2016) wamewahi kufanya utafiti uliohusiana na vipengele vya kimtindo na dhamira katika kazi za fasihi. Kwa mfano, Massoud (2013) alifanya utafiti linganishi wa tamthiliya ya *Mashetani* na *Kivuli Kinaishi* kwa kutumia mkabala wa Fasihi

Linganishi. Lengo kuu lilikuwa ni kulinganisha tamthiliya za *Mashetani* na *Kivuli Kinaishi* na sababu zilizofanya tamthiliya hizo zifanane na zitofautiane kimaudhui na kifani. Katika utafiti huo pamoja na kuchunguza vipengele vyengine vya kifani pia kipengele cha mtindo kilichunguzwa. Vilevile, Oiko (2017) alifanya uhakiki wa mtindo katika tamthiliya za Arege. Katika utafiti huo aligundua kuwa mtindo ni kipengele muhimu katika kusana kazi ya fasihi ambacho huamua jinsi ujumbe ulivyopelekwa na ulivyopokelewa. Katika kutalii machapisho mbalimbali mtafiti hakuona utafiti uliowahi kufanyika ukiwa na lengo la kuchunguza mtindo na dhamira katika tamthiliya ya *Mondlane na Samora* iliyoandikwa na Emmanuel Mbogo. Hivyo, mtafiti ameona ipo haja ya kufanya utafiti kwenye mada hii ya kuchunguza mtindo na dhamira katika tamthiliya ya *Mondlane na Samora* iliyoandikwa na Emmanuel Mbogo ili kupunguza mwanya ulioachwa na watafiti wengine.

## 1.4 Malengo ya Utafiti

Utafiti huu una malengo ya aina mbili: Lengo kuu na malengo mahsusi:

### 1.4.1 Lengo Kuu

Kuchunguza Mtindo na Dhamira katika tamthiliya ya *Mondlane na Samora* (2016) ya Emmanuel Mbogo

### 1.4.2 Malengo Mahsusi

Utafiti huu una malengo mahsusi yafuatayo:

i) Kubainisha vipengele vya mtindo katika tamthiliya ya *Mondlanena Samora.*

ii) Kubainisha dhamira katika tamthiliya ya *Mondlane na Samora.*

### 1.5 Maswali ya Utafiti

Utafiti huu uliongozwa na maswali yafuatayo:

i) Ni vipengele vipi vya mtindo vilivyotumiwa na Emmanuel Mbogo katika tamthiliya ya *Mondlane na Samora*?

ii) Ni dhamira zipi zilizojitokeza katika tamthiliya ya *Mondlane na Samora?*

### 1.6 Umuhimu wa Utafiti

Utafiti ni hazina muhimu katika maendeleo ya taifa lolote duniani. Kwa hivyo, umuhimu wa utafiti huu umejitokeza katika maeneo ya msingi yafuatayo:

**Kitaaluma:** Matokeo ya utafiti huu yatakuwa marejeleo muhimu kwa wasomi wa ngazi zote za taaluma ya fasihi. Wanafunzi, walimu na wasomi wengine wa kazi za fasihi ambao watayatumia matokeo ya utafiti huu kama ni sehemu ya marejeleo yao ya kukamilisha malengo ya tafiti zao watakazokuwa wanazifanya. Aidha, matokeo ya utafiti huu yatatumika kama sehemu ya kujiimarisha, ili kubainisha pengo la maarifa ambalo wao watalijaza katika tafiti zao. Matumaini ya mtafiti kuwa, wanataaluma ambao ni walimu, wahadhiri na wataalamu wengineo katika taaluma ya fasihi watauona umuhimu wa utafiti huu katika kuandika vitabu, makala na maandalio ya masomo ya kufundishia wanafunzi wao wa ngazi tafauti za elimu.

**Kinadharia:** Utafiti huu umetoa uthibitisho kwamba, nadharia za uhakiki wa fasihi zinapotumika kuhakiki kazi za fasihi huifanya kazi hiyo kuwa imara na yenye mashiko ambayo huaminika kitaaluma. Kupitia utafiti huu, watafiti wa baadaye wataona umuhimu wa kutumia nadharia ya Umitindo katika uchambuzi wa kazi za

fasihi. Hivyo, nadharia hii imejidhihirisha katika kazi hii kivitendo, jambo ambalo limetoa mwongozo katika uchambuzi wa kazi za fasihi hasa katika uwanja wa kutathmini mitindo kwa mkabala wa Nadharia ya Umitindo. Sambamba na nadharia hiyo, nadharia ya Mwitiko wa msomaji imetumika kwa lengo la kubainisha dhamira katika tamthiliya teule.

**Kisera:** Kwa watunga será nchini ni matumaini ya mtafiti hasa kwa upande wa dhamira, watazichukua ili ziingizwe katika será na zifanyiwe utekelezaji kwani utafiti huu umechunguza kwa kina na kubaini matatizo mengi ya kijamii ambayo yanaikumba kwa sasa kama vile: Masuala ya elimu, matabaka na umasikini, mauaji, vita, mapenzi na ndoa, ukombozi, usaliti, umoja wa Bara la Afrika. Pamoja na matatizo hayo yalivyojadiliwa, utafiti huu ulibainisha namna ya kuondokana na matatizo hayo katika jamii zetu na kuishi kimaendeleo kwa kurejelea kazi ya mwandishi mteule.

## 1.7 Mipaka ya Utafiti

Emmanuel Mbogo ni mwandishi mashuhuri na mwenye uwezo mkubwa katika fani ya uandishi wa kazi hasaza fasihi. Mbogo, ameandika tamthiliya nyingi. Miongoni mwa tamthiliya hizo ni pamoja na: *Giza Limeingia*(1980),*Tone la Mwisho* (1981), *Ngoma ya Ng'wanamalundi* (1988),*Morani* (1993), *Fumo Liongo* (2009), *Sundiata*(2011), *Nyerere na Safari ya Kanaani* (2015), *Wangari Maathai* (2015), *Sadaka ya John Okello* (2015), *Malkia Bibi Titi Mohamed* (2016) *Mondlane na Samora* (2016) na *Mtumwa hadi Siti binti Saad* (2018).

Mtafiti anaamini kuwa kazi za mwandishi huyu (Mbogo) zinapasa kuendelea kufanyiwa utafiti na wanazuoni mbalimbali kulingana na mada za wataalamu hao, lakini amebaini kuwa isingekuwa rahisi kufanya utafiti wa kuchunguza mitindo na dhamira katika tamthiliya zote za mtunzi huyu. Hivyo basi, utafiti huu umejikita katika kuchunguza mtindo na dhamira katika tamthiliya ya *Mondlane na Samora*. Mtafiti hatojihusisha na uchunguzi wa mtindo na dhamira katika tamthilia nyengine za Mbogo zaidi ya ile ya *Mondlane na Samora.*

## 1.8 Muundo wa Tasnifu

Utafiti huu wenye mada isemayo: *Kuchunguza Mtindo na Dhamira zilizobainishwa katika tamthiliya ya Mondlane na Samora* umegawanywa katika sura kuu tano (5) zifuatazo:

Sura ya Kwanza itakuwa niutangulizi wa Jumlaambayoimewasilisha vipengele muhimu vya kiutangulizi katika utafiti. Vipengele hivyo ni pamoja nautangulizi wa sura, usuli wa mada, tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti, mipaka ya utafiti,muundo wa tasnifu na hitimisho.

Sura ya Pili ni ile inayozungumzia Mapitio ya Kazi Tangulizi na Mkabala wa Kinadharia. Sura hii imewasilisha vipengele vifuatavyo: Utangulizi, ufafanuzi wa istilahi mbalimbali, mapitio ya kazi tangulizi na mkabala wa kinadharia. Nadharia zilizochaguliwa na kufafanuliwa ni Nadharia ya Umitindo na nadharia ya Mwitiko wa Msomaji na hitimisho.

Sura ya Tatu; Mbinu za Utafiti: Sura hii imechambua na kuwasilisha vipengele vifuatavyo: Utangulizi, eneo la utafiti, kundi lengwa, sampuli na usampulishaji, ukusanyaji wa data, mbinu za ukusanyaji wa data, mbinu za uchambuzi wa datana hitimisho.

Sura ya Nne; Uwasilishaji, na Uchambuzi wa Data za Utafiti: Sura hii imejadili vipengele vifuatavyo: Utangulizi, usuli wa mwandishi Emmanuel Mbogo, muhtasari wa tamthiliya ya *Mondane na Samora*. Baadae ni uwasilishaji na uchambuzi wa vipengele vya kimtindo vilivyotumika katika tamthiliya ya *Mondlane na Samora*.Pia uwasilishaji na uchambuzi wadhamira katika tamthiliya ya *Mondlane na Samora* umefanyika. Mwisho sura hii imemalizia kwa kutoa hitimisho.

Sura ya Tano; Muhtasari, Hitimisho na Mapendekezo:Sura hii imezungumzia vipengele vya msingi vifuatavyo: Muhtasari wa kila sura (sura ya kwanza hadi sura ya tano) kwa kuzingatia malengo na maswali ya utafiti husika. Mwisho utafiti huu umetoa mapendekezo kwa watafiti wengineo.

## 1.9 Hitimisho

Sura hii imeonesha uwasilishaji wa vipengele vya msingi vya kiutangulizi ambavyo vimetoa picha kamili ya utafiti huu. Hili linathibitika kupitia vipengele vya mada ya utafiti vilivyofafanuliwa ambavyo ni: Usuli wa mada ya utafiti, tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti, maadili ya utafiti, mpango wa tasnifu na Hitimisho. Sura itakayofuata ni Mapitio ya Kazi tangulizi na Mkabala wa Kinadharia.

# SURA YA PILI

# MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA MKABALA WA KINADHARIA

## 2.1 Utangulizi

Sura hii ni miongoni mwa sura muhimu katika utafiti huu. Hii ni kwa sababu sura imezingatia vipengele vya msingi ambavyo vitaendeleza kuufanya utafiti huu kuwa na thamani. Vipengele vya msingi katika sura hii ni vifuatavyo: Ufafanuzi wa istilahi mbalimbali, mapitio ya kazi tangulizi na mkabala wa kinadharia. Mwisho ni Hitimisho. Uchambuzi wa vipengele hivyo ni kama ifuatavyo:

## 2.2 Ufafanuzi wa Istilahi Mbalimbali

Utafiti huu umehusu mada inayohusu *Kuchunguza mtindo na dhamirakatika tamthiliya yaMondlanena Samora*. Katika utafiti huu, mtafiti amefafanua kwa kina istilahi mbalimbali muhimu ambazo zimetoa mchango mkubwa katika kuimarisha utafiti huu, ili kufikia malengo na maswali ya mada ya utafiti.

### 2.2.1 Dhana ya Mtindo katika Kazi za Fasihi

Dhana ya mtindo ni pana katika kazi ya fasihi. Mtindo umekuwa ukielezwa kwa mitazamo tofauti. Mathalan, Haji na wenzake (1981) wanasema kuwa mtindo katika kazi ya fasihi unaweza ukawa wa kihistoria ambapo mwandishi husimulia maisha yake mwenyewe au ya mtu mashuhuri katika jamii yake. Jambo la muhimu la kuzingatia hapa ni kuwa historia na fasihi ni taaluma mbili tafauti. Kwa hivyo, fasihi inapochagua kufuata mtindo wa historia, huwa hailazimiki kuifuata historia kama ilivyo, kwasababu fasihi ina uhuru wa kupitia njia zake ambapo historia haina budi kujifunga na matukio pamoja na tarehe zake kama zilivyo. Hivyo, fasili iliyotolewa na Haji na wenzake (ktj) imesaidia utafiti huu kuchunguza maswala ambayo

yameweza kuchambuliwa kama mtindo katika kazi za fasihi ambayo mtafiti wa kazi hii amejikita nayo katika uchambuzi. Dhana ya mtindo ni katika kipengele muhimu kilichozingatiwa katika mada ya utafiti huu.

Senkoro (1987) anaeleza kuwa mtindo katika kazi ya fasihi ni matumizi ya lugha ya aina kwa aina. Katika matumizi hayo mtafiti amegundua tamathali za usemi kama vile tashibiha, sitiari, tashihisi, taashira, taniaba, misemo, nahau, methali, uteuzi wa misamiati, miundo ya sentensi, ufundi wa kuwachora au kuwaeleza wahusika, mandhari na matukio pamojana utamu wa lugha yenyewe ilivyotumiwa.Pia, kuna masuala ya vipeo, ucheshi, matumizi ya komedia na tanzu za namna kwa namna zilivyotumika katika kazi husika.

Maelezo ya Senkoro (ktj) kuhusu dhana ya mtindo, kwa kiasi fulani, yameweza kuonesha vipengele vilivyohusiana na lugha ambavyo hutumiwa kama mtindo katika kazi ya fasihi. Imani ya mtafiti ni kwamba lugha ndiyo nyenzo kuu iliyoibua dhana ya mtindo katika kazi za kifasihi. Mawazo haya yametoa msukumo mkubwa kwa mtafiti wa kazi hii katika kuchanganua mtindo katika kazi teule ili kufikia malengo ya utafiti huu.

Njogu na Chimerah (2008) wanasema kuwa mtindo ni tabia ya utungaji inayopambanua mtunzi mmoja na mwengine. Ni dhana inayoelezea sifa inayobainisha kazi fulani na kuzitenga kazi nyenginezo. Pia, mtindo humtambulisha mtunzi aliyehusika. Madumulla (2009) anaeleza mtindo ni kipengele cha fani ambacho huonesha kazi ya sanaa namna ilivyosimuliwa. Kifaa kinachotumika zaidi katika kujadili mtindo wa fasihi ni lugha na jinsi ilivyotumika. Sambamba na hayo,

ametilia mkazo matumizi ya lugha na masimulizi akiamini kuwa hivyo ndivyo vipengele vikuu vilivyojenga mtindo. Madumlla kwa msingi huo amempatia mtafiti wa kazi hii uelewa kuhusu dhana hii, kuwa mtindo katika kazi ya fasihi unaweza kubainika kwa kuichunguza kazi ya fasihi kupitia kipengele cha masimulizi na matumizi ya lugha.

Pamoja na mchango mkubwa wa Madumulla (ktj) katika dhana hiyo ya mtindo, mtafiti amebaini kuwa bado iko haja ya kuijadili dhana ya mtindo  kwa kina zaidi. Hii ni kwa sababu mtafiti wa kazi hii kwa vidokezo alivyovipata nyuma amebaini kwamba,dhana ya mtindo ni zaidi ya matumizi ya lugha na masimulizi. Dhana hiyo katika kazi ya fasihi imejumuisha vipengele kadhaa vya lugha na masimulizi vikiwa ni vipengele viwili tu kati ya hivyo. Kwa mtazamo wa mtafiti vipengele vyengine muhimu vya kimtindo ni pamoja na mianzio na miisho ya kifomula katika  kazi za fasihi, uchotaji wa tanzu za fasihi simulizi ndani ya fasihi andishi, matumizi ya vipengele vya fasihi simulizi kama vile wahusika watambaji, motifu za safari, uhalisiajabu pamoja na usemezano wa wahusika. Vipengele hivyo bado havijahusishwa na Madumulla (ktj).

Mapitio haya kuhusu maana ya mtindo, mtafiti anaweza kuhitimisha kwa kusema kuwa mtindo katika kazi ya fasihi ni upekee wa msanii uliojitokeza katika kazi yake ambao humtafautisha na wasanii wengine. Tofauti hizi hudhihirika katika matumizi ya tanzu ndani ya utanzu, usawiri wa wahusika, motifu za safari, matumizi ya tamathali za usemi, usawiri wa mandhari, upangaji wa matukio, matumizi ya mbinu za uhalisiajabu pamoja na ujengaji wa maudhui katika kazi za fasihi.

### 2.2.2 Vipengele vya Kimtindo katika Fasihi

Senkoro (2001) anasema mtindo katika kazi ya fasihi ni ile namna ambayo msanii hutunga kazi hiyo na kuipa sura ambayo kifani na kimaudhui huainisha kanuni au kawaida zinazofuatwa kama zilizopo (za kimapokeo) au za kipekee. Vilevile Senkoro (ktj) anaueleza mtindo kama ni kaida zinazofuata jadi ya utanzu husika. Kwa hali hii ipo haja ya mawazo haya kujadiliwa zaidi.

Jilala (2016) anasema mtindo huonesha sifa ya kipekee aliyonayo mtunzi mmoja na mtunzi mwengine. Mtindo huweza kuwatafautisha watunzi wa kipindi, wakati na miongo tofauti na kuonesha sifa bainifu za kisanii zinazoweza kuwatafautisha wasanii, msanii binafsi na wasanii wa kipindi fulani. Sambamba na hayo, anaeleza kuwa mtindo katika kazi za fasihi hujibainisha katika vipengele anuai kama vile; uteuzi wa msamiati wa mtunzi, miundo na mpangilio wa sentensi, uteuzi wa matumizi ya tamathali za usemi na jazanda Vipengele vyengine vinavyohusu mtindo ni usawiri wa wahusika, motifu na dhamira zilivyokaririwa katika kazi za watunzi, usimulizi na mbinu za usimulizi wenyewe na sifa ya uakifishi. Kwa mantiki hiyo, ili uweze kujua tafauti ya mwandishi mmoja na mwengine ilipasa kuvibaini vipengele vya kimtindo vya msanii huyo na jinsi vinavyomtafautisha msanii huyo na wasanii wengine.

Mtafiti wa kazi hii kama alivyokwishaeleza hapo juu, Senkoro (1987) ametilia mkazo kuwa, mtindo katika kazi ya fasihi ni matumizi ya lugha ya namna tofauti tofauti. Matumizi hayo yanajumuisha tamathali za usemi kama vile tashibiha, sitiari, tashihisi, taashira, taniaba, nakadhalika. Vipengele vyengine vya mtindo Senkoro amevitaja kuwa ni misemo, nahau, methali, uteuzi wa misamiati, miundo ya sentensi,

ufundi wa kuwachora au kuwaeleza wahusika, mandhari na matukio pamoja na utamu wa lugha yenyewe itumiwavyo. Pia, kuna masuala ya vipeo pamoja na ucheshi, matumizi ya komedia na tanzu katika tanzu namna zilivyotumika katika kazi husika.

Maelezo ya Senkoro (ktj) yameingia ndani zaidi kuhusiana na dhana ya mtindo kama ilivyokwishaelezwa hapo juu. Maelezo haya yameweza kutuonesha jinsi mtindo katika kazi ya fasihi unavyotawaliwa na matumizi ya vipengele mbalimbali. Hivyo basi, mtafiti wa kazi hiiamefaidika sana na mawazo hayo,kwa sababu mtafiti amebaini kupitia maelezo haya vipengele vya kifani ambavyo vinahusishwa na mtindo katika kazi za kifasihi. Vipengele hivyo vimechunguzwa na mtafiti ili kubaini jinsi vilivyojidhihirisha katika tamthiliya teule.Kimsingi mjadala wa vipengele vya mtindo kama vilivyojadiliwa na Senkoro (1987) na Jilala (2016), vimetumiwa katika kukusanya data za utafiti huu kama kielelezo cha namna ya kukusanya data kuhusiana na matumizi yamtindo katika tamthiliya teule.

Murumba (2013) anawanukuu Leech (1969), Simpson (2004) na Wamitila (2008), wakieleza vipengele muhimu vinavyopaswa kuchunguzwa katika matini kwa kutegemea dhana ya Umitindo. Uchambuzi huo unajidhihirisha kama ifuatavyo:

#### 2.2.2.1 Kiwango cha Maandishi au Grafolojia (Kiwango cha Utendaji)

Kiwango hiki kinahusisha vipengele vya kifonetiki, kifonolojia na kigrafolojia. Kinahusu jinsi lugha inavyotamkwa na kuandikwa. Kwa kawaida, kila kazi ya fasihi huwa katika maandishi fulani na mahsusi tena huwa katika abjadi zinazoeleweka na kuzoeleka na walengwa. Hata hivyo, matini za kifasihi huweza kuwa na sifa za

kimaandishi ambazo zinachimuzwa na hivyo kutilia uzito kiwango hiki cha ukiushi. Ukiushi huu unahusu mambo yafuatayo; kubadilisha matamshi ya maneno k.v miujiza liwe "miuza"; matumizi ya herufi kubwa kwa njia isiyo ya kawaida; kutumia herufi ndogo mahali pa herufi kubwa, matumizi ya herufi za mlazo/italiki; mpangilio wa aya (au ukosefu wake) na matumizi ya viwakifishi kama koma, alama ya hisi, koloni, na vistari (Leech 1969, Wamitila 2008).

### 2.2.2.2 Kiwango cha Umbo

Matumizi ya lugha kwa kawaida huhusisha uteuzi wa maneno au msamiati unaotumiwa. Kwa kuwa fasihi inatumia lugha kujieleza, vipengele ambavyo huhusishwa katika uteuzi huu ni vingi. Kuna kiwango cha kimsamiati (kileksia), matumizi ya lahaja, na kiwango cha rejesta/sajili (yaani, jinsi lugha inavyotumiwa katika muktadha maalum). Ukiushi wa kimsamiati unahusu yafuatayo: kubuni maneno mapya kwa kutumia minyambuliko isiyo ya kawaida na ubuniji huu hutokea kwa kutafuata kanuni za kisarufi km. maskini –"maskinisha‟, dhambi – "ikanidhambi‟. Pia kuna matumizi ya maneno ya kale/kizamani kama kutumia *munyu* (chumvi), *swi* (samaki) na *nyuni* (ndege), matumizi ya inkisari na mazida; kuchanganya ndimi/ kuhamisha ndimi na matumizi ya maneno ya kigeni kama ya Kiingereza au Kilatini. Suala la uteuzi halihusishwi na maneno peke yake. Mwandishi pia anafanya uteuzi wa wahusika anaowatumia kwenye kazi yake; usimulizi anaoutumia na mtazamo wake; na mada anayoishughulikia. Kwa mfano, uteuzi wa mhusika anayepatikana katika mazingira au muktadha maalum unamaanisha kuwa lazima lugha yake iafikiane na mazingira hayo.

#### 2.2.2.3 Kiwango cha Kisarufi

Kiwango hiki ni nguzo ya matamshi ya kiisimu na msingi mkuu wa lugha unaodhibiti matumizi ya lugha yenyewe. Huwa inajumuisha viwango vya kimofolojia na kisintaksia.

Hushughulikia mpangilio wa maneno katika sentensi kwa kubainisha visehemu vyake, ambavyo huwa na dhima maalumu. Ukiushi huu huhusisha masuala kama kubananga sarufi; matumizi ya anafora - neno moja kuanza kila mstari hasa katika nyimbo na mashairi na kurudiwarudiwa kwa sentensi au kifungu. Huwepo pia, ukiushi wa kilahaja na matumizi ya rejesta/sajili. Kwa ujumla, huzingatia ukiushi katika muundo wa kawaida wa matumizi ya lugha, urefu wa sentensi (fupi au ndefu) na sentensi zenye dosari. (Leech 1969 na Wamitila 2008:512).

#### 2.2.2.4 Kiwango cha Kisemantiki

Kiwango hiki kinahusu lugha ya kitamathali na miundo ya lugha ambayo ni sifa muhimu ya kuchunguza matini ya kifasihi tunapotumia nadharia ya Umitindo. Ni matumizi ya lugha yanavyoathiri maana kwa njia fulani. Ukiushi wa aina hii unahusu matumizi ya maneno na jinsi maana hiyo inavyofasiriwa katika hali za kawaida. Mara nyingi huhusisha matumizi ya maneno kwa njia ambazo si za kawaida kimaana. Huwepo matumizi ya tamathali za usemi; mbinu ya kinaya/kejeli; mbinu ya kweli-kinzani (paradoksi); mbinu ya oksimora (tanakuzi) km. anwani *Kiza katika Nuru* ya S.A. Mohamed; na mbinu ya sitiari kama ujana ni moshi. Pia, huhusisha matumizi ya jazanda, yaani lugha ya picha aidha za kimaelezo au za kiishara (ambazo si taswira au picha tu bali zina ujumbe wa ziada) (Wamitila 2008:518).

### 2.2.2.5 Mazungumzo na Mbinu za Uwasilishaji Usemi na Mawazo

Katika kiwango hiki, mhakiki wa kimtindo anafaa kuchunguza mazungumzo au usemezano baina ya wahusika na mbinu nyingine zinazotumiwa katika mazungumzo hayo kwa lengo la kuwasilisha usemi na mawazo ya wahusika (Wamitila 2008). Murumba (2013), anamnukuu Ngara (1982), akieleza kuwa wahusika wanawakilisha matumizi ya lugha ya kawaida katika jamii kama binadamu wa kawaida. Aghalabu, binadamu hutumia lugha kwa njia ambazo zinatofautiana katika viwango vya misamiati, miundo ya sentensi, mkazo, n.k. Tofauti hizi za kimatumizi zinaonekana katika tungo za kifasihi. Ni jukumu la mhakiki kuangazia tofauti zilizoko katika matumizi ya lugha miongoni mwa wahusika. Ikiwa wahusika ni wasomi au walioelimika huenda wakaongea Kiswahili sanifu kutokana na athari za elimu waliyopata. Wenye elimu ndogo huenda wakaathiriwa na lugha ya kwanza. Huwepo matumizi ya lugha za kigeni kama Kiingereza na Kilatini. Kulingana na Ngara (1982), kutofautisha wahusika katika misingi ya matumizi ya lugha ni sifa nzuri ya uandishi.Matumizi yao daima huwa yanaakisi matumizi ya lugha katika jamii.

### 2.2.2.6 Usimulizi au Muundo wa Masimulizi

Usimulizi hurejelea hali ya kuwepo au matukio yanayosimuliwa katika hadithi, na kuleta mabadiliko. Uchunguzi wa muundo wa usimulizi unahusika kimsingi na uchunguzi wa ploti au msuko wa kazi husika. Matukio na visa katika matini ya kazi ya kifasihi lazima yafuate ruwaza fulani. Msuko huweza kuwa wa moja kwa moja au changamano. Mpangilio wa matukio huendana na wakati toka mwanzo hadi mwisho au huwepo mpangilio wa kwenda mbele na nyuma (mbinu rejeshi). Vilevile, kuna utoaji wa maelezo/masimulizi. Mara nyingi, huwepo sauti inayotoa masimulizi aidha

ya mwandishi au ya mhusika mmojawapo. Masimulizi huweza kutolewa katika nafsi ya kwanza, au katika nafsi ya tatu ambapo mhakiki atabainisha sifa hizi za kimtindo na athari inayoleta kwa wanaosimuliwa. Mara nyingine nafsi zote mbili (ya kwanza na ya tatu) hutumiwa ili kuleta athari fulani.

#### 2.2.2.7 Itikadi, Mtazamo na Mtindo

Mwandishi huchukua mkabala fulani kuhusu anayoyazungumzia na mtazamo huu unaweza kuwa na mchango mkubwa kwenye upokezi wa maneno anayoyasema au jinsi mlengwa anavyoyaelewa au kukipokea kisa kinachosimuliwa. Mtazamo ni dhana muhimu katika uchanganuzi wa mitindo ya matini. Vilevile, ni muhimu kuchanganua mwelekeo wa kimsimamo au kimawazo (yaani itikadi) unaochukuliwa na msimulizi wa kazi inayohusika. Lugha huwa ni nyenzo muhimu ya kubainisha au hata kuchimuza itikadi hiyo. Mchunguzi wa kimitindo anastahili kuchunguza jinsi uteuzi wa maneno au uteuzi wa kiisimu unavyochangia katika kuiangazia itikadi hiyo (Wamitila 2008). Katika utafiti huu nadharia ya Umitindo ilitumika katika uchambuzi wa data zinazohusu vipengele vya mtindo katika tamthiliya ya *Mondlane na Samora* kwa mnasaba wa kufanikisha lengo mahsusi la kwanza na swali la kwanza la utafiti huu wenye mada inayohusu *Kuchunguza Mtindo na Dhamira katika tamthiliya ya Mondlane na Samora*.

#### 2.2.2.8 Nadharia ya Umitindo

Murumba (2013), anaeleza kuwa mwasisi wa Nadharia ya Umitindo ni Geoffrey Leech (1969) ambaye alipokuwa akiandika tasnifuyake ya uzamili, alipenda lugha ya fasihi, ambayo kwayo aliandika makala mbili, mnamo mwaka 1965 na mwaka 1966.

Kwa mara ya kwanza, hapo isimu ya lugha ilihusishwa na usomaji/ ufundishaji wa lugha ya fasihi. Mtazamo huu ulizua kutokuelewana baina ya wasomi wa fasihi na wa isimu. Ni wakati huu ambapo Leech alionelea mwafaka upatikane baina ya mitazamo – husika miwili; yaani ule wa kiisimu na ule wa kifasihi. Kutokana na maoni ya wanaisimu na wahakiki walioshikilia kuwa taaluma mbili hizi; uhakki wa kifasihi na kazi za kiisimu hutafautiana na kuwa hazina uhusiano wowote, Leech alipata motisha wa kuandika kitabu chake, *A Linguistic Guide to English Poetry* (1969), ambacho kilionesha suala la mitindo katika kuchanganua matini za kifasihi.

Murumba (2013), akimnukuu Leech (1969) anasema kuwa umitindo kama taaluma katika uwanja wa fasihi, inafungamanisha uhakiki wa kifasihi na kiisimu ingawa haijisimamii kivyake. Msamiati mpana wa kimsingi wa uhakiki wa kifasihi kama vile; sitiari, taswira, kinyume, kinaya/ kejeli, usambamba na jazanda hauwezi kufafanuliwa bila ya kurejelea dhana za kiisimu. Kwa hiyo, kama msingi wa kutumia taaluma za kifasihi na za kiisimu, umitindo ni uwanja ambamo masuala ya kushughulikiwa.

Kulingana na Leech (ktj), malengo ya stadi za umitindo ni fasihi pamoja na maumbo mengine ya matini zilizoandikwa katika nyanja za matangazo ya biashara, utamaduni, siasa au dini. Kwamba, umitindo pia hujaribu kubainisha kanuni za kuelezea uteuzi mahsusi unaofanywa na wahusika katika matumizi yao ya lugha kuhusu mambo ya kijamii, utoaji na upokeaji wa maana, uhakiki wa kidiskosi na wa kifasihi.

Sifa nyingine za umitindo alizozitaja Leech (ktj) ni pamoja na matumizi ya dayalojia au mazungumzo yanayohusisha lafudhi za kimaeneo na lahaja za wazungumzaji, lugha elezi na sarufi k.m sauti, urefu wa sentensi na rejesta. Umitindo huweza kutumiwa kubainisha uhusiano uliopo baina ya umbo na athari zake katika kiwango fulani cha lugha. Akizungumzia lugha katka Fasihi, Leech (ktj) anasema kuwa, athari ya matini yoyote ile huamuliwa kwa kiasi kikubwa na mtindo. Kwamba, mtindo ni njia na jinsi lugha inavyotumiwa, nao mtindo haujabanwa tu katika fasihi, ila ni sehemu ya usemi wowote ule kwa sababu katika kila muktadha, msemaji huchagua jinsi ya kuzungumza.

Kwa muhtasari, nadharia ua Umitindo hutmiwa kurejelea mkabala wa uchanganuzi wa matini za kifasihi kwa kuchunguza mtindo kwa njia ya kisayansi. Kwa kufata misingi na taratibu za kitaaluma na huweza kuelezwa kama na nadharia iliyo katikati ya fasihi na isimu. Kimsingi, nadharia hii ina mwelekeo wa kifani na inadhamiria kuchunguza mtindo wa kinachosemwa (maudhui) na jinsi kinavyosemwa (fani). Nadharia ya Umitindo imepitia hatua kadhaa kufika sasa. Wamitila (2003) anasema dhana hii hutumiwa kurejelea taaluma inayohusu uchunguzi wa lugha na matukio mbali mbali katika kazi za kifasihi. Ni taaluma ilyoko kati ya uchunguzi wa lugha na uchunguzi wa fasihi au jinsi lugha inavyotumiwa katika matini au kazi za kifasihi. Umitindo huweza kuhusisha uchunguzi wa sifa za kimtindo zinazojitokeza katika kazi fulani na zinzomtambulisha mwandishi anayehusika.

Nadharia ya Umitindo imepitia katika viwango kadhaa. Leech (1969) ameoredhesha aina kadhaa za ukiushi wa kaida za matumizi ya lughaambao hutokea katika mtindo wa kazi za kifashi. Viwango hivyo vya ukiushi ni; ukiushi wa kimsamiati, ukiushi wa

kisarufi, ukiushi wa kilahaja, ukishi wa sajili/rejesta, ukiushi wa kifonolojia, ukiushi wa kimaandishi/kigrafolojia, ukiushi wa kimapisi/kihistoriana ukiushi wa kisemantiki.

Wamitila (2008) anamnukuu Simpson (2004), akivielezea vipengele vinavyofaa kuchunguzwa katika kazi za kifasihi na mhakiki ambaye anatumia mwelekeo wa kihakiki wa mitindo. Vipengele hivyo ni lugha za kitamathali na mtindo, uteuzi na mtindo, sarufi na mtindo, usimulizi na mtindo, uchimuzi na mtindo, itikadi, mtazamo na mtindo; muwala , mshikamano na mtindo, mazungumzo na mbinu za uwasilishaji usemi na mawazo.  Hivyo katika sehemu ifuatayo mtafiti amefanya ufafanuzi wa Dhamira zilizojitokeza katika tamthiliya teule.

### 2.2.3 Maana ya Dhamira

Ndungo na Wafula (1993) wanaeleza kwamba dhamira ni sehemu moja tu ya maudhui ya kazi ya fasihi. Hivyo dhamira ni kiini cha suala linalozungumzwa na msanii katika kazi ya fasihi. Waandishi hawa wamezigawa dhamira katika makundi mawili, nayo ni dhamira kuu na dhamira ndogo ndogo. Kwa mfano, wanaeleza kuwa mwandishi  anaweza kuwa na dhamira ya vita vya ukombozi, dhamira ya ujenzi wa jamii, dhamira ya utu bora, uvivu na ulanguzi.

Mawazo ya Ndungo na Wafula (ktj) yamemsaidia sana mtafiti wa kazi hii kubaini dhamira katika kazi ya utafiti huu unaolenga tamthiliya ya *Mondlane na Samora.* Hii ni kutokana na kwamba, waandishi hao wametoa mifano ya dhamira zilizojitokeza katika kazi za fasihi. Kwa hivyo, mtafiti amechukua maelezo hayo kama ni hoja ya

kuanzia katika kutafiti wa dhamira katika kazi iliyotafitiwa kama zilivyojitokeza kupitia mitindo mbali mbali.

Sengo (1999) anaelezea kuwa dhamira ni sehemu ya maudhui, na maudhui ni yale yasemwayo na maandishi ya kazi za fasihi. Dhamira ya mtunzi wa asili yaweza kuwa ni mgogoro wa ndoa, maandishi yakatoa dhamira kadhaa juu ya kugongana wenyewe kwa wenyewe viongozi wa juu wa serikali.

Mawazo ya Sengo (ktj) na yale ya Ndungo na Wafula (ktj) kuhusiana na dhamira katika utafiti huu yameonekana yana mantiki kubwa. Mtafiti amekubaliana na mawazo hayo. Hata hivyo, ufafanuzi wa Sengo (ktj) umeingia ndani zaidi kuhusiana na suala la dhamira, kwa sababu amefafanua zaidi kwamba mgogoro ndiyo unaoibua dhamira katika kazi za fasihi.

## 2.3 Mapitio ya Kazi Tangulizi

Mapitio ya kazi tangulizi ni usomaji wa kina wa maandishi ya watafiti watangulizi, uliofanywa na mtafiti kwa ajili ya uchambuzi kuhusu suala la utafiti. Mapitio ya kazi tangulizi lazima yaoneshe uhusiano wa maandishi hayo na mada ya utafiti. Katika mapitio ya kazi tangulizi huoneshwa pia nadharia zilizotumika katika uchambuzi wa data. Aidha, mapitio ya kazi tangulizi ni maarifa yaliyopatikana kwa kina kutokana na maandishi ya huko nyuma ambayo hufananishwa na taarifa hai zilizopatikana ndani ya utafiti wa sasa (Enon, 1998). Katika utafiti huu mapitio ya kazi tangulizi yamegawanywa katika makundi mawili makubwa: Mosi; Mapitio ya kazi tangulizi kuhusu Mtindo na Dhamira katika tamthiliya za Kiswahili. Pili; Mapitio ya kazi tangulizi kuhusu tamthiliya ya Emmanuel Mbogo.

### 2.3.1 Mapitio ya Kazi Tangulizi kuhusu Mtindo na Dhamira katika Tamthiliya za Kiswahili

Malengo ya utafiti huu yameelekezwa katika msingi mkuu wa dhana ya Mtindo na Dhamira katika tamthilia ya *Mondlane na Samora.* Hivyo basi mapitio ya kazi tangulizi yaliyozingatiwa na kufafanuliwa yamehusu mtindo na dhamira kama ifuatavyo:

Mugambi (1980) amehakiki *"Maudhui katika tamthiliya zilizochapishwa nchini Kenya za kipindi kati ya mwaka 1957 hadi 1981".* Katika utafiti wake ameonyesha mbinu za kifani walizotumia watunzi katika tamthiliya hizo ili kuendeleza maudhui. Kwa upande wa maudhui, mtafiti aligundua dhamira mbalimbali kama vile: Udhalimu, usaliti, ukombozi, nafasi ya mwanamke katika jamii, utetezi wa haki za wanyonge na ukoloni mamboleo. Aidha, ameonesha mandhari, wahusika, matumizi ya lugha hasa jazanda na tamathali zasemi kama mbinu muhimu katika ujenzi wa maudhui ya kazi za wakati huo.

Kwa hakika kazi ya Mugambi (ktj) ilikuwa ni tafauti na tamthiliya ambayo utafiti huu umehusu, hata hivyo kazi hiyo imekuwa na umuhimu mkubwa katika kufikia malengo ya utafiti huu. Hii ni kutokana utafiti huo umezingatia kwa kina kipengele cha Maudhui kama ndio roho yake. Sambamba na dhamira zilichambuliwa vyema ikiwa ni sehemu nyeti katika kazi hiyo.  Kwa mnasaba huo, kipengele cha dhamira kimekuwa ni hazina muhimu ya kuimarisha utafiti huu kwasababu ni miongoni mwa lengo la utafiti wenye mada; *Kuchunguza Mtindo na Dhamira katika tamthiliya ya Mondlane na Samora.*

Musyoka (1996) alihakiki *"Fani katika tamthiliya nne za Jay Kitsao*, *Uasi* (1980) *Malimwengu Ulimwengu* (1983), *Bibi Arusi* (1983), *na Tazama Mbele* (1987)". Katika utafiti huo, alifanya uchambuzi wa vipengele vya fani katika usambamba wa msingi na kiada za utanzu wa tamthiliya. Anaendelea kueleza kuwa fani niuumbaji na ufundi wa kipekee ambao huhusishwa na mtindo wa muandishi mahsusi.Ametathmini umbuji wa msanii na jinsi fani ilivyoathiri na kuchangia katika kiwango cha kisanaa na kazi hizo. Uchambuzi huo uliongozwa na Nadharia ya Mwingilianomatini.

Utafiti wa Musyoka (ktj) umekuwa na manufaa makubwa katika kusukuma mbele utafiti huu. Hii imetokana na kazi hiyo kufanya uchambuzi wa vipengele vya mtindo ambao ni miongoni mwa msingi mkuu katika utafiti huu. Kwa mantiki hii mtafiti amepata uelewa wa namna ya kufanya uchambuzi wa data za kimtindo zilizokusanywa. Hali hiyo imemuwezesha mtafiti kufikia hatua nzuri ya kutimiza malengo na maswali ya mada ya utafiti kwa kurejelea tamthiliya ya *Mondlane na Samora*.

Sarara (1997) amechanganua "*Maudhui katika tamthiliya za Said Ahmed Mohammed.*Tamthiliya zilizotafitiwa ni: *Pungwa* (1988), *Kivuli Kinaishi*(1990) na *Amezidi* (1995)".Katika maudhui ya utafiti huo, mtafiti amechanganua dhamira zilizolenga jamii kwa upande wa kisiasa kama vile: Kudhulumiwa kwa wanawake, mapambano ili kuleta  ukombozi, rushwa na ufisadi pamoja naumasikini miongoni mwa jamii.

Utafiti wa Sarara (ktj) umemsaidia sana mtafiti.Hii ni kwa sababu kipengele cha dhamira zilizohakikiwa zimeongeza mwamko na kuupa mwelekeo mzuri zaidi utafiti huu. Kwa minajili hiyo, dhamira zilizochambuliwa ni tegemeo kubwa la mtafiti katika utafiti wake. Hali hii imemuongoza mtafiti kukitumia kipengele cha dhamira kama hatua mojawapo muhimu ya kufikia mada husika lakini kupitia tamthiliya teule ya *Mondlane na Samora.*

Wafula (1999) alifanya "*Uchambuzi wa mtindo wa majaribio katika tamthiliya ya Amezidi".* Katika uchambuzi wake anahitimisha kwa kusema kuwa mtindo wa tamthiliya ya *Amezidi* umesawiri utunzi mpya katika tamthiliya ya Kiswahili. Mbali na mtunzi kutumia vipengele vya kifasihi vinavyotokana na "sanaa tendaji inayodunisha."Ametumia taswira kama sehemu ya mtindo ili kuelezea hali mbovu katika bara la Afrika. Kimaudhui tamthiliya ya *Amezidi* imeonesha ukame na utupu uliosababishwa na uongozi wa bara la Afrika. Msanii ameeleza kwamba fikra potofu ndizo zilizosababisha hali ngumu ya Afrika.

Uchambuzi huu wa Wafula (ktj) pia ulitoa mchango katika kufikia malengo ya utafiti huu. Kwanza tuliona namna data za mtindo zilivyowasilishwa katika kazi za fasihi. Pia, tuliona namna tamthiliya zilivyobeba mawazo ya mtunzi yaliyoihusu jamii na namna mawazo hayo yalivyojidhihirisha katika miktadha ya kifasihi. Kwa hivyo utafiti huu uliotumia mawazo hayo na hatimae ulikamilisha malengo ya utafiti huu.

Too (2011) alitafiti "*Tamthiliya ya Nguzo Mama (1982), ya Penina Muhando".*Katika utafiti huo alitumia nadharia ya Umuundona Simiotiki.Uchambuzi

wa kazi hiyo, ulijikita katika uchanganuzi wa vipengele vya lugha na namna vilivyotumiwa na msanii katika tamthiliya hiyo ya *Nguzo Mama.*

Utafiti wa Too (ktj) umekuwa na umuhimu katika utafiti huu kutokana na kutoa muongozo wa namna ya kufanya uchambuzi wa data zinazohusiana na vipengele vya lugha katika fasihi. Kwa sababu vipengele vya lugha vilivyotumiwa katika utafiti huo wa Too (ktj) baadhi yao vimetumika kuwa ni miongoni mwa vipengele vya mtindo katika utafiti huu. Hivyo basi mtafiti amejifunza namna vipengele hivyo vilivyoweza kufanyiwa uchambuzi na hatimae kutoa majibu ya maswali ya utafiti huu wenye mada: *Kuchunguza mtindo na dhamira katika tamthiliya ya Mondlane na Samora.*

Jilala (2016) alilinganisha tamthiliya ya *Mashetani* (1971) na *Mfalme Adepode* (1971). Katika utafiti huo, ulihusisha vipengele vya kimtindo na dhamira katika tamthiliya za *Mashetani* na *Mfalme Adepode*.Matokeo ya uchambuzi wa vipengele hivyo vya kimtindo ni pamoja na: Motifu ya safari, matumizi ya lugha na hadithi ndani ya hadithi.

Utafiti wa Jilala (ktj) umemuongezea maarifa makubwa mtafiti kwa lengo la kuiendea vyema kazi yake ya utafiti. Hii ni kwa sababu vipengele vya kimtindo na dhamira vilitumika katika uchambuzi wa utafiti huo kwa kina. Sambamba na hayo vipengele hivyo ndio hazina na raslimali pekee ambayo imeuongoza na kuusukuma mbele utafiti huu kwa kuzingatia malengo na maswali ya mada ya utafiti isemayo: *Kuchunguza mtindo na dhamira katika tamthiliya ya Mondlane na Samora.*

Oiko (2017) alifanya uchunguzi wenye mada *"Uhakiki wa Mtindo katika Tamthiliya za Arege."*Katika utafiti huo aligundua kuwa mtindo huamua jinsi ujumbe unavyopelekwa kwa hadhira iliyokusudiwa. Vilevileametumia mtindo wa kinaya katika kusanii kazi yake. Mtindo huu wa kinaya ameutumia ili kuwakejeli Waafrika ambao hadi leo wanang`ang`ania ukoloni mamboleo.

Kazi hii ya Oiko (ktj) ilikuwa na faida kubwa kwa utafiti huu. Hii ni kwa sababu kazi hii ilifanya uchambuzi wa vipengele vya mtindo kama ilivyo katika utafiti huu.Pia, utafiti wa huoulichambua namna mtindo wa kinaya unavyoibua dhima mbalimbali. Katika kazi hiyo kumeelezewa kinaya na nmana ilivyoibua mawazo ya mtunzi katika miktadha ya kifasihi. Hivyo basi utafiti huo umezidisha hamasa ya kuchunguza mtindo na dhamira katika tamthiliya ya *Mondlane na Samora* kama ilivyo mada ya utafiti.

Naye Mnenuka (2018) alifanya uchambuzi unaohusu *"Kuchunguza Fomula ya Tamthiliya ndani ya Tamthiliya"*. Katika uchunguuzi wake alitumia mifano kutoka tamthiliya *za Jogoo Kijijini*, *Ngao ya Jadi* na *Lina Ubani*za mwandishi Ebrahim Hussein. Katika maelezo yake amesema kwamba mtunzi wa tamthiliya hufungwa na mtindo maalumu. Kwa mantiki hiyo mitindo mbalimbali itaendelea kutumiwa na watunzi wa tamthiliya kadri muda unavyoendelea. Pia, ameonyesha namna ya vipengele vya mtindo vilivyotumiwa na msanii kuibua maudhui katika tamthiliya *za Jogoo Kijijini*, *Ngao ya Jadi* na *Lina Ubani*.

Kazi ya Mnenuka (ktj) ilikuwa na umuhimu katika kusukuma mbele utafiti wetu hadi kufikia malengo ya utafiti huo. Katika kazi hiyo mtafiti alipata uelewa wa kina

kuhusu mtindo katika fasihi hasa utanzu wa tamthiliya. Pia, mtafiti alibaini namna ya kufanya uchambuzi na kuwasilisha data zinazohusu mtindo. Kwa mantiki hiyo kazi hii iliuwezesha utafiti huu kuwasilisha data zinazohusu mtindo kwa misingi ya kitaaluma na kwa kuzingatia malengo na maswali ya utafiti huu.

Kwa hakika mapitio ya kazi tangulizi kuhusu mtindo na dhamira yamekuwa ni msaada mkubwa katika maendeleo ya utafiti huu. Hakuna shaka mapitio hayo yameongeza thamani ya kufikia utafiti huu kwa kuzingatia malengo na maswali ya utafiti. Sambamba na hilo kipengele cha mtindo na dhamira ndio msingi wa utafiti huu kwa kurejelea tamthiliya ya *Mondlane na Samora*. Hivyo ni imani ya mtafiti kuwa, kazi tangulizi hizo zimeakisi utafiti huu wenye mada*: Kuchunguza Mtindo na Dhamira katika tamthiliya ya Mondlane na Samora.*

### 2.3.2 Mapitio ya Kazi Tangulizi kuhusu Tamthiliya za Emmanuel Mbogo

Profesa Emmanuel Mbogo ni miongonii mwa waandishi mahiri katika uandishi wa kazi za kitaaluma ikiwemo kazi za Fasihi. Katika uandishi wa kazi za fasihi, mwandishi huyu amebobea zaidi katika utanzu wa riwaya na tamthiliya. Kwa utanzu wa tamthiliya baadhi ya tamthiliya zake ni pamoja na:*Giza Limeingia* (1980), *Watoto Wetu* (1981), *Tone la Mwisho* (1981), *Ngoma ya Ng'wanamalundi* (1988), *Morani* (1993), *Fumo Liongo* (2009), *Sundiata* (2011), *Nyerere na Safari ya Kanaani* (2015), *Wangari Maathai* (2015), *Sadaka ya John Okello* (2015), *Malkia Bibititi Mohamed* (2016) na *Mondlane na Samora* (2016) na *Mtumwa hadi Siti binti Saad* (2018).

Kwa upande mwengine tamthiliya za Prof. Emmanuel Mbogo zimefanyiwa utafiti na wataalamu kadhaa kama mwandishi mteule (pekee) na mwandishi mmojawapo

katika tafiti hizo. Miongoni mwa waliotafiti katika tamthiliya hizo ni pamoja na: Masoti (1993), Fadhili (2014), Clemence (2015), Mningo (2015), Shemweta (2015), Makame (2017). Baadhi ya ufafanuzi wa matokeo ya tafiti hizo ni kama ifuatavyo:

Masoti (1993) ametafiti*“Maudhui katika tamthiliya nne za Emmanuel Mbogo: Giza Limeingia* (1980), *Tone La Mwisho* (1981), *Watoto Wetu* (1981), *na Ngoma ya Ng’wanamalundi* (1988)”. Katika utafiti huo amejadili maudhui kwa misingi ya nadharia ya uyakinifu wa kijamaa. Miongoni mwa maudhui aliyoyagundua ni ukombozi, dhulma, usaliti, ubinafsi na nafasi ya mwanamke katika jamii.

Ni ukweli usiopingika, kazi ya Masoti (ktj) ni yenye ubora mkubwa katika kuongezea thamani ya utafiti huu. Pamoja na ubora huo, kazi hiyo ni tafauti na ile ya utafiti huu. Uhalisia wa hayo umejitokeza kwa kuwa kazi tangulizi hiyo imeakisi na kuchambua dhamira mbalimbali zilizojitokeza katika tamthiliya za Emmanuel Mbogo. Ni manufaa makubwa kwa mtafiti kupitia kazi hiyo, kwa sababu kipengele cha dhamira ndio lengo mahsusi la pili la utafiti huu. Mbali na tamthiliya hizo, *Mondlane na Samora*ni tamthiliya ya mwandishi Emmanuel Mbogo na ndio msingi wa kufikia mada ya utafiti.

Njogu na Chimerah (1999) walifanya uchunguzi wenye anuani*“Uchawi katika tamthiliya ya Mbogo.* Watafiti haowalifanya uchambuzi wa tamthiliya ya *Ngoma ya Ng`wanamalundi*. Katika uchambuzi wa tamthiliya hiyo wameeleza kuwa uchawi ni moja kati ya imani za kijadi ambazo zipo katika jamii za Afrika.Wamemtumia mhusika Chidama ambaye ni mchawi. Aliyetumia uchawi kuwafisha watu kisha kuwafufua. Kupitia mbinu ya matumizi ya urogi, watafiti hao wameeleza kuwa

jazanda imetumikakuwakilisha mbinu za kidhalimu za kuwaogopesha waongozwa katika bara la Afrika.

Kazi ya Njogu na Chimerah (ktj) ilikuwa na umuhimu katika utafiti huu. Kwanza mtafiti aliona namna Mbogo alivyotumia mitindo ya jadi katika kusana kazi zake. Pia, alipata uelewa wa mawazo ya mtunzi kuhusu mtazamo wake juu ya uongozi wa ambao umekuwa ukishika hatamu za uongozi katika bara la Afrika. Kwa hivyo mtafiti aliweza kupata muongozo katika kujadili dhamira katika tamthiliya ya *Mondlane na Samora.*

Mbonde (2002) alifanya utafiti wenye mada*"Uhakiki wa fani na maudhui katika tamthiliya ya Morani"*. Katika uhakiki anasema kuwa tamthiliya hiyo iliandikwa ili kusawiri hali ya maisha ya ulanguzi, usaliti, rushwa, uvunjifu wa maadili katika jamii ya Tanzania wakati wa miaka ya 1980. Uchambuzi wake umejikita pia katika mtindo na dhamira. Kwa hivyo kazi hii pia ilimsaidia mtafiti kuona namna data zilizohusiana na mtindo zinavyofanyiwa uchambuzi na hatimae kuwasilishwa. Pia, aliweza kuona dhamira mbalimbali ikiwemo ile ya usaliti ilivyojitokeza katika tamthiliya ya *Morani.* Ambapo katika utafiti huu ilijitokeza dhamira kama hiyo ndani ya *Mondlane na Samora*.

Fadhili (2014) alifanya utafiti *"Kuchunguza Dhima za Mtindo katika tamthilya za Kihistoria: Utafiti linganishi wa tamthiliya za Morani na Kinjeketile"*. Katika utafiti huo aligundua kuwa tamthiliya hizo zinafanana katika mbinu za kisanii na kiubunifu. Kwa upande mwengine aligundua kuwa tamthiliya hizo zinatafautiana. Tamthiliya ya *Morani* imetumia lugha ya kitamathali wakati *Kinjeketile* imetumia lugha ya

kawaida, ya wazi na ya kawaida. Pia, tamthiliya ya *Morani* ilijadili suala la historia baada ya uhuru nchini Tanzania wakati *Kinjeketile* ilijadili suala la kupigania uhuru toka kwa wakoloni huko Tanganyika. Kwa upande mwengine watunzi hawa wanafanana kutokana na kujadili masuala muhimu yanayoihusu jamii kama vile rushwa, harakati za ukombozi, usaliti, unyonyaji na ukandamizaji.

Utafiti wa Fadhili (ktj), ulikuwa na mchango mkubwa katika utafiti huu. Utafiti huo ulihusu tamthiliya tafauti na tamthiliya ya *Mondlane na Samora*ya , hata hivyo utafiti huo ulisaidia sana kufikia lengo la utafiti huu. Mtafiti alitalii kwa kina kazi hii na hatimae alipata uelewa wa namna ya kufanya uchambuzi wa vipengele vya mtindo hasa vinavyohusiana na matumizi ya lugha pale vilivyotumika kama sehemu ya mtindo. Kwa kufanya hivyo mtafiti alipata kujua namna ya kufanya uwasilishaji na uchambuzi wa data kutoka katika tamthiliya ya *Mondlane na Samora*.

Mningo (2015) alifanya utafiti wenye mada: *"Tathmini ya Mwingilianomatini katika utunzi wa Emmanuel Mbogo: Utafiti linganishi wa tamthiliya ya Ngoma ya Ng'wanamalundi na Fumo Liongo"* Katika utafiti huo pia alichunguza vipengele vya kimtindo kama vile matumizi ya hadithi, ngoma, majigambo, ushairi, matumizi ya wahusika wa fasihi simulizi na usihiri (uchawi) ambapo alilinganisha kazi za mwandishi mmoja katika vipindi tofauti huku akiongozwa na nadharia ya Mwitiko wa Msomaji na nadharia ya mwingiliano matini.

Kazi ya Mningo (ktj) imekuwa na mchango mkubwa katika maendeleo ya utafiti huu. Hii ni kwa sababu kazi hiyo imelenga katika uchambuzi wa tamthiliya za Mbogo katika misingi ya ulinganishi. Mbali na hilo vipengele viliyohakikiwa vya

mtindo vimeengeza faida ya kufikia mada ya mtafiti. Kwa mnasaba huo kipengele cha mtindo ni lengo la kwanza la utafiti huu wenye mada: *Kuchunguza Mtindo na Dhamira katika tamthiliya ya Mondlane na Samora*. Kwa minajili hiyo kazi tangulizi hiyo ni yenye kufaa sana.

Ni ukweli uliowazi mapitio ya kazi tangulizi kuhusu tamthiliya za Emmanuel Mbogo ni ya muhimu sana katika utafiti huu. Hii ni kwa saababu kazi hizo zimeakisi mwandishi mteule wa utafiti huu. Sambamba na hilo kazi hizo zimezidisha ufafanuzi wa kufikia malengo na maswali ya utafiti na kudhihirisha uwepo wa mahitaji ya kufanya utafiti kulingana na mada husika: *Kuchunguza Mtindo na Dhamira katika tamthiliya za Mondlane na Samora.*

## 2.4 Pengo la Utafiti

Katika utafiti huu, mtafiti ametalii kazi za waandishi mbali mbali kabla ya kuamua kuanza kuiandikia mada ya utafiti huu. Wakati wa kutalii waandishi wa kazi tangulizi, mtafiti amebaini kuwa tamthiliya za Kiswahili hasa za mwandishi Emmanuel Mbogo zimewahi kutafitiwa na watafiti kadhaa katika vipengele mbalimbali vikiwemo vya fani na maudhui. Miongoni mwa watafiti hao ni pamoja na: Masoti (1993), Fadhili (2014), Clemence (2015), Mningo (2015), Shemweta (2015) na Makame (2017). Pamoja na juhudi kubwa za watafiti hao, mtafiti hakuona utafiti uliowahi kufanywa wenye mada sawa na utafiti huu. Hivyo basi katika utafiti huu pengo la utafiti limejitokeza ambalo limemsukuma mtafiti wa mada hii kwa kuzingatia malengo na maswali ya mada ya utafiti isemayo: *Kuchunguza mitindo na dhamira katika tamthiliya ya Mondlane na Samora.*

## 2.5 Mkabala wa Nadharia

Fasili ya neno “nadharia” imekuwa na mawanda mapana. Wataalamu mbalimbali wameeleza kuhusiana na neno hilo. Miongoni mwa wataalamu hao ni wafuatao: Senkoro (1980) anasema kuwa nadharia ni istilahi ya kijumla inayomaanisha miongozo inayomwelekeza msomaji wa kazi ya fasihi kuielewa kazi hiyo ya fasihi katika vipengele vyake vyote. Mushengezi (2003) amesema kwamba, nadharia ni maarifa yaliyopangwa ili kuelezea dhamira fulani au wazo fulani.

Kwa ujumla, nadharia huchukuliwa kuwani dira ya kumwongoza mtafiti au mchambuzi kulikabili na kulielezea vyema jambo fulani kwa mtazamo ambao mtafiti ameujengea imani kwamba unaweza kuleta manufaa zaidi kuliko mtazamo mwengine pindi ukitumika. Nadharia hutoa mwongozo katika utatuziwa jambo ambalo halijaweza kuhakikishwa ukweli wake. Ni mawazo, maelezo au mwongozo uliopangwa ili kusaidia kutafuta au kuekeleza jambo.

Kazi yoyote ile ya fasihi ambayo inafanyiwa utafiti, kwa kawaida huwa na nadharia ambayo inaakisi muktadha wa kazi hiyo. Zipo nadharia mbalimbali ambazo zinaweza kutumika katika kuchunguza na kuchambua kazi za fasihi. Kila nadharia inaweza kufaa ama kutokufaa kuzichambua kazi za fasihi kwa kuzingatia lengo la utafiti wa kazi inayotafitiwa. Katika utafiti huu mtafiti ametumia nadharia ya Umitindo ambayo ndiyo nadharia muafaka itakayojibu lengo mahsusi la kwanza na swali la utafiti la kwanza hii ni kutokana na nadharia hiyo kujikita zaidi kimitindo na kumpa fursa mtafiti kuteua nadharia ya Mwitiko wa Msomaji ili kujibu lengo mahsusi la pili na swali la pili la utafiti na kufanikishaa vyema mada ya utafiti

isemayo: *Kuchunguza Mtindo na Dhamira katika tamthiliya za Mondlane na Samora*.

### 2.5.2 Nadharia ya Mwitiko wa Msomaji

Njogu na Wafula (2007) wanaeleza, nadharia ya Mwitiko wa Msomaji ambayo jina lake jengine ni nadharia ya Upokezi husisitiza nguvu za msomaji.Nadharia hiyo pia inahusu mabadiliko ya jumla ya umakinikaji kutoka kwa mwandishi na kazi yake kwenda kwa matini na msomaji. Nadharia ya Mwitiko wa Msomaji inaakisi mabadiliko ya mbinu katika historia ya fasihi na ilizingatiwa kama jibu kwa jamii, wanazuoni na maendeleo ya fasihi huko Ujerumani Magharibi mwishoni mwa miaka ya 1960.

Njogu na Wafula (ktj) wanaendelea kufafanua kuwa Wanaitifaki wa nadharia hii wanashikilia kwamba msomaji au mpokeaji huipa maana kazi ya fasihi kutokana na uzoefu wake wa maisha. Kwa hivyo, nadharia ya Mwitiko wa Msomaji hufasili fasihi kama mchakato wa namna msomaji na msanii wanavyoathiriana. Uzoefu wa maisha wa msomaji unaweza kutoa tafsiri tafauti kwa kazi ya fasihi kutoka msomaji mmoja na mwengine.Nadharia hiyo husemwa kwamba ina mapungufu kwa sababu inaifanya kazi ya Fasihi kutokuwa na maana mpaka pale inapoingia mikononi mwa msomaji. Kwa mantiki hiyo, msomaji asiyekuwa makini anaweza kuipa kazi husika maana finyu.

#### 2.5.2.1 Waasisi wa Nadharia Mwitiko wa Msomaji

Njogu na Wafula (2007) wanaweka wazi kuwa Nadharia ya Mwitiko wa Msomaji iliasisiwa na wahakiki wa Kijerumani mwishoni mwa miaka ya 1960. Miongoni

mwa waasisi hao ni Robert C. Holub, Hans Robert Jauss na Wolfagang Isser. Waasisi hawa ni Wajerumani, wanaamini kuwa kazi ya fasihi inapaswa kutazamwa kwa kulingana na mila, desturi na utamaduni wa msomaji. Kwasababu msomaji ana uhuru wa kutafsiri kama aonavyo kutokana na uzoefu wake, na si kutokana na uzoefu wa muandishi. Wananadharia hawa wanaweza kuwekwa katika matapo matatu ambayo ni:

i) Wale wanaoangazia kwenye tajriba za kipekee za msomaji. Hawa ni pamoja na C.C. Lewis, (1961), Stanley Fish (1967), na Normana Holland (1968),

ii) Wale wanaofanya majaribio ya kisaikolojia kwa kikundi maalumu cha wasomaji. Hawa ni Reuven Tsur, Richarad Gerring, David Miall na Donald Kuiken

iii) Wale wanaochukulia wasomaji wote wa kazi ya fasihi wataipokea kwa njia iliyosawa.

Hata hivyo, Stanley Fish (ktj) anadai kwamba sanaa ya maneno haichanganuliwi kwa kutumia mikakati ya jaribio la kisayansi. Anayefanya jaribio la kisayansi huweka mpaka wa kihisia na kimawazo kati ya nafsi yake na jambo linalomshughulisha.Wananadharia hao wanaeleza kuwa kazi ya fasihi inajikita katika ishara na taswira. Kutokana na ishara na taswira hizo matini za kifasihi huwa hazina maana moja bali zinakuwa na maana zaidi ya moja. Msingi mkuu wa nadharia hii ni kwamba kazi yoyote ya sanaa hurejelea kazi inayosomwa kwa tafsiri ili ithibitishwe kuwa kazi hiyo inaafikiana na yale yanayokumbukwa na msomaji wa kazi ya fasihi. Aidha, hubainisha jinsi miktadha ya matini isiyohusiana moja kwa moja na maandishi inavyoweza kuhusishwa na kutangamanishwa na msomaji.

#### 2.5.2.2 Mihimili ya Nadharia ya Upokezi

Njogu na Wafula (2007), wanasema wananadharia ya Mwitiko wa msomaji huuliza maswali ambayo kwayo misingi ya nadharia hii imejiegemeza. Maswali hayo ni kama haya yafuatayo:

i) Kuna uwiano wowote kati ya maana inayosomwa na jinsi msomaji anavyoihakiki?

ii) Je, kila kazi ya fasihi ina maana kufuatana na msomaji binafsi na namna anavyoichukulia?

iii) Kuna wasomaji ambao husoma na kufasiri kazi za fasihi vizuri zaidi kuliko wasomaji wengine.

iv) Msomaji hutumia vigezo gani kujijulisha iwapo mawazo yake juu ya kazi fulani yanafaa au hayafai?

Kwa mnasaba wa mada ya utafiti, nadharia ya Mwitiko wa Msomaji ni muhimu sana. Msingi mkuu wa uteuzi wa nadharia hii ni kwamba, imemsaidia sana mtafiti kuweza kuhakiki na kutumia uzoefu wa taaluma aliyonayo ili kuhakiki kazi ya fasihi katika tamthiliya teule ikiwa ni pamoja na uchambuzi wa lengo mahsusi la pili na kujibu swali la pili la utafiti huu wenye mada: *Kuchunguza Mtindo na Dhamira katika tamthiliya ya Mondlane na Samora.*

## 2.6 Hitimisho

Katika sura hii mtafiti amefanya uhakiki na uchambuzi wa kina wa vipengele muhimu ambavyo vimejitokeza katika sura husika. Vipengele viilivyohakikiwa ni pamoja na Ufafanuzi wa istilahi mbalimbali, mapitio ya kazi tangulizi kuhusu mtindo

na dhamira katika tamthiliya za Kiswahili na mapitio ya kazi tangulizi kuhusu tamthiliya za Emmanuel Mbogo. Mbali na hayo uchambuzi kuhusu nadharia umezingatiwa vyema. Nadharia ya Umitindo imefafanuliwa kwa ajili ya lengo mahsusi la kwanza na swali la kwanza la utafiti. Nadharia ya Mwitiko wa Msomaji imeelezwa vyema kwa ajili ya lengo mahsusi la pili na swali la pili la utafiti.

# SURA YA TATU

# MBINU ZA UTAFITI

## 3.1 Utangulizi

Sura hii kama sura zilizotangulia, imekuwa na thamani kubwa katika utafiti huu. Hii ni kwa sababu imejadili kwa kina mambo ya msingi katika utafiti. Vipengele husika ni pamoja na eneo la utafiti, usanifu wa utafiti, kundi lengwa, sampuli na usampulishaji, ukusanyaji wa data, uchambuzi wa data, zana/vifaa vya ukusanyaji wa data na Hitimisho.

## 3.2 Eneo la Utafiti

Eneo la utafiti ni mahali ambapo utafiti umefanyika kulingana na vile mtafiti anavyopendekeza ili kupata data za kujibu maswali yake ya utafiti (Crewell, 2009). Utafiti huu ni wa maktabani. Hivyo basi, umefanyika katika maktaba za Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (OUT) na Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) na maktaba kuu Zanzibar (zote tawi la Pemba). Sababu ya kuchagua maeneo hayo ni kwamba mtafiti aliamini kwamba angepata machapisho yanayohusiana na utafiti huo. Imani yake hii ilithibitika kwa kuwa chaguo la eneo la utafiti huu na kuweza kupata nyaraka mbalimbali zilizomwezesha mtafiti kufikia malengo ya utafiti wake. Vilevile kwa kutumia maktaba na kutumia fursa ya utulivu wa mazingira ya maktaba, mtafiti amepata nafasi ya kusoma matini za tamthiliya teule kwa utulivu wa kutosha. Mbali na hayo mtafiti ametumia wavuti/ tovuti kutoka katika mitandao kwa lengo la kuongeza maarifa yenye kuhusiana na mada ya utafiti huu. Aidha, mtafiti alitumia maktaba ya Chuo Kikuu SUZA ili kupata tasnifu nyengine ambazo alizisoma na kumpatia hoja za kushadidia mada yake.

### 3.3 Usanifu wa Utafiti

Utafiti huu una sura tano. Sura ya kwanza ni utangulizi wa jumla. Sura ya pili ni mapitio ya kazi tangulizi na mkabala wa kinadharia. Sura ya tatu ni mbinu za utafiiti.. Sura ya nne imehusu uwasilishaji na uchambuzi wa data za utafiti na sura ya tano muhtasari, hitimisho na mapendekezo ya utafiti.

### 3.4 Kundi Lengwa

Utafiti ni kazi inayohitaji umakinifu wa hali ya juu ili kuweza kufikia malengo ya utafiti husika kulingana na mada. Pamoja na hayo utafiti huwa na kundi lengwa ambalo hutumika ili kuweza kufikia malengo ya utafiti huo. Cresswell (2009) anaweka wazi kuwa, kundi lengwa ni jumla ya wanachama wote, mtu mmoja, kikundi au elementi ambazo mtafiti amekusudia kuzitumia na kuzihusiha katika utafiti wake kulingana na mada. Walliman (2011) anaeleza Kundi lengwa ni jumla ya vitu vyote vinavyostahiki na kuhusishwa kufanyiwa utafiti. Kwa maana ya watu, taasisi au matukio mengineo kwa ujumla. Kwa fasili nyengine kundi lengwa ni jumla ya walengwa au wakusudiwa wote katika utafiti ambapo sampuli husika ya utafiti inaweza kuhusishwa na kuchaguliwa.

Kwa muhtasari, kundi lengwa ni jumla ya walengwa au watafitiwa ambapo mtafiti amekusudia kuwatumia kwa lengo la kukusanya data/ taarifa anazozihitaji kulingana na mada ya utafiti. Katika utafiti huu, kundi lengwa ni tamthiliya teule ya *Mondlane na Samora* ya mwandishi Profesa Emmanuel Mbogo. Mtafiti amekusudia kusoma kwa kina tamthiliya hiyo kwa lengo la kupata taarifa/data za kina zinazohusu mtindo na dhamira kulingana na mada ya utafiti. Kazi tangulizi nyengine zimetumika kwa makusudi ya kuongeza maarifa yaliyohusiana na mada hiyo ipasavyo.

### 3.5 Sampuli na Usampulishaji

Kothari (2004) anasema, sampuli ni kundi dogo la watafitiwa waliochaguliwa kuwakilisha sifa mbali mbali na tabia za kundi zima ambalo humsaidia mtafiti kupata taarifa kutoka sampuli hiyo ili atoe majumuuisho ya utafiti wake. Usampulishaji ni unaohusisha mbinu mbali mbali za uteuzi wa utafiti kwa lengo la kumpatia mtafiti taarifa ambazo zilitumika kwa kutoa majumuisho yanayowakilisha kundi kubwa la watafitiwa ( Kothari 2004) au mchakato ulio rasmi wa kuchagua kikundi maalum cha vitu au watu kutoka katika kundi kubwa ili kuweza kutumika katika utafiti husika kama kiwakilishi cha kundi kubwa la utafiti. Hii ni kwa sababu sio rahisi kwa mtafiti kuweza kutafiti kundi lote (Enon, 1998) .

Katika utafiti sampuli mbalimbali hutumika na mtafiti kwa makususdi ya kufikia malengo na maswali ya mada ya utafiti. Katika utafiti huu mbinu ya usampulishaji lengwa na sampuli lengwa imetumika.

#### 3.5.1 Sampuli na Mbinu ya Usampulishaji Lengwa

Yin (1994) anafafanua kuwa sampuli lengwa ni aina ya sampuli ambayo mtafiti huteua kwa makusudi vitafitiwa au watafitiwa ambao anaamini watamridhisha mtafiti kwa kumpatia datazitakazomuwezesha kutimiza malengo ya utafiti wake kwa ukamilifu. Babbie (1999) anaona kuwa mbinu ya usampulishaji lengwa ni mbinu ya usampulishaji ambayo mtafiti huteua sampuli ya watafitiwa makusudi akiwa na imani ya kwamba sampuli hiyo itampatia data za utafiti anazozihitaji kwa wepesi kulingana na mada.

Katika utafiti huu, sampuli lengwa iliyotumika ni tamthiliya teule ya *Mondlane na Samora*. Tamthiliya hiyo imeteuliwa kutokana na uelewa wa awali wa mtafiti kwamba, ni tamthilia yenye matumizi ya aina kwa aina ya mitindo na dhamira zilizosheheni. Kwa hali hiyo data ambazo zimekusanywa zimepelekea kufanikisha vyema malengo na kujibu maswali ya utafiti huu kwa kiwango kizuri zaidi.

## 3.6 Aina za data zilizokusanywa

Katika utafiti huu, data zilizotumika ni za aina mbili: Data za Awali na Data za Upili:

### 3.6.1 Data za Awali

Data za awali (msingi) ni zile ambazo zimekusanywa kwa mara ya kwanza na hazijawahi kukusanywa na mtafiti mwingine yeyote kwa lengo na matumizi kama yanayofanywa na mtafiti wa kwanza (Furlong, 2000).

Data za msingi ni zile zilizokusanywa kwa mara ya kwanza na hivyo ni data halisi (Kothari, 2004). Data hizo huwa hazijawahi kukusanywa na wala kutumiwa na mtafiti mwengine yeyote kwa ajiliya utafiti kama huo anaoufanya mtafiti.Data za msingi katika utafiti huu zimekusanywa kutoka katika tamthilia ya *Mondlane na Samora.*

### 3.6.2 Data za Upili

Data za upili ni zile ambazo tayari zilikwisha kusanywa na watafiti wengine kwa ajili ya kutimiza malengo ya utafiti waona kuandikwa katika ripoti, makala, majarida, wavuti na vitabu tayari kwa ajili ya kusomwa kama

marejeleo katika maktaba mbalimbali (Creswell,2009). Madhumuni ya kutumia data za upili ni kwa ajili ya kukazia maarifa yanayotolewa katika data za msingi. Data za Upili hukusanywa na mtafiti kwa kuchagua machapisho mbali mbali ambayo yanaendana na mada ya utafiti kisha kuyasoma machapisho hayo kwa kina kwa lengo la kupata data za Upili. Data za upili za utafiti hu zimetokana na ripoti, tasnifu, makala, majarida, wavuti na vitabu mbalimbali vyenye kuhusiana na mada ya utafiti huu. Data hizo zimetumika wakati wa uchambuzi wa data za utafiti ili kuzipa nguvu hoja za data za msingi.

## 3.7 Mbinu za Ukusanyaji wa Data

Seale (2012) anaeleza kuwa kuna mbinu mbali mbali ambazo mtafiti huweza kutumia ili kukusanya data za utafiti. Kwa mantiki hiyo , Seale (ktj) amekusudia kueleza kuwa hakuna mbinu moja peke yake ambayo inajitosheleza . Uteuzi wa mbinu hizo hutegemea data anayoikusanya mtafiti . katika utafiti huu, data zilizo tumika ni za aina mbili :Data za Awali na Data za Upili .Utafiti huu umekusanya data kwa kutumia mbinu ya usomaji makini maktabani na mbinu ya upitiaji wa nyaraka wa tamthiliya teule. Mbinu ya usomaji makini imetumika katika ukusanyaji wa data za msingi na mbinu ya upitiaji wa nyaraka imetumika katika ukusanyaji wa data za Upili. Ufafanuzi wake ni kama ifuatavyo:

### 3.7.1 Mbinu ya Usomaji Makini Maktabani

Mbinu ya usomaji makini maktabani, ni mbinu ya usomaji wa kina na kukusanya data za msingi katika matini kama vile riwaya, ushairi na tamthiliya kwa lengo la kupata data ya utafiti unaokusudiwa kufanywa (Kothari, 2015). Mbinu hii ya usomaji makini kupitia maktabani imetumika katika utafiti huu kukusanya data za awali/

msingi kwa kurejelea tamthiliya ya *Mondlane na Samora*. Mtafiti ametumia mbinu hii kwa kusoma tamthiliya ya *Mondlane na Samora* kwa umakini wa hali ya juu, neno kwa neno, sentensi kwa sentensi kuanzia mwanzo hadi mwisho zaidi ya mara moja hadi kujiridhisha. Hii imemsaidia sana mtafiti kunukuu dondoo mbalimbali zinazohusiana na mada husika kwa kuzingatiamtindo na dhamira ambazo zinaendana na malengo na maswali ya utafiti. Vilevile mbinu hii imekuwa rahisi kwa mtafiti kwa sababu imemuwezesha kupata taarifa za msingi alizozihitaji kwa wepesi na ukweli wake. Data za msingi zilizokusanywa zilihifadhiwa katika daftari maalumu lililoandaliwa.

### 3.7.2 Mbinu ya Upitiaji wa Nyaraka

Robson (2007), anaeleza kusoma machapisho maktabani ni mbinu ya kukusanya data za upili kwa mtafiti kusoma kazi tangulizi zinazohusiana na mada yake ya utafiti ili kupata data za kujalizishia data za msingi. Jilala (2014), anasema mbinu hii huhusisha uchambuzi wa maudhui yaliyomo katika nyaraka kama vile vitabu, magazeti na maudhui ya maneno ambayo yanaweza kuwa ya maandishi au mazungumzo.Kwa hakika katika utafiti huu mbinu hii imekuwa na umuhimu wake katika utafiti huu. Mtafiti ametumia mbinu hii kwa kupitia nyaraka mbalimbali zikiwemo, tasnifu, makala, majarida, vitabu, tovuti / wavuti mbalimbali ambazo zinahusiana na mada ya utafiti. Hali hii imezidi kuimarisha utafiti huu katika maeneo tafauti ya utafiti ikiwemo kazi tangulizi. Sambamba na hilo nyaraka hizo zimeongeza thamani ya utafiti huu na kuufanya uimarike zaidi.

### 3.8 Uchambuzi wa Data

Babbie (1999) anaeleza kuwa, data zinazokusanywa wakati wa utafiti hazina budi kufanyiwa uchambuzi wa kina kwa lengo la kujibu maswali ya utafiti yaliyokusudiwa. Hivyo basi ni dhahiri kwamba uchambuzi wa data ni jambo la lazima ili kuweza kupata taarifa zilizosahihi baada ya kukusanya data za utafitiUchambuzi wa data kwa mujibu wa Kothari (2013), ni kitendo cha kufupisha na kupangilia vizuri data zilizokusanywa kwa namna ambayo itasaidia kujibu maswali ya utafiti husika. Katika utafiti mbinu mbalimbali hutumika katika uchambuzi wa data lakini data za utafiti huu zimechambuliwa kwa kutumia mbinu ya mkabala wa kimaelezo.

#### 3.8.1 Mkabala wa Kimaelezo

John (2007) anaeleza, uchambuzi wa kimaelezo ni mbinu inayomruhusu mtafiti kusikiliza au kuona au kusoma kazi ya fasihi tamthiliya, kisha kuelewa maudhui ambayo yamebeba dhamira, falsafa, migogoro, ujumbe na mtazamo/ msimamo wa mtunzi. Kwa mantiki hii mtafiti ataelewa matumizi ya mitindo mbalimbali pamoja na dhamira zilizomo katika kazi ya fasihi.

Mtafiti ametumia mbinu hii ili kuweza kukusanya data kwa urahisi. Mbinu hii hutumika sana katika kuchambua data zinazohusiana na fasihi kwa sababu fasihi ni taaluma ya maneno ambayo huzungumzwa au huandikwa. Hivyo basi, uteuzi wa mbinu hii sio kwamba data za utafiti haziwezi kuwasilishwa na kuchambuliwa kwa mbinu ya kimahesabu isipokuwa ni uamuzi tu wa mtafiti mwenyewe kutumia mkabala wa kimaelezo ambao ameona ndiyo mbinu muafaka ya uchambuzi wa data za utafiti wake. Kwa misingi hiyo

mbinu ya mkabala wa kimaelezo imetumika katika uchambuzi wa data katika tamthiliya ya *Mondlane na Samora* kwa wastani wa asilimia themanini (80%). Mbali na hilo mkabala wa kimahesabu/kitakwimu umetumika kwa kiwango kidogo kwa wastani wa asilimia 20%. Lengo kuu la kutumia mkabala wa kimahesabu ni kurahisisha ufahamikaji wa kazi husika pamoja na kutumika kimuhtasari wa uchambuzi wa data zilizofanywa na mkabala wa kimaelezo.

### 3.9 Maadili ya Utafiti

Maadili ya utafiti huhusisha mila na desturi ambazo jamii huziamini katika eneo ambalo mtafiti amekusudia kuchunguza kitu fulani. Lengo la maadili katika utafiti ni kulinda mambo ya kibinaadamu yanayoaminiwa na jamii. Vilevile kuhakikisha utafiti unafanyika katika miktadha unaokubalika, kwa mtu mmoja mmoja, kikundi cha watu au jamii kwa ujumla na kuhakikisha kuwa miradi ya tafiti inazingatia maadili kama vile masuala ya uongozi na athari zake, utunzaji siri na utoaji wa habari (http:/researchethics).

Miongoni mwa vitu muhimu anavyotakiwa mtafiti kuvizingatia ni maadili ya utafiti yanayohusu kupata kibali cha kufanya utafiti na kutunza siri za watafitiwa. Hivyo katika utafiti huu maadili ya utafiti yamezingatiwa ipasavyo kabla na baada ya kukusanya data. Kwa vile utafiti huu ni wa maktabani mtafiti amehakikisha kuwa nukuu kutoka katika tamthiliya teule zinafanywa kwa usahihi na umakini mkubwa na baadae kuchambuliwa kifasihi kwa kuongozwa na nadharia mbili za uhakiki wa kifasihi. Nadharia ya Umitindo na nadharia ya Mwitiko wa Msomaji.

### 3.10 Vifaa vya Kukusanyia Data

Mulokozi (1983) anaeleza kuwa vifaa vya utafiti hutegemea aina ya utafiti, lakini aghlabu baadhi ya vifaa hivyo: Kalamu na karatasi, shajara, tepurikoda na vifaa vyake, video/ kamera rikoda na vifaa vyake, kompyuta na vikokotoo vyake, hojaji na dodoso, vifaa vya kupimia na kuhesabu, darubini, vionambali na kadhalika. Katika utafiti huu data za utafiti zimekusanywa kwa kutumia zana zifuatazo:

#### 3.10.1 Shajara na Kalamu

Kwa mujibu wa kamusi ya TUKI (2013), shajara ni kitabu cha kuwekea kumbukumbu za kila siku. Zana hii imetumika kuhifadhi kumbukumbu za data zilizopatikana katika machapisho mbali mbali. Kalamu ni kifaa kilichotumika kuandikia na kuweka kumbukumbu za data za utafiti teule kwa ajili ya kufanyiwa uchambuzi.

#### 3.10.2 Kompyuta

Kompyuta ni zana ambayo mtafiti ameitumia tangu mwanzo hadi mwisho wa utafiti wake. Kompyuta ni mashine ya kielektroniki inayotumika kuhifadhi na kusarifu taarifa zinazoingizwa ndani yake (BAKIZA, 2010). Mtafiti ameitumia zana hii kuchapa kazi yake ya utafiti, kuhifadhi data, kutafuta machapisho na maandiko mbalimbali yahusuyo utafiti huu yanayopatikana katika tovuti na wavuti mbalimbali.

#### 3.10.3 Vitabu, Tasnifu, Makala na Majarida

Kwa hakika vifaa hivi ni muhimu sana katika maendeleo ya utafiti huu. Vifaa hivi vimetumika kikamilifu katika maeneo mbali mbali muhimu ikiwemo kwenye

mapitio ya kazi tangulizi. Msingi mkubwa wa kutumia vifaa hivi ni kuendelea kutilia mkazo mada husika kwa kuzingatia dhana kuu za mtindo na dhamira ambazo zimeenda sambamba na malengo na maswali ya mada ya utafiti huu.

## 3.11 Hitimisho

Sura hii imehusu mbinu za utafiti. Katika mbinu hii vipengele vya msingi vimefafanuliwa vyema. Vipengele hivyo ni pamoja na Eneo la utafiti ambalo ni Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (OUT), Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) na Maktaba kuu Zanzibar (zote tawi la Pemba). Vile vile kundi lengwa la utafiti huu ni tamthilia teule ya *Mondlane na Samora.* Sampuli iliyotumika ni sampuli lengwa ambayo ni tamthiliya teule. Mbinu za ukusanyaji wa data zilizotumika ni pamoja na usomaji makini kwa data za awali na upitiaji wa nyaraka kwa data za upili. Mbinu za uchambuzi wa data zilizofafanuliwa ni mkabala wa kimaelezo na mwisho ni zana/ vifaa vya utafiti.

# SURA YA NNE

# UWASILISHAJI NA UCHAMBUZI WA DATA ZA UTAFITI

## 4.1 Utangulizi

Sura hii inalengo la kuwasilisha na kuchambua kwa undani data zilizokusanywa na mtafiti wa kazi hii kutoka maktabani aliko kwenda maksudi kwa ajili ya kutafuta data hizo. Vipengele vya msingi vilivyohusika katika eneo hili ni usuli wa mwandishi Prof. Emmanuel Mbogo, Muhtasari wa tamthiliya ya *Mondlane na Samora*, Uwasilishaji na uchambuzi wa vipengele vya kimtindo kwa kurejelea nadharia ya Umitindo. Uwasilishaji na uchambuzi wa dhamira katika tamthiliya ya *Mondlane na Samora* kwa kuhusisha na nadharia ya Mwitiko wa Msomaji. Mwisho mtafiti ametoa hitimisho la sura nzima.

## 4.2 Usuli wa Mwandishi Emmanuel Mbogo

Profesa Emmanuel Yakobo Mbogo ni mtunzi na mwandishi wa tamthiliya za Ngoma ya Ng'wanamalundi na Fumo Liongo. Ni msomi na Profesa wa sanaa za maonyesho na Fasihi ya Kiswahili. Wakati wa usaili na msanii huyu, tuliweza kupata usuli wa maisha yake na utunzi kwa ujumla. Kutokana na maelezo yake, Emmanuel Mbogo alizaliwa tarehe 01/03/1947 katika wilaya ya Kongwa, mkoa wa Dodoma. Alisoma katika shule ya msingi Mpwapwa na kuhitimu darasa la nane mwaka 1963. Baadaye alijiunga na masomo ya sekondari katika shule ya sekondari Indian (kwa sasa inajuulikana kama Shule ya Sekondari Dodoma ) na kuhitimu mwaka 1967. Wakati akisubiri matokeo yake , ya mtihani wa Sekondari alifanya kazi ya ukarani katika Wizara ya Kilimo, mkoani Dodoma. Baada ya kufaulu mwaka 1968, alijiunga na Chuo cha Ualimu Morogoro kwa ajili ya mafunzo ya Ualimu daraja la IIIA na

kuhitimu mwaka 1969. Akiwa chuoni hapo, ndipo alipgundua kipaji chake cha uandishi. Hii ni baada ya kuandika hadithi aliyoiita James I Die of Love (1968) katka jarida la chuo lililokuwa linaitwa Morani, hadithi hiyo iliwavutia wasomaji na kusifiwa sana mwalimu wake wa Fasihi ya Kiingereza na wanachuo wenzake. Hadithi hii ndiyo iliyomtanabaishia uwezo wake wa kutunga hadithi na kumpa hamasa na ari ya kuingia katika ulimwengu wa sanaa na utunzi.

Mwaka 1970, alipangiwa kufundisha katika shule ya msingi ya Mwitikira iliyopo mkoani Dodoma. Akiwa anaedelea kufanya kazi, alijiunga na Chuo cha Rapid Result College kilichopo nchini London kwa mfumo wa elimu msafa, na kusomea masomo ya Kiswahili na Jiografia kwa lengo la kuongeza alama ziitakazomwezesha kujiunga na masomo ya stashahada. Wakati huohuo akiwa katika shule hiyo, alitunga tamthiliya yake ya kwanza aliyoiita *Mama Tamasha* (1970). Mwaka 1971 alihamia katika shule ya Nara. Akiwa katika shule ya msingi Nara, aliufanyia mazoezi mchezo huo na wanafunzi wake darasani, lengo likiwa ni kusikiliza namna unavyosikika katika mazungumzo na vitendo. Mchezo huo uliigizwa waka 1972 alipokuwa akifundisha shule ya Msingi Bwigiri. Wakati huo yeye na kundi lake la waigizaji ambao ni wanafunzi wake, walitembea na kuigiza mchezo huo katika vijiji na shule mbalimbali kwa kutumia usafiri wa magari yaliyokuwa yanahamishia watu kwenye kijiji cha ujamaa. Mchezo huu aliubadili jina na kuuita *Watoto Wetu* (1972).

Mwaka 1973 alijiunga na masomo ya stashahada ya ualimu na sanaa za maonyesho katika Chuo cha Ualimu Chang’ombe, kilichopo jijini Dar es Salaam na kuhitimu mwaka 1974. Baada ya kumaliza mafunzo ya stashahada, alipangwa kufundisha katika Chuo cha Ualimu Katoke, ambapo alifundisha hadi Juni 1976, alipojiunga na

Chuo Kikuu cha Dar es Saalam, kusomea shahada ya kwanza na ya pili katika Sanaa za Maonyesho ( B. A in Theatre Arts na M. A in Theatre Arts). Akiwa chuoni hapo, alitunga tamthiliya yake ya pili iliyoitwa *Tone la Mwisho* (1981). Akiwa bado mwanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dar es Saalam alitunga tamthiliya nyengine iliyoitwa *Giza Limeingia* (1977), ambayo ilivutia na kuonyesha uwezo wa kipaji chake. Yeye ndiye alikuwa mwongozaji wa tamthiliya hiyo iliyoigizwa katika chuo Kikuu cha Dar es Saalam. Mbogo, alihitimu masomo yake ya shahada ya sanaa za maonyesho mwaka 1981. Mwaka 1982 alijiunga na Chuo Kikuu cha Humboldt kilichopo mjini Berlin nchin Ujerumani, kwa masomo ya shahada ya tatu katika sanaa za Maonyesho (PhD in Theatre Arts) na kuhitimu mwaka 1984.

Baada ya kumaliza masomo yake alirudi nchini Tanzania na kufanya kazi katika Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili (TUKI), ambayo kwa sasa inatambulika kama Taasisi ya Taaluma za Kiswahili (TATAKI), iliyopo Chuo Kikuu cha Dar es Saalam hadi mwaka 1989. Mwaka 1990, alikwenda nchini Kenya na kufundisha katika Chuo Kikuu cha Moi hadi mwaka 1991. Mwaka 1992 alihama na kwenda kufundisha katika Chuo Kikuu cha Maseno kilichopo Kisumu hadi mwaka 2002, kisha mwaka 2003 alihamia Chuo Kikuu cha Kenyata ambapo alifundisha hadi mwaka 2006.

Baada ya hapo mwaka 2007 alikwenda nchini Rwanda na kufundisha katika Chuo Kikuu cha Kigali kwa muda wa mwaka mmoja. Mwaka 2008 alirudi nchini Tanzania na kujiunga na Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, ambapo yupo hadi sasa akiwa ni mhadhiri chuoni hapo.

Mtunzi ameshatunga vitabu kadhaa vya riwaya na tamthiliya. Tamthiliya alizokwishatunga na kuzichapisha ni *Watoto Wetu* (1972), *Giza Limeingia* (1980), *Tone la Mwisho* (1981), *Ngoma ya Ng'wanamalundi* (1988), *Morani* (1993), *Fumo Liongo* (2009), *Sundiata* (2011), *Sadaka ya John Okelo* (2014) na *Nyerere na safari ya Kanaani* (2015). Vilevile ametunga tamthiliya iitwayo *Tunuafrika – Wangari Maasai* (haijatoka). Pamoja na tamthiliya hizo, ametunga riwaya kama vile *Watoto wa Mama Ntilie* (2002), *Vipuli vya Figo* (2008) na *Siri ya Maisha* (2010).

Katika utafiti huu tulichagua tamthiliya zake mbili za Ngoma ya Ng'wanamalundi na Fumo Liongo kama ilivyojadiliwa katika sura zilizotangulia. Kwa hiyo mjadala wetu utajikita katika tamthiliya hizo mbili.

### 4.3 Muhtasari wa Tamthiliya ya *Mondlane na Samora*

Tamthiliya ya *Mondlane na Samora* ni miongoni mwa tamthiliya za kihistoria iliyohusu harakati ya kusaka uhuru wa Msumbiji kwa mtutu wa bunduki. Rais wa kwanza wa Frelimo, Edwardo Mondlane aliyaongoza mapigano dhidi ya ukoloni wa Mreno kwa ujasiri mkubwa; lakini akiwa Dar-es-salam tarehe 3/2/1969, Mondlane alipokea paseli kutoka Lisbon, akaifungua na bomu likaripuka na kumuua. Baada ya tanzia hii Samora Machel akachukua uongozi wa Frelimo na kuendeleza vita vya msituni hadi Msumbiji ilipopata uhuru wake tarehe 25/6/1975. Baada ya kutawala kwa miaka kumi na moja, Rais Samora Machel naye alikufa kwa ajali ya ndege iliyotunguliwa na makombora ya makaburu wa Afrika ya Kusini. Mwandishi ameonesha pia jinsi Nyerere na Watanzania kwa jumla walivyojitoa muhanga kwa hali na mali ili kuung'oa ukoloni barani Afrika. Askari wengi wa Tanzania walikufa walipokuwa wakipigana dhidi ya ukoloni huko Msumbiji, Angola, Zimbabwe na

Namibia.Tamthiliya ya *Mondlane na Samora* ina jumla ya maonyesho saba ambapo kila onyesho ni mwendelezo wa onyesho jingine.Pia katika tamthiliya hii kuna mjengano wa visa na matukio. Wahusika wakuu wa tamthiliya hii Mondlane na Samora kama jina la kitabu linavyojieleza.

Katika utafiti huu tamthiliya ya *Mondlane na Samora* imetumika kwa kuzingatia malengo na maswali ya mada ya utafiti isemayo: *Kuchunguza Mtindo na Dhamira katika tamthiliya ya Mondlane na Samora.*

### 4.4 Matumizi ya Mtindo katika Tamthiliya ya *Mondlane na Samora*

Mada ya utafiti huu ni*Kuchunguza Mtindo na Dhamira katika Tamthiliya ya Mondlane na Samora.* Lengo mahususi la kwanza la utafiti huu lililenga “Kubainisha vipengele vya mtindo katika tamthiliya ya *Mondlane na Samora*.”Lengo hili lilikwenda sambamba na swali la kwanza la utafiti lisemalo “ni vipengele vipi vya mtindo vilivyobainishwa katika tamthiliya ya *Mondlane na Samora?*” Ili kufanikisha vyema uwasilishaji  na uchambuzi wa data kwa mnasaba wa lengo mahsusi la kwanza na swali la kwanza la utafiti huu, nadharia ya Umitindo imetumika vyema katika utafiti huo. Uwasilishaji na chambuzi wa data hizo ni kama ifuatavyo:

#### 4.4.1 Matumizi ya Lugha

Matumizi ya lugha ni moja kati ya kipengele cha mtindo kilichotumiwa na msanii katika tamthiliya teule ya *Mondlane na Samora*. Mlaga (2017), anaeleza kuwa lugha inaweza kutumika kama mtindo pale inapotumika kuendana na shughuli au tukio. Mtazamo huu unaegemea hoja kwamba uteuzi wa lugha hutegemea shughuli au muktadha uliopo. Muktadha huwa unaamua ni aina gani ya maneno yanakubalika na

yapi hayakubaliki kutumika katika muktadha huo. Hivyo basi, katika fasihi,lugha kama mtindo huweza kuangaliwa kwa kuzingatia wahusika namna wanavyotumia lugha wakiwa katika shughuli ama miktadha mbali mbali. Katika utafiti huu, matumizi ya lugha kama mtindo yamejidhihirisha katika tamthiliya ya *Mondlane na Samora* kupitia miktadha mbali mbali kama ifuatavyo:

#### 4.4.1.1 Matumizi ya Tamathali Semi

Tamathali za semi ni maneno au sentensi zinazotmiwa na wasanii wa fasihi kutia mkazo katika maana, mtindo na hata sauti katika maandishi ama kusema (Senkoro 2011). Katika *Mondlane na Samora*, tamathali za semi zimejitokeza kama ifuatavyo:

##### 4.4.1.1.1 Tashbiha

Syambo na Materu (1992) wanasema kuwa tashbiha ni yale maneno yanayofananisha kitu au kitendo kimoja na kingine. Katika tamthiliya ya *Mondlane na Samora,* mtafiti amegundua tashibihambalimbali. Baadhi ya tashbiha hizo ni kama zifuatazo:

(i) *"Hii ni damu ya Msumbiji inayotiririka kama maji ya mto Ruvuma"*(uk. 5)

Tashbiha hii imetumiwa na Mondlane wakati akiwa jukwaani akihutubia na kuonesha namna Afrika ilivyohitaji ukombozi kutokana na ukandamizwaji na unyonywaji uliofanywa na wakoloni. Ili kuondokana na unyama uliokuwa ukifanywa na wakoloni, msanii ametumia vita vya Frelimo dhidi ya Wareno huko Msumbiji kama ni harakati za kupinga ukoloni wa Wareno na matendo yao yakiwemo yale ya mauaji ya kinyama na ya kikatili dhidi ya raia wasiokuwa na hatia.Tashbiha

nyengine ni ile aliyoibaini mtafiti kupitia muhusika Josina wakati akiwa msituni huko Msumbiji. Mwandishi ameelezatashbiha hiyo kwa kusema:

(ii) "*...nitazipaka mafuta ya nazi ili ziwe laini kama mbelewele za mahindi*" (uk.18).

Msanii ametumia mbinu hii ili kumuonesha Josina namna alivyokuwa na mapenzi ya kweli dhidi ya Samora. Kutokana na upendo huo mwandisi ameonesha namna Josina alivyo na hamu ya kutaka kuhitimisha lengo lao la ndoa baina yake na Samora. Suala la ndoa linachukuliwa uzito mkubwa na umuhimu wa aina yake. Kama asemavyo Sengo (1992), kwamba suala la ndoa na harusi lina umuhimu wa aina yake miongoni mwa jamii za Uswahilini. Asasi hii ndiyo kitivo muhimu kwa maisha ya Uswahilini. Kutokana na hamu hii ya mapenzi kati ya Josina na Samora msanii ametumia tashibiha isemayo:

(iii) "*Wanaanguka, wanabingiria kama gunia*" (uk. 21).

Katika tashibiha hii msanii amedhihirisha namna Samora na Josina walivyokuwa wakikidhi haja yao ya kimapenzi. Vile vile, msanii ametumia tashibiha wakati akijadili namna Mwalimu Nyerere alivyookoka wakati akiwa Msumbiji walipovamiwa na wanajeshi wa Ureno. Tashibiha hii inasema:-

(iv) "*Nadhani ni kama fimbo ya Nabii Mussa iliyogawa bahari ya Sham*"(uk 88).

Tashibiha hii imeonesha namna baadhi ya watu walivyokuwa na itikadi dhidi ya Mwalimu Nyerere. Kwa ujumla tashibiha hii imesawiri imani za baadhi ya watu ambao waliamini kuwa fimbo ya Mwalimu Nyerere ilikuwa na uwezo wa kisihiri

ambao iliweza kumuokoa na matatizo ambayo yangeweza kumkabili. Imani ya wanaoliamini hilo ni kwamba, nguvu hizo ndizo zilizomfanya aokoke na mashambulizi ya maangamizi ya majeshi ya Wareno wakati wakiwa msituni huko Msumbiji.Pia, msanii ametumia tashibiha wakati akitusimulia namna Mwalimu Nyerere na Samora walivyokuwa na ukaribu na urafiki. Katika kusawiri uhusiano huu masanii ametumia tashibiha inayosema

(v) "*Loo! Unajua, kwake Samora; Nyerere ni kama baba yake mzazi*' (uk.71).

Kutokana na uhusiano huu wa karibu kati ya Nyerere na Samora kunaashiria udugu wa dhati wa kihisia kwa wapigania uhuru wanchi za Kiafrika. Nyerere akiwa mstari wa mbele bila kujali dini, rangi wala kabila. Udugu huo wa hali na mali ndiyo uliokuwa chachu ya harakati za uhuru wa wanaMsumbiji. Tashbiha nyengine zilizojitokeza ni:

i) *Usizime! Usife mpenzi! Tazama pacha hizi kama nusu mbili za vifuu vya nazi*

ii) (uk.21)

iii) *Usilie! Usilie! Mpenzi Unguruma kama Simba* (uk. 21)

iv) *Kama! Kamua, kunywa! Zikuwashe kama pilipili manga!* (uk. 21)

v) *Wafe mbu wote kama askari wa Salazari* (uk. 24)

vi) …*kuongozwa na mwanajeshi, siyo Muhafidhina kama Adward Mondlane* (uk.26)

vii) *Nikiwa mkubwa, nataka niwe komando kama baba yangu* (uk.74)

viii) *Utapona ewe mwenye sauti kama maanguko ya maji ya mto Limpopo* (uk. 90)

ix) *Utapona mwenye miondoko ya madaha kama twiga wa Serengeti* (uk.90)

Kwa kurejelea nadharia ya Umitindo ambayo imeongoza lengo mahsusi la kwanza na swali la kwanza la utafiti huu,mtafiti ameona kuwa msanii ametumia kipengele cha msamiati kama uteuzi wa mtindo wake. Kama asemavyo Leech (1969), kwamba Umitindo huchunguza kuwepo kwa vipengele kadhaa vya misamiati, huku misamiati hiyo ikizingatiwa namna ilivyotumika katika sajili mbalimbali. Kwa sababu hiyo mtafiti amebaini matumizi ya uteuzi wa misamiati katika tamthiliya ya *Mondlane na Samora* yamesawiri katika suala la mapenzi miongoni mwa wanajamii. Kwa mfano, mwandishi aliposema "*nitazipaka mafutaya nazi ili ziwe laini kama mbelewele za mahindi"*(uk.18). Msanii amechagua maneno kama vile "*nitazipaka mafuta ya nazi*" ili kuonesha upendo waliokuwa nao Josina na Samora. Aidha, matumizi haya ya tashbiha ni mtindo wa msanii kwasababu umelenga kutuchorea picha ya miktadha ya mapenzi na ukombozi. Kama asemavyo Mlaga (2017), kwamba mtindo kama matumizi ya lugha huendana na shughuli ama tukio linalofanyika. Anaendelea kufafanua kuwa uchaguzi wa aina ya lugha ya kutumika hutegemea shughuli au muktadha uliopo. Hi ina maana kwamba shughuli au miktadha iliopo ndiyo inayozaa mitindo mbali mbali ya lugha.

**4.4.1.1.2 Sitiari**

Kahigi (1995) na Mlaga (2017), wanaeleza kuwa sitiari ni tamathali ya semi ambayo hulinganisha kitu, vitu au dhana mbili kwa kuifanya dhana moja na bila ya kutumia kiunganishi chochote. Hii ni tamthali ya semi ambayo hutumika kama ni kipengele cha mtindo katika kazi za fasihi. Hivyo, katika tamthiliya ya *Mondlane naSamora*data zilizokusanywa zimebainisha kuwa mtunzi wa tamthiliya hii

ametumia sitiari hizo kama ifuatavyo: Msanii ametumia tamathali ya semi ambayo nisitiari aliposema:

(i) “*Miungu ya Ulaya ilipodai sadaka ya damu ya mtu mweusi huku udenda ukiwavuja mbweha wale…* “ (uk. 6).

Sitiari hii imetumiwa na mhusika Mondlane ili kuonesha utabaka katika jamii ya Afrika. Katika sitiari hii msanii ametumia neno “*Miungu ya Ulaya*” ili kuonesha namna Afrika ilivyokandamizwa na Wazungu. Wakoloni walijifanya miungu watu na wakawa wanawakandamiza na kuwaonea Waafrika. Hali hii ya ukandamizaji uliokuwa na unaoendelea kufanywa na Wazungu katika bara la Afrika hadi leo kumezishughulisha kalamu za waandishi wengi katika bara hili la Afrika. Mathalani, Hussein (1977), katika tamthiliya ya *Mashetani* anawafananisha wakoloni na mashetani kutokana na maovu wanayoyatenda katika bara la Afrika.Pia, msanii ametumia mtindo tamathali ya semi ambayo ni sitiari katika tamthiliya hii ya *Mondlane na Samora* pale aliposema:

(ii) *“Ubepari ni jini litakalofyonza damu za Wanamsumbiji”* (uk.14).

Sitiari hii imetumiwa na muhusika Samora akijadili itikadi za mifumo ya kiuchumi katika jamii ya Msumbiji. Samora ameufananisha mfumo wa kibepari na jini linalofyonza damu ya wanamsumbiji. Hapa Samora ameonesha kuwa kupitia mfumo wa kibepari jamii ya Msumbiji inanyonywa na kukandamizwa. Hivyo basi, Samora anaona ipo haja ya Msumbiji kufuata mfumo wa Ujamaa chini ya mihimili ya mtazamo wa Kimarx. Suala hili lilizua mjadala mkubwa miongoni mwa Waafrika. Wapo waliokubaliana na Ubepari na wapo walioona kuwa Ujamaa hauna maslahi katika jamii. Kwa mfano, mhusika Nungo ameonekana akilaani na kuona wale

ambao wanashadadia mfumo wa Ujamaa kuwa bado hawajajielewa. Katika kulieleza hilo Nungo ametumia sitiari isemayo

*(iii)* *"Baadhi ya nchi za Kiafrika zimepagawa na huyu kibwengo wa kikoministi"*(uk.15).

Kutokana na sitiari hii ni wazi kuwa wapo watu kama Nungo na Kavandame katika jamii ambao wamekuwa wakipinga mfumo wa Ujamaa ndani ya bara la Afrika.Kezilahabi katika maandishi mbalimbali amekuwa akiujadili mfumo wa ujamaa huku akiulinganisha na mfumo wa kibepari. Katika kazi zake kama vile tamthiliya ya Kaptula la Marx (2010) ameonesha namna Afrika ilivyovamia mfumo huo bila ya kujitambua. Katika tamthiliya hiyo amemtumia muhusika Raisi Kapera akifuata mfumo wa Ujamaa ambao hauna tija naye. Kutokana na mawazo kama haya msanii amemtumia Nungo akitumia sitiari isemayo "*Kasuku wote wa Max wamelala saa hizi…*" (uk. 25) ili kukejeli na kudhihaki wale ambao wanafuata mfumo wa Ujamaa.

Kama hiyo haitoshi, muhusika Nungo ametumiwa na msanii katika sitiari inayosema:

(iv) "*Afrika imepatwa na degedege la Stalin na wazimu wa Fidel Castro*" (26).

Kutokana na sitiari hii msanii ameonesha namna suala la Ujamaa na Ubepari lilivyoibua mgogoro miongoni mwa wapigania uhuru. Kutokana na mitazamo changamano kuhusu mifumo ya kiuchumi, baadhi ya watu walichukuliwa kama ni wasaliti. Nungokatika tamthiliya ya *Mondlane na Samora*ameonekana kuwa ni msaliti kutokana na kukataa mfumo wa ujamaa huku aking`ang`ania mfumo wa

kibepari. Hivyo Nungo anawaona watu kama vile Mondlane na Samora ni vibaraka wa Marx kwa kukumbatia mfumo wa Ujamaa.

Omary (2011), anaeleza kuwa mfumo Ujamaa ambao ulipigiwa mbiu na Mwalimu Nyerere ulilenga kufanya ukombozi wa Watanzania. Hata hivyo mfumo huu ulishindikana kutokana na baadhi ya watu kwenda kinyume na misingi ya mfumo wa Ujamaa. Mathalani, baadhi ya viongozi walilisaliti taifa na kuwa walaji rushwa, hongo na wabinafsi. Matokeo yake viongozi wengi walifikiria maendeleo yao binafsi badala ya ujenzi wa taifa.Sitiari nyengine zilizotumika katika tamthiliya ya *Mondlane na Samora*kama kipengele cha mtindo ni kama zifuatazo:

(v) *Nakusikiliza tausi wangu* (uk.19)
*(vi)* *Hatuwezi kupigana bega kwa bega na moma anayejifanya kuwa kondoo Rahim*(29-30)
(vii) *Sote tunawajua popo wawili waliopo miongoni mwetu* (uk. 34)
(viii) *Ewe dume la simba, nyata,nyemelea, uyapokee mawindo ya chaguo lako* (uk. 39)

Kwa kurejelea nadharia ya Umitindo, imeonyesha kwamba mitindo ya lugha ya sitiari imelandana na kile kinachoelezwa katika nadhariahii katika msingi wa itikadi, mtazamo na mtindo. Katika msingi huu mtafiti amebaini kuwa maneno hutumika ili kuonesha itikadi fulani. Hivyo, maneno wanayopewa wahusika kama vile Nungo yanaashiria itikadi ya Ubepari na maneno ya Mondelane na Samora ni ishara ya uendelezaji wa itikadi ya Ujamaa.

Sambamba na hayo, mtafiti amegundua kuwa sitiari zilizotumiwa na wahusika hawa ni mtindo wa mtunzi. Hii ni kwasababu mtunzi ameteua maneno maalumu ili kuwasilisha mjadala kuhusu ubepari na ujamaa. Kama asemavyo Mlaga (2017),

mtindo huweza kujitokeza kutokana na utamaduni wa jamii kuwa na kawaida na taratibu za kuchagua dhana mahususi za kiisimu za kuweza kutumika kutokana na muktadha unaoongoza mawasiliano husika. Hivyo nyenzo au dhana za kiisimu hufanywa kutegemeana na sababu za mtunzi.

#### 4.4.1.1.3 Tashihisi

Kahigi (1995), anafasili tashhisi kuwa ni usemi ambao sifa ya uhai huwa umehamishiwa kwenye kitu kisicho na uhaiau dhana dhahania. Anaendelea kusema kuwa Tashihisi ni usemi ambaosifa ya uhaihuhamishwa kwenye kitu kisicho na uhai. Data zilizokusanywa na mtafiti zimeonesha kuwa Emmanuel Mbogo ametumia mbinu ya tashihisi kama mtindo katika kusanii tamthiliya teule. Mifano ya matumizi ya tashihisi katika tamthiliya ya *Mondlane na Samora* ni kama ifuatayo:

Moja ya tashihisi katika tamthiliya hii ni ile iliyotumiwa na Samora alipokuwa akizungumzia suala la usaliti miongoni mwa Waafrika. Katika miktadha hii anasema kuwa baadhi ya Waafrika wamenunuliwa na wageni. Kwa hivyo ili kuonesha tukio hilo la kihistoria Samora ametumia tashihisi inayosema

(i) *"Lakini nasema: Iache mifupa ya Wanamsubiji iwe shahidi…" (*uk.11).

Tashihisi hii imetumika ili kuonesha namna jamii za Afrika zilivyogawanyika wakati wa mapambano ya kupigania uhuru. Wapo waliosimama kwa nia safi na kuamua kujitoa mhanga ili kufanikisha ukombozi wa Afrika. Hata hivyo kundi la pili ni lile lililowasaliti Waafrika katika harakati hizoambalo liliwakilishwa na Nungo pamoja

na Kavandame.Vilevile, msanii ametumia tashhisi nyengine iliyojitokeza katika tamthiliya ya *Mondlane na Samora*isemayo:

> (ii) "…*wakifa polepole hali moto ukiziramba na kuzitafuna ngozi zao*" (uk. 101).

Tashihisi hii imetumiwa na msanii wakati Samora akisimulia namna Wareno walivyoleta maafa makubwa huko Msumbiji. Wareno walipambana na jeshi la Frelimo kwa muda wa miaka kumi. Katika vita hivyo wapambanaji walileta athari kubwa miongoni mwa watu wa Msumbiji. Katika mapambano hayo watu waliuawa kinyama bila ya kujali utu. Kutokana na athari hizo za kivita ndiyo msanii ametumia tashihisi inayosema

(i) "*Kaburi la Kireno limeumeza uhai wa Baba wa Taifa la Msumbiji*" (uk.60)

Katika tashihisi hii msanii ameonyesha namna harakati za mapambano dhidi ya ukoloni yalivyopelekea vifo vikiwamo vya majemedari wa Afrika. Kutokana na mapambano hayo Mondlane alipoteza maisha kwa kupewa bomu lililokuwa katika paseli na hatimae kumripukia. Mbogo (2016), anasema tarehe 3/2/1969 Mondlane alipokea paseli toka Lisbon akaifungua na bomu likamripukia na kumuua. Pia, katika mapambano ya Msumbiji askari wengi wa Tanzania walikufa wakati wa mapigano dhidi ya ukoloni huko Msumbiji, Zimbabwe, Angola na Namibia.

Vilevile, mtafiti amegundua matumizi mengine ya tashihisi yamejitokeza katika tamthiliya ya *Mondlane na Samora* pale msanii aliposema:

> (ii) "…*kwa kitambo kidogo tutasahau makaburi yanayoendelea kuitafuna miili na mifupa*…" (uk.18).

Tashhisi hii imetumiwa na Samora wakati akisubiri kwa hamu ndoa kati yake na Josina. Harusi hiyo iliadhimiwa kufanyika msituni katika harakati za kivita vya Frelimo dhidi ya mkoloni wa Kireno. Katika tashihisi hii msanii ameonyesha namna unyama uliokuwa ukifanywa na Wareno ulivyofanya watu wakose raha na kitulizano.

Hivyobasi,kwa kurejelea nadharia ya Umitindo ambayo ni moja kati ya nadharia inayoongoza utafiti huu, mtafiti aligundua kwamba matumizi haya ya tashihisi yamelandana na nadharia hii. Kama asemavyo Wamitila (2003), kwamba Umitindo hutumika kurejelea taaluma inayohusu uchunguzi wa lugha na matukio mbali mbali katika kazi ya fasihi. Ni taaluma iliyopo kati ya taaluma ya lugha na uchunguzi wa fasihi na jinsi lugha inavyotumika katika matini husika. Hivyo basi, matumizi ya tamathali ya semi ambayo nitashihisi katika tamthiliya ya *Mondlane na Samora* yamehusishwa a wahusika kutumia maneno maalumu kuvipa vitu uhai ili kusawiri miktadha ya mapambano dhidi ya ukoloni na athari zake kwa Waafrika. Kwa ujumla mbinu hii imetumiwa zaidi na mhusika Samora. Hali hii imeibua mtindo maalum wa kitashihisi kwa mtunzi wa tamthiliya teule. Huu ni mtindo wa matumizi ya lugha yanavyoendana na shughuli au tukio. Mlaga (2017) anaona kwamba mtindo kama matumizi ya lugha huweza kujitokeza kwa mwanafasihi kuwapa wahusika wake lugha sahihi kuendana na muktadha au shughuli inayofanyika. Hivyo, Samora amepewa matumizi ya tashihisi hizo zilizojadiliwa ili kukidhi mawasiliano katika muktadha wa mapambano ya kivita.

#### 4.4.1.1.4 Taswira

Taswira ni tamthali ya semi katika matumizi ya lugha inavyojengwa kwa picha ya hali au jambo fulani kwa msomaji.Picha hizi hujengwa akilini mwa msomaji kwa maelezo fulani na pia huweza kujengwa kwa matumizi ya tamathali za semi kama tashbiha na sitiari. Lengo la kutumia taswira ni kumfanya msomaji aelewe vile mtu au kitu kilivyo (Wamitila, 2008).Tamthiliya ya *Mondlane na Samora*imetumia aina hii ya tamathali ya semi ya taswira katika kueleza matukio mbalimbali. Hivyo basi, katika tamthiliya hii taswira mbalimbalizimebainishwa na mtafiti kupitia tamthiliya teule kama ifuatavyo:

Miktadha ya kwanza iliyotujengea taswira ni ile ya mapambano ya kivita. Katika mapambano hayo msanii ametujengea taswira inayosema

> "*Samora…! Samora…Unanisikia? Ova…Mondlane…Lete askari wengine upande huu. Ova…Tunahitaji haraka sanduku la dawa.Ova*(uk. 5).

Maelezo haya yametumiwana mhusika Mondlane wakati akizungumza na Samora kwanjia ya simu ya upepo. Mtindo huu wa mazungumzo umejenga taswira ambayo imemfanya mtafiti aone na kusikia kile ambacho kilikuwa kikiendelea katika mapambano kati ya Frelimo na Wareno. Taswira hii imetuonyesha namna watu walivyokuwa wakipata majeruhi na kulazimika kupata matibabu ili kuokoa maisha yao.

Vilevile, mtindo wa taswira umetumiwa na msanii wakati alipokuwa akisimulia namna wapambanaji wa Frelimo walivyoshiriki na kufurahia sherehe ya harusi kati

ya Josina na Samora. Sherehe hiyo ilifanyika msituni kwa sababu hata ndoa hiyo nayo ilifungwa huko huko msituni ambako mapambano yalikuwa yakiendelea:

> SAMORA: [*anaingia kavaa sare ya jeshi. AKA 47 inaning'inia begani. Anaingia akicheza…Anakaa kwenye gogo pembeni*]
> JOSINA: [*anaingia kabebwa na mama mmoja mgongoni. Kafunikwa mwili mzima. Anaketishwa mbali upande wa pili wa jukwaa, mkabala na Samora*]

Taswira hii imetumika ili kuonesha namna shughuli za kijamii kama vile ndoa, malezi na hata mapenzi ya wanandoa ziliathiriwa na vita. Matukio haya ya kijamii pamoja na kwamba yaliendelea lakini hayakurudisha nyuma harakati za ukombozi wa bara la Afrika. Kutokana na umuhimu wa mapambano, ndiyo maana hata wakati wa sherehe ya harusi yake mwenyewe Samora alikuwa amechukua silaha yake mgongoni.

Vile vile, matumizi ya taswira yamejitokeza katika mkutano wa viongozi wa Umoja wa Nchi Huru za Afrika wakiwa nchini Addis Ababa tarehe 24.05.1963.Katika taswira hii msanii ametumia mbinu ya sauti ambayo imetujengea picha ya kuyasikia maneno ambayo yalikuwa yakisikika kupitia sauti hiyo kama ifuatavyo:

> SAUTI: [*Toka kwenye spika*]. *Anayefuata kuhutubia mkutano huu wa kimataifa ni kiongozi kutoka nchi ya Zinja-anthropus. Zinja-anthropus aliishi katika Bonde la Oldivai takriban miakamilioni mbili iliyopita. Ni kiongozi kutoka nchi yenye kilele cha Kilimanjaro, milima mrefu kabisa kuliko yote barani Afrika. Waheshimiwa, ni wakati wa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere raisi wa Tanganyika, kuhutubia mkutano huu wa kihistoria hapa Addis Ababa, Ethiopia.* [*Makofi*].
> [*Kimya*]
> [*Nyerere anasimama sehemu ya kuhutubia*] (uk.1).

Katika dondoo hili msanii ametumia mbinu ya taswira ya sauti ili kuonesha namna viongozi wa bara la Afrika walivyokuwa wakifanya harakati mbalimbali ikiwa ni pamoja na kufanya mikutano ya kimataifa ya kuhamasisha umuhimu wa umoja na mshikamano katika harakati za ukombozi wa bara la Afrika. Kutokana na harakati hizo ndiyo hatimae kuliundwa jumuia iliyoziunganisha nchi zote za Afrika, yaani OAU.

Mbinu nyengine ya taswira ambayo imetumiwa kama kipengele cha mtindo ni wakati Josina alipokuwa msituni huko Msumbiji akiwasomesha wapambanaji wa Frelimo. Katika taswira hii mtunzi ametujengea picha ya namna juhudi za makusudi zilizokuwa zikifanywa na Josina ili kuhakikisha kwamba wapambanaji wanajua kusoma na kuandika. Taswira hii imejengwa kama ifuatavyo:

JOSINA: [*Anaonesha na fimbo*] *Sema*:
*a….e…i…o…u. Safi! Sasa mmoja mmoja.*
*Wewe soma!*
*Vizuri: Sema:*
*ba…be…bi…bo…bu. Safi:*
*Sema: baba…babu…*
*Sema: mama…mama…*
*Sasa tungo kamili: baba na mama… baba na mama*
JOSINA: *Nataka kuwakumbusha tena kuwa:kusoma*
*ni muhimu. Kamanda Mondlane, kabla hajatutoka,*
*kila mara alisisitiza kuwa: uhuru wa Msumbiji*
*lazima uende sambamba na vita dhidi ya*
*maadui watatu: ujinga, maradhi na umasikini*.(uk. 67)

Katika taswira hii msanii ametuonyesha namna elimu ilivyokuwa na umuhimu katika kuleta ukombozi. Msanii amedhihirisha kuwa harakati zozote zenye nia ya kuleta mabadiliko lazima ziambatane na watu kuelimishwa. Katika kushadadia umuhimu wa elimu katika jamii,Njogu na Chimerah (1999) wanasema kuwa elimu ni kitu

muhimu sana na haifai kutumiwa kama nyenzo ya utabaka na ukabila. Hii inamaana mwanadamu anapaswa kupata elimu bila ya kujali tabaka lake na kabila analotoka.

Mbinu hii ya matumizi ya sauti ambayo imetujengea taswira ni moja kati ya mihimili inayoweza kujenga picha katika akili za wasomaji ama wasikilizaji. Kama asemavyo Mdungi (2000), kwamba taswira huweza kujengwa kwa kutumia sauti ambapo kiungo kinachotumika kukamilisha taswira hii ni masikio. Mtindo huu wa matumizi ya taswira umelandana na nadharia ya Umitindo ambayo imeongoza lengo mahsusi la kwanza na swali la kwanza la utafiti huu. Mazungumzo haya yamelandana na kipengele cha usimulizi ambao umetegemea miktadha. Kama asemavyo Murumba (2013), kwamba usimulizi hurejelea hali ya kuwepo matukio katika hadithi inayosimuliwa. Kwa mantiki hii msanii ametumia mtindo wa sauti ya mkutanoni ili kuonesha taswira ya juhudi za viongozi wabara la Afrika wakati wa ukombozi wa bara hilo.

Taswira nyengine kama mtindo ambayo imetumiwa na msanii wakati akisimulia namna Mondlane alivyoripukiwa na bomu.Kutokana na tukio hili Mwalimu Nyerere alihudhuria katika msiba huo na kuhutubia hadhira hiyo kama ifuatavyo:

NYERERE: [*anaongea, anahutubia*]
*Wana wa Afrika*
*Wana wa Msumbiji*
*Vidonda havijapona bado*
*Damu bado inachuruzika*
*Tunalia machozi*
*Kwa haya mengi majonzi*
*Wanapokufa wanamapinduzi*
*Na kuwaacha wao wapenzi.*
*Lakini mioyo haitakufa ganzi*
*Kwani bado tunayokazi*

*Ya kuvitengua vyote vitanzi*…" (uk. 60-61).

Taswira hii imetumika ilikuonyesha namna Waafrika walivyopoteza maisha kutokana na mapambano ya Wakoloni wakati wa kudai uhuru. Mbinu kadhaa zilitumiwa na wakoloni ili kudhoofisha harakati za kudai uhuru wa bara hili.

Maelezo haya ya mhusika Nyerere yanasawiri nadharia ya Umitindo kutokana na mhusika huyo kuchagua misamiati maalumu kama vile; "*Vidonda havijapona bado*"ili kukidhi haja ya mawasiliano kulingana na tukio hilo la kuomboleza. Hapa mhimili wa kiwango cha umbo wa nadharia ya Umitindo umejitokeza kutokana na utumiaji wa misamiati ambayo imekidhi rejista ya msibani. Hivyobasi, mtindo huo ndioalioutumia msanii wa kumpa mhusika maelezo ambayo yamelenga kubeba ujumbe alioukusudia. Wazo hili limeelezwa na Mlaga (2017), kwamba maelezo ya wahusika huweza kupewa lugha ambayo hutumika katika miktadha maalumu kama ni mtindo wa msanii.

#### 4.4.1.1.5 Takriri

Takriri inafasiliwa na Wamitila (2008), kwamba ni hali ya kurudiarudia wazo, silabi, maneno au sentensi kwa lengo la kusisitiza jambo linalozungumzwa. Mawazo haya yamelingana nayale ya Faki (2015), ambaye anasema kuwa takriri katika kazi ya fasihi ni urudiaji wa silabi, maneno au sentensi kwa nia ya kusisitiza jambo linalozungumziwa na mtunzi. Pia, katika ushairi takriri huweza kufanyika ili kuleta mlingano sawa wa sauti. Data zilizokusanywa na mtafiti kutoka tamthiliya ya *Mondlane na Samora*zimeonesha mtunzi wa tamthiliya hii ametumia mbinu ya

takriri kama sehemu ya mtindo. Hivyo matumizi hayo ya takriri kama mtindo wa mtunzi yamefanyiwa uchambuzi kama ifuatavyo:

Wakati Nyerere akiwa jukwaani akihutubia katika mkutano wa viongozi wa Umoja wa Bara la Afrika huko Addis Ababa alisikika akirudia rudia baadhi ya maneno na virai ambavyo vinawafanya viongozi wengine katika ukumbi huo wa mkutano kufanya takriri. Kwa mfano, mwishoni mwa hotuba ya Nyerere kuna urudiaji uliojitokeza kama hivi ifuatavyo:

> NYERERE: Na mintarafu ndugu yangu rais Sekou Toure; Tanganyika tuko tayari kutenga asilimia wahedi ya bajeti ya nchi yetu kwa ajli ya ukombozi wanchi kusini mwa Afrika!
> VIONGOZI: Viva!
> NYERERE: Ndiyo! Na mintarafu ndugu yangu Waziri Mkuu wa Algeria, Mheshimiwa Ahmed Ben Bella "tuko tayari kufa kidogo" ili kung`oa udhalimu wa ukoloni barani Afrika. Asanteni kwa kunisikiliza. Aluta Continua!
> VIONGOZI: Aluta Continua!
> NYERERE*: Viva Afrika!*
> VIONGOZI: *Viva!*

Dondoohilo hapo juu limebainisha namna msanii alivyotumia mbinu ya takriri kwa kurudia neno ama baadhi ya vifungu vya maneno kama vile; "*mintarafu ndugu yangu*" ambapo takrri hii imetumika kuondoa utabaka katika bara la Afrika na hivyo kuonyesha kwamba Waafrika wote ni ndugu. Pia, kuna kurudia rudia maneno yaliyosema "*Aluta Continua*." Kifungu hiki cha maneno kimerudiwa rudiwa ili kuonesha haja ya kuendeleza mapambano hadi pale Afrika itakapopata uhuru.Maneno mengine yaliyotumiwa kama mtindo wa takriri katika dondoo hili ni "*Viva Afrika*." Takriri hii imetumika ili kusisitiza na kuunga makubaliano na mawazo ya harakati za ukombozi wa bara la Afrika.Kwa ujumla vifungu hivi vya

maneno vimekuwa vikirejewa rejewa katika sehemu kadhaa za tamthiliya hii na kufanya ndiyo msingi wa kusawiri mawazo yanayopatikana katika tamthiliya hii.Kupitia mhusika Mondlane msanii ametumia takriri pale aliposema:

"*Lazima Waafrika tuungane! Tuwe nchi moja, tuwe na jeshi moja*..." (uk.7).

Katika takriri hii kuna kurejewa rejewa kwa neno "*moja*"Mbinu hii ya takriri imetumiwa na msanii ili kuhamasisha umoja wa Waafrika katika harakati za ukombozi wa bara la Afrika. Mtafiti amebaini kuwa msanii alionyesha kwamba ili kupata ukombozi wa kweli bara hili lazima liondokane na utabaka wa aina zote. Hii ndiyo sababu wahusika wote wakuu katika tamthiliya hii wameonekana wakihamasisha umoja na mshikamano. Kwa ufupi basi, kila taifa linapaswa kulisaidia taifa jengine ili kufanikisha ukombozi. Mawazo haya yameungwa mkono na Njogu na Chimerah(1999) wakieleza kwamba mtu hafanikiwi kwa kutegemea tabaka lake au jamii yake.Matumizi mengine ya takriri kama mbinu ya mtindo yametumiwa na Josina wakati akizungumza na mpenzi wake Samora kuhusu suala la mapenzi pale aliposema

"*Mimi nakuchagua wewe. Nakutaka wewe. Nakupenda wewe…*" (uk.18).

Mtindo huu wa takriri umetumiwa na msanii ili kuonyesha namna Josina alivyokuwa na mapenzi ya dhati kwa Samora. Mapenzi hayo yalimpelekea kuzirejelea chanjo hizo za kimapenzi kama vile "*mimi*" na "*wewe*," "*nakutaka*" na "*nakupenda*" ili kumhakikishia Samora, mapenzi yaliyofichika kifuani mwake. Hii ndiyo sura ya mapenzi yanayofaa kuigwa ili kujenga uaminifu miongoni mwa wapendanao. Mapenzi haya yalitiliwa nguvu na Robert (1969) katika diwani ya "*Mapenzi Bora*"

ambapo ameonesha kwamba mapenzi bora ndiyo msingi wa mafanikio ya kila jambo katika maisha ya kila siku.

Kwa mnasaba wa nadharia ya Umitindo, matumizi haya ya takriri ni miongoni mwa tamathali za semi za kimtindo ambazo mtafiti amegundua kuwa msanii amechagua misamiati teule yenye kujikita katika miktadha maalumu. Kwa mfano, wakati msanii akizungumzia maswala ya mapenzi kati ya Josina na Samora,ameteua misamiati ambayo inaathari ya kuonyesha upendo kati ya wahusika hawa. Matumizi haya ya maneno hutegemea miktadha maalumu,kamailivyosemwa na Jilala (2016), na Mlaga (2017), kwamba mtunzi wa kazi za fasihi huteua misamiati maalumu kutegemea miktadha ya jambo analolizungumza kama sehemu ya mtindo wake.

#### 4.4.1.1.6 Tanakalisauti

Tanakalisauti ni tamathali za semi zinazotoa au kuiga sauti za mlio wa vitu, watu au wanyama (Kahigi na Mulokozi 1979). Mtafiti amebaini kuwa katika tamthiliya ya *Mondlane na Samora*,mwandishi ametumia tanakalisauti kuwa nikipengele cha mtindo. Mathalani, wakati Samora akizungumza na Josina wakiwa huko msituni msanii ametumia tanakalisauti inayosema

> *"…nitawamiminia risasi:Titititi! Traaa! Traaa! Traaa! Bumuu!"* (uk. 24).

Tanakalisauti hii imetumika ili kuoneshanamna Samora alivyokuwa na ushujaa. Alikuwa haogopi mapambano ya kivita. Kutokana na ushujaa huo ndiyo maana aliweza kujigamba mbele ya Josina namna alivyopambana na jeshi la Wareno.Katika tamthiliya ya *Mondlane na Samora*, mtafiti amegundua matumizi ya tanakalisauti nyengine iliyotumikaambayo inasema:-

*"Mara tunasikia Makombora ya Mreno Taaa! Taaa!Bum! Bum!"* (uk.48).

Tanakalisauti hii imetumiwa na Josina ambapo alisimulia namna walipokuwa msituni walivyovamiwa na mashambulizi kutoka kwa Wareno. Kupitia tanakalisauti hii msanii ameonyesha namna Waafrika wakati wa harakati za mapambano ya kutafuta uhuru walivyoishi maisha ya hatari. Maisha ya kuviziana kati ya wapambanaji wa Frelimo na Wareno. Pia, Wareno walikuwa na silaha nzito ukilinganisha na Waafrika. Kutokana na hali hiyo baadhi ya maeneo Waafrika walishindwa kutokana na silaha duni. Kwa mfano, Hussein (1969) katika tamthiliya ya *Kinjeketile*alionyeshanamna Watanganyika walivyoshindwa na Wajerumani katika vita vya Maji Maji kutokana na Wajerumani haokuwa na silaha nzito ukilinganisha na zile za Watanganyika.

Kwa kuzingatia nadharia ya Umitindo, mtafiti aligundua namna mbinu hiyo ya Tanakalisauti ilivyotumika kwa lengo la kuonyesha jinsi ya uonevu na chuki walizokutana nazo wapiganaji wa Msumbiji dhidi ya maadui zao wa Kireno kiasi ambacho waliteketeza na kuwaangamiza Wanamsumbiji.

#### 4.4.1.1.7 Mdokezo

Cuddom (1998) na Mulokozi (2002) wanasema kwamba mdokezo ni mtindo wa lugha ambao msanii hutoa nafasi ya kuishirikisha hadhira yake kutokana na uzoefu fulani wa maisha. Hivyo datazilizokusanywa na mtafiti katika tamthiliya ya *Mondlane na Samora* zimeonyesha kwamba tamthiliya hii imetumia mbinu ya mdokezo kuwa kipengele cha mtindo kama ifuatavyo:

Kwanza imeelezwa kuwa baada ya kukagua majeruhi waliokufa Mondlane alitumia mawasiliano ya simu ya upepo ili kutoa maelekezo ya kuhitajika askari zaidi. Pia, ni katika miktadha hii ambayo Mondlane aliwasiliana na Samora ili alete masanduku ya dawa zaidi. Mdokezo huo ulikuwa ukisema hivi:

> MONDLANE:[*baada ya kukagua majeruhi na waliokufa anaongea na Ova-ova*] *Samora..! Samora… Unanisikia? Ova…Mondlane…Lete askari wengine upande huu. Ova…Ova… tunahitaji haraka sanduku la dawa. Ova.* [anazima ova] (uk.5).

Mbinu hii ilitumika ili kuonesha namna hali ya mapambano ilivyokuwa katika vita vya Frelimo. Watu wengi walipoteza maisha na wengine kubakia na ulemavu kutokana na mapambano hayo. Katika wakati huo kulihitajika ongezeko la wapambanaji zaidi ili kuendeleza harakati za kugombania uhuru wa bara la Afrika. Pia, madawa nayo yalihitajika ili kuwatibu wale waliopata majeraha kutokana na mapambano ya kivita.

Vilevile, mtindo mwengine wa mdokezo uliojitokeza katika tamthliya hii ya *Mondlane na Samora* ni ule uliosema:

> *"Nani? ...Namba ya siri? ...Sawa …Karibieni"*(uk.8).

Mtindo huu ulitumiwa na Askari wa Frelimo alipokuwa anapokea simu kutoka kwa askari wengine wa Frelimo. Katika mtindo huu mwandishi ameonyeshwa namna vifaa vya mawasiliano vilivyokuwa naumuhimu wakati wa harakati za mapambano ya kupigania uhuru ili kuwasiliana na wapambanaji kutoka eneo moja na jengine. Kuwepo kwa njia hizo za mawasiliano kuliwezesha kupanga mapambano na hata kuagizia vifaa vilivyohitajika kwa wakati huo.

Mfano mwengine wa mdokezo ni ule uliotumiwa na Josina wakati akimuhakikishia Samora namna alivyompenda. Mwandishi alitumia aina hii ya mdokezo ili kumuachia nafasi msomaji ama msikilizaji kuweza kujaza maelezo ambayo yangeweza kuwiana na miktadha ya mazungumzo ya kimapenzi yaliyosimuliwa na Josina. Kama alivyotueleza msanii hivi ifuatavyo:

> *"Hata mimi nakupenda* [*kimya*] *Samora…nina hamu … natamani uipande hima mbegu ya pendo lako hapa. Ukamuumbe kiumbe ndani ya tumbo hili la kike ili nikuzalie pacha* [*Samora anacheka*]*Usicheke. Nitakuzalia pacha mvulana na msichana. Kisha tutawaondoa pacha wetu huku vitani." (uk.19).*

Kwa mnasaba wa nadharia ya Umitindo, mtafiti anashawishika kusema kuwa mtindo huu wa kutumia mbinu ya mdokezo imempa nafasi msomaji ama msikilizaji kukamilisha maelezo ambayo yamehusisha dhana nzima ya mawasiliano katika harakati za maisha ya kila siku. Vile vile mtindo huo umedokeza umuhimu wa mahusiano ya dhati kwa wapendanao hasa kupitia muhusika Josina katika miktadha ya mapenzi. Mtafiti amebaini kwamba msanii ametumiamtindo huo ilikudokeza mazungumzo ya kimapenzi kutokana na sababu za kiutamaduni. Kama inavyoeleweka kuwa utamaduni wa msanii huyu (Emmanuel Mbogo) hauruhusu kuzungumza masuala ya mapenzi waziwazi. Mtindo huu umeshadadiwa hatimae na Mutembei (2012), pale alipoona kuwa mdokezo huweza kutujengea korasi kama kimya cha kiutamaduni kutokana na mtunzi wa kazi za fasihi kuepuka kuzungumza mambo wazi wazi kwa sababu ya miiko ya utamaduni.

#### 4.4.1.1.8 Nidaa

Nidaa ni tamathali ya semi inayoonyesha kushangazwa na jambo fulani (Wamitila, 2008). Ni matumizi ya lugha ambayo mtunzi hutumia maneno hayo na kuleta mshangao kwa kile alichokisema. Mtunzi wa tamathiliya hii ya*Mondlane na Samora* ametumia mbinu hii katika kazi yake kama ifuatavyo:-

i) *Viva Afrika!* (uk. 1)
ii) *Aluta Continua! (*uk.2*)*
iii) *Mamaaaa! Niacheni! Naumia! Nakufa! Washenzi ninyi!* (uk.6)
iv) *Mwalimu! Nyerere! Rudi haraka! Rudi Haraka!Ova! …(*uk .59)
v) *….No! Hapana! Edwardo! No! My God! Have mercy…!* (uk .59)

Kwa kurejelea nadharia ya Umitindo, ambayo msingi wake mkuu ni kushughulikia mitindo mbalimbali iliyojitokeza katika kazi za fasihi, mtafiti amegundua kuwa matumizi ya nidaa yamesaidia sana kazi ya mwandishi kuifikia hadhira na kujenga tafakuri ya hali ya juu katika tukio au jambo lililojadiliwa. Matumizi hayo ya nidaa husaidia sana kujenga na kuibua fikra mpya ambazo zitarahisisha kufika hatua ya mafanikio katika msingi wa jambo lililoelekezwa kwa hadhira lengwa.

#### 4.4.1.1.9 Tafsida

Tafsida ni utumiaji wa maneno ambayo huficha karaha ya waziwazi, maneno hayo hutumika ili kuepuka karaha.Msanii ameonekana akitumia maneno ya tafsida ili kukidhi haja ya mawasiliano kutegemea miktadha ya wasomaji wake. Mathalani, mtunzi ametumia tafsida iliyosema:

*"Ufiche uso wako katikati ya bonde la dodo hizi!Ni zako?!"*(uk. 20).

Tafsida hii imetumiwa na mwandishi kupitia kwa muhusika Josina alipomwambia Samora afiche uso wake katikati ya matiti. Pia, msanii ametumia tafsida iliyosema

> "*Siku ya leo kichwa cha kobe kinaenda kupata hifadhi ndani yagamba lake na kuyafaidi maisha*" (uk. 38).

Katika tafsida hii msanii ameonyesha namna alivyo na ujuzi wa kuwapa wahusika wake lugha ya tafsida ili kuepusha karaha. Badala ya kusema kwamba usiku wa leo Samora atafanya ngono mtunzi aliteua mtindo wa mazungumzo ambao unapunguza ukali wa kile kilichozungumziwa.

Kwakuhusisha nanadharia ya Umitindo, mtafiti ameona kuwauteuzi huu wa misamiati ambayo imeficha karaha wakati wa mazungumzo ni mtindo wa mtunzi. Kama asemavyo Mlaga (2017), kwamba mtunzi huweza kuchagua misamiati maalumu ambayo inaakisi miktadha fulani ya mazungumzo ikawa ni moja kati ya mtindo wa mtunzi wa kazi ya fasihi.

Kwa maelekezo ya nadharia ya Umitindo ambayo imelenga kuweka wazi matumzi ya vipengele mbalimbali vya kimtindo katika kazi za fasihi, mtafiti ameona kuwa matumizi ya Mchanganyondimi/lugha husaidia sana kubainisha athari na asili za wahusika katika maisha yao ya kila siku. Hali hii hujitokeza na kuchangiwa na sababu mbalimbali ikiwemo uwezo wa taaluma, mamlaka, fedha na utawala au mazingira walionao baadhi ya wahusika katika mfumo na asili ya maisha yao.

**Jadweli 01: Muhtasari wa vipengele vya Lugha vilivyotumiwa kuwa Mtindo**

| Nambari | Vipengele vya Lugha vilivyotumiwa kuwa Mtindo |
|---|---|
| 01 | Tashbiha |
| 02 | Sitiari |
| 03 | Tashbiha |
| 04 | Tashhisi |
| 05 | Taswira |
| 06 | Takriri |
| 07 | Tanakalisauti |
| 08 | Mdokezo |
| 09 | Misemo |
| 10 | Tafsida |
| 11 | Mchanganyondimi |

Chanzo: Data kutoka katika tamthiliya ya *Mondlane na Samora*. Septemba, 2018

Kwa udhati kabisa,mtafiti amefanya uwasilishaji nauchambuzi wa data zilizokusanywa zilizohusu matumizi ya mtindo yaliyojikita katika kipengele cha lugha. Hivyo katika utafiti huu uwasilishaji na uchambuzi wa data ambazo zimehusu vipengele vyengine vya mtindovilivyobainishwa katika tamthiliya ya *Mondlane na Samora* ni kama vifuatavyo:

### 4.4.2 Vipengele vyengine vya Kimtindo katika Tamthiliya ya Mondlane na Samora

Katika utafiti huu wenye mada: *Kuchunguza mtindo na dhamira katika tamthiliya ya Mondlane na Samora,* mtafiti kwa kuzingatia lengo mahususi la kwanza na swali la kwanza la utafiti, amebaini vipengele vyengine vya kimtindo katika tamthiliya teule.Uwasilishaji na uchambuzi wa vipengele hivyo vyengine vya kimtindo mbali

ya kipengele cha awali cha matumizi ya lugha ambacho tayari kimeshawasilishwa na kuchambuliwa kwa kina, ni kama ifuatavyo:

#### 4.4.2.1 Nyimbo

Mulokozi (1996), anasema kwamba nyimbo ni kila kinachoimbwa. Data za utafiti huu zimeonyesha kuwa mtunzi ametumia mtindo wa nyimbo ambazo ziliimbwa na wahusika kama sehemu ya matukio ya kijamii. Kwa mfano, katika (uk. 105-106) kuna matumizi ya nyimbo ambayo ilikuwa ikiimbwa na Samora huku akiitikiwa na umati wa watu. Nyimbo hiyo ilikuwa inasema ifuatavyo:

SAMORA: *Viva, viva, viva viva Frelimo*
*Viva, viva, viva viva Frelimo*
*Viva, viva, viva viva Frelimo*
*Viva, viva Frelimo!*
UMMATI: *Viva, viva, viva viva Frelimo*
*Viva, viva, viva viva Frelimo*
*Viva, viva, viva viva Frelimo*
*Viva, viva Frelimo!* (uk.105-106)

Wimbo huu umetumiwa na msanii kama mtindo wa kikorasi ili kuonesha wazo/dhamira kuu ya tamthiliya hii yaani Harakati za ukombozi. Wimbo huu umetokea mwishoni mwa tamthiliya hii kama ni kifupisho cha mawazo yaliyomo ndani ya mchezo huu. Kama asemavyo Mutembei (2012), kwamba wimbo kama mtindo wa kikorasi huweza kutokea mwishoni ili kufanya muhtasari wa kile kilichoelezwa hapo kabla.Wimbo huu umeimbwa baadaa ya wapambanaji kupata ushindi ambapo Frelimo walikabidhiwa madaraka ya uongozi wanchi ya Msumbiji.Hivyobasi,pambazuko hilo jipya ambalolilijenga matumaini ya kuondokana na kila maovu na ukiukwaji wa haki za kibinadamu.

Wimbo mwengine katika tamthiliya ya *Mondlane na Samora* ni ule ulioimbwa na raia wa Msumbiji wakiongozwa na Samora. Wimbo huu uliimbwa ili kuhamasisha harakati za ukombozi kama ifuatavyo:

> *"Viva Frelimo, vivaa!*
> *Viva Frelimo, vivaa!*
> *Vivaaa Mozambique!*
> *Viva Frelimo, vivaa!*
> *Viva Frelimo, vivaaa!*
> *Vivaaa na Tanzania!"* (uk 42-43)

Mwandishi ameutumia wimbo huu ili kuwatia hamasa wapiganaji.Kama asemavyo Mulokozi (1996), kwamba wimbo hutumika ili kutia hamasa katika vita. Kutokana na dhima hiyoSamora ametumia wimboili kuwaunganisha pamoja wapambanaji bila ya kujali ukabila wala utaifa kwa lengo la kumuondoa mkoloni. Wimbo huu umetumia neno"Tanzania" ili kuonesha namna Watanzania walivyokuwa mstari wa mbele kuhakikisha Afrika imejikomboa.

Kwa kurejelea nadharia ya Umitindo ambayo ndiyo iliyoongoza lengo mahsusi la kwanza na swali la kwanza la utafiti huu ni kwamba,mtindo wa matumizi ya nyimbo umelandana na nadharia hii. Kama asemavyo Murumba (2013), kwamba mwanafasihi huweza kutumia sajili mbalimbali katika kazi yake kama sehemu ya mtindo. Hivyo basi, utumiajihuu wa nyimbo ni moja kati ya mtindo uliotumiwa na msanii ili kuonyesha mawazo yake kwa jamii kuhusu historia ya harakati za kupambana na ukoloni katika nchi ya Msumbiji.

#### 4.4.2.2 Barua

BAKIZA (2010) wanaeleza, Barua ni ujumbe wa maandishi wenye mtindo maaalum unaopelekwa kwa mtu au katika taasisi. Mdee na wenzake (2011) wanasema, Barua ni maandishi yanayotumwa kwa mtu yenye ujumbe fulani ambayo hutumwa kwa njia ya mkono au kwa kupitishia posta au elektroniki.

Data za utafiti huu zimeonyesha kuwa mtunzi wa tamthiliya ya *Mondlane na Samora* ametumia mtindo wa barua kama sehemu ya mawasiliano kati ya wahusika wake. Kwa mfano, ipo barua iliyoandikwa na Mondlane kumpelekea Janet. Katika barua hiyo Mondlane alimueleza Janet hatari iliyomkabili kutokana na wasaliti ambao walikuwa na njama ya kutaka kumuua. Hata hivyo, Mondlane alimtaka Janet asiwe na wasiwasi kwa hilo. Iwapo atapoteza maisha alimsihi aendelee kuwalea vizuri watoto wao. Barua hiyo ilikuwa inasema hivi:

> "*Mpenzi Janet, nahisi kuna kenge*
> *wenye meno ya chuma wanaotamani*
> *kuirarua roho yangu. Nikifa yaache*
> *machozi yatiririke, lakini usikate*
> *tamaa. Tunza watoto wetu:*
> *Eduardo, Jennifer na Nyeleti.*(uk.29)

Kwa kuhusisha na nadharia ya Umitindo, mtafiti amebaini kuwa matumizi ya barua katika tamthiliya ya *Mondlane na Samora*, yamekusudia kuonesha suala zima la usaliti katika jamii. Msanii alionyesha kwamba usaliti ni jambo la kihistoria na halikuanza hivi karibuni tu bali tatizo hili lipo tangu wakati wa ukoloni. Mapambano ya kupigania uhuru dhidi ya wakoloni yalikwazwa na baadhi ya Waafrika kama vile mhusika Nungo na Kavandame ambao waliweka mbele maslahi yao binafsi. Suala la

usaliti pia limewahi kuelezwa na Salim (2015), kuwa hata ndugu wa damu huweza kusalitiana.

#### 4.4.2.3 Hotuba

Mdee na wenzake (2011) wanaweka wazi kuwa, Hotuba ni maelezo au mazungumzo yanayohusu jambo maalum kama siasa ambayo hutolewa hadharani na mtu mmoja.Hotuba ni maelezo ambayo, hutolewa na mtu mbele ya watu. Hutolewa kwa madhumuni maalumu.Mtunzi wa tamthiliya ya *Mondlane naSamora* ametumia mtindo wa hotuba kama ni mbinu ya kufikisha ujumbe kwa jamii. Kwa mfano katika tamthiliya hii ipo hotuba iliyotolewa na Mwalimu Nyerere huko Addis Ababa kwenye mkutano wa Umoja wa Nchi Huru za Afrika(OAU) akiwa na lengo la kutaka nchi za Kusini mwa Afrika ziondokane na minyororo ya ukoloni na ubaguzi wa rangi. Hotuba hiyo ilikuwa inasema ifuatavyo:

> NYERERE: *“Naomba nianze kwa kuwasalimu kwa mtindo wa ndugu zetu wa Frelimo: Viva Frelimo!*
> VIONGOZI: *Viva!*
> NYERERE: *Aluta Continua!*
> VIONGOZI: *Aluta Continua!*
> NYERERE: *Mwenyekiti, mwenyeji wetu: Mstahiki Mfalme Haile Salassie.Viongozi wa Nchi huru za Afrika ikiwa ni pamoja na Rais Kwame Nkrumah,Gamal Abdel Nasser, Ahmed Sekou Toure, Ahmed Ben Bella…Itifaki inazingatiwa. Ndugu zangu. Nataka nianze kwa kusema kuwa: hatukuja Adiss Ababa ili kujadili iwapo tunataka Afrika iwe huru au la. Hata maadui wakubwa wanajua kuwa: lazimatujikomboe toka minyororo ya ukoloni…Hivyo,tumekutana hapa Adiss Ababa ili kutafuta mkakati wa pamoja wa kuleta umoja huo…”* (uk.1- 4).

Hotuba hii iliyotolewa na Nyerere ililenga kuzitaka nchi za Afrika kuwa na umoja ulioimara ambao utapelekea kupatikana kwa uhuru wa kweli. Nyerere alieleza kuwa

kila mmoja kati yetu anahitaji kupambana na wakoloni kwa sababu ya kutaka kuwa huru. Hata hivyo mbinu muhimu ya kuondokana na ukoloni ni kwa bara la Afrika kuwa na umoja ili kuhakikisha kila nchi ya Afrika imejikomboa kutoka katika utumwa wa wakoloni. Njogu na Chimerah (1999), wanaona kuwa wakoloni waliifanya Afrika kuwa tabaka lililokandamizwa kutokana na miktadha hiyo. Jilala (2016), anaona kwamba kutokana na ukandamizaji unaofanywa na wakoloni hadi leo ipo haja ya kupiga vita ukoloni. Swali ambalo mtafiti anajiuliza hapa ni Je, Waafrika wamejikomboa aubado wako katika mikono ya wakoloni. Jawabu ni kwamba hadi leo Afrika bado imo katika mikono ya wakoloni. Yaelekea mawazo ya mhusika Nyerere kushindwa kuleta umoja wa kweli wa Waafrika ndiko kunakopelekea kuendelea kwa ukoloni katika bara hili.

Kwa mnasaba wa nadharia ya Umitindo, mtafiti amebaini kuwa matumizi haya ya hotuba ndani ya tamthiliya ni mbinu ya kimtindo iliyoteuliwa na mtunzi wa tamthiliya hii. Kama wasemavyo Murumba (2013), Jilala (2016) na Mlaga (2017), kwamba matumizi ya sajili mbali mbali katika kusana kazi za fasihi huweza kutumiwa na mtunzi wa kazi za fasihi ili kujenga mitindo ya kazi za fasihi.

#### 4.4.2.4 Mawasiliano ya Simu

Simu ni chombo / kifaa cha kielektroniki ambacho hutumiwa na watu kwa ajili ya mawasiliano.Mtindo huu wa mawasiliano ya simuumetumiwa na Mondlane wakati alipokuwa akikagua majeruhi na maiti waliokuwa wamelala baada ya kushambuliwa na jeshi la Wareno.Mawasiliano hayo yalikuwa hivi:

> *"Samora…!Samora…Unanisikia? Ova…Mondlane… Lete askari wengine upande huu. Ova…Tunahitaji haraka sanduku la dawa. Ova*." (uk.5)

Mawasiliano haya ya simu yaliyofanywa kati ya Adward na Samora yaliyotumia simu aina ya *redio call* wakiwa msituni katika mapambanoambayo yalikuwa yameonesha ni mbinu ya kimtindo iliyoteuliwa na mtunzi wa tamthiliya hii, namna watu walivyokuwa wamejeruhiwa kutokana na mapambano ya kivita.

Kwa kutilia mkazo wa nadharia ya Umitindo, mtafiti ameona kuwa matumizi haya ya mawasiliano ya simu katika tamthiliya ya*Mondlane na Samora*,yamekuwa na umuhimu mkubwa kutumika kuwa ni kielelezo chenye tija na manufaa makubwa ya kurahisisha upatikanaji wa huduma ya afya kwa maslahi ya wapambanaji wakiwa vitani.

#### 4.4.2.5 Matangazo ya Redioni

Matangazo ya kwenye redio ni mtindo mwengine uliotumiwa na msanii katika tamthiliya ya *Mondlane na Samora*. Matangazo hayo yalirushwa kutoka viwanja vya mkutano ambapo iliripotiwa na redio ya BBC kupitia ripota wake BBC1 na BBC2. Matangazo hayo yalikuwa yanahusu uhuru wa Frelimo na yalikuwa yanasikika hivi:

> BBC1*:Hii ni BBC London…Karibuni wasikilizaji na wapenzi wa BBC London. Habari zinazogonga vichwa vya habari. Samora Moses Machel ahutubiamkutano mkubwa huko Beira…Habari kamili.Baada ya makubaliano ya Lusaka, Samora Moses Machel, Rais wa Frelimo atahutubia mkutano mkubwa kwa mara ya kwanza mjini Beira jioni hii. BBC2 anaripotimoja kwa moja toka mjini Beira. BBC2 unanisikiliza?*
> BBC2*: Nakupata vizuri BBC1.*
> BBC1*: Hali ikoje hapo mjini?*
> BBC2*: Ni mjini Beira. Mji ulioko kusini kabisa mwa Msumbiji. Ni katika Uwanja Mkubwa wasoka wa Beira. Watu kwa maelfu*

*wanamiminika kuja kumsikiliza Samora Moses Machel* (uk 94 106)

Kwa kuunganishwa na nadharia ya Umitindo, mtafiti amegundua kuwa matumizi ya mtindo wa matangazo redioni kupitia kwa msanii kuwa amekusudia kuonesha namna hali ilivyokuwa huko Msumbiji siku ya kukabidhiwa uhuru kutoka kwa Wareno. Watu walikuwa na shauku kubwa. Kutokana na tukio hilo la kihistoria viongozi na wananchi kila pembe walijawa na shauku ya kupatikana kwa uhuru huo.

#### 4.4.2.6 Rejista ya Jeshini

Rejesta ni mtindo wa lugha inayotumika mahali penye shughuli fulani ambayo ni tofauti na lugha ya kawaida. Katika tamthiliya ya *Mondlane na Samora*utafiti huu umebaini uwepo wa matumizi ya rejista ya jeshini. Kwa mfano, mtunzi ameitumia sajili hii ya lugha ya jeshini wakati wa mazungumzo kati ya Mondlane, Samora na Askari. Mazungumzo hayo yalikuwa kama ifuatavyo:

MONDLANE: *Yuko wapi Kanali Mahfoudh?*
SAMORA*: Kanali Mahfoudh amechukua*
*batalioni moja, ameelekea*
*Bwawa la Kabora Bassa.*
MONDLANE*: Tunahitaji kupanga mikakati mipya.*
*Wengine toweni maiti. tayarisheni*
*makaburi. tutawazika mashujaa wetu*
*baada ya mkutano huu mfupi.*
ASKARI: *Sawa Afande* (uk 8-9)

Katika dondoo hili msanii ametuonyesha namna wanajeshi wa Afrika walivyokuwa wakati wa harakati za ukombozi. Wakati huo kulikuwa na wanajeshi waliokuwa na vyeo ambao walitoa maelekezokwa wenzao. Pia, katika dondoo hili imeonyeshwa

namna raia waliokuwa hawana hatia walivyopoteza maisha kwa sababu ya kudai nchi yao.

Kwa kuhusisha na nadharia ya Umitindo, utafiti huu umeona kuwa mazungumzo baina ya Mondlane, Samora na Askari yalikuwa na manufaa makubwa katika harakati za ukombozi. Mazungumzo hayo ambayo yalilenga kuhusu maelekezo ya viongozi kwa wapiganaji katika vita. Hivyo basi mtindo huu wa mtunzi kuteua maneno maalumu ambayo yameshabihiana na miktadha umeleta faida katika kufikisha ujumbe kwa jamii kuhusu kujitolea kwa ajili ya taifa dhidi ya ukoloni. Kwamfano msanii ametumia maneno kama vile "*komanda,*" "*vita,*" "*batalioni,*" "*kanali,*" na "*afande*" ambayo yalitumiwa na wanajeshi.Uchotaji huu wa misamiati maalumu katika miktadha umelandana na nadharia ya Umitindo katika msingi wa kiwango cha umbo. Murumba anasema kwamba mwandishi hufanya uteuzi wa wahusika aliowatumia kwenye kazi yake, usimulizi alioutumia na mtazamo wake na mada aliyoishughulikia ili kukidhi kufikisha ujumbe alioukusudia.

#### 4.4.2.7 Rejista ya Shuleni

Rejista ya Shuleni ni mtindo unaotumiwa hasa na wanataaluma kwa mfano wanafunzi kwa walimu , walimu kwa walimu au wanafunzi kwa wanafunzi katika miktadha ya shuleni au taasisi za elimu. Mtafiti amebaini kuwa msanii ametumia rejista ya shuleni katika tamthiliya ya *Mondlane na Samora.*Kwa mfano, katika tamthiliya hii Josina amepewa nafasi ya kuwa mwalimu ili kuwafundisha wapigania uhuru wawe na uwezo wa kujua kusoma na kuandika. Kutokana na nafasi hiyo Josina alikuwa mwalimu akiwa msituni. Mtindo huu umejitokeza ifuatavyo:

JOSINA*: Sasa kila mtu achukue daftari lake.*
*Nataka mwandikesomo liliko ubaoni*
*Sawa?*
DARASA*: Sawa mwalimu.*
JOSINA*: Nataka uandike mwandiko safi.*
*Mwandiko unaosomeka. Sawa?*
DARASA*: Sawa mwalimu.* (uk. 67)

Kwa muongozo wa nadharia ya Umitindo, Utafiti umebaini kuwa msanii ametumia mbinu hii ili kuonesha kwamba elimu inahitajika katika mazingira yoyote. Kutokana na umuhimu wa elimu ndiyo maana wakati wa harakati za mapambano ya kivita wanajeshi wa Frelimo wakishirikiana na wale wa Tanzania walilazimika kujifundisha kusoma na kuandika. Pia, huu ni mtindo ambao unatokana na msanii kuteua misamiati maalumu. Kama asemavyo Mlaga (2017), kwamba msanii huweza kuwapa wahusika wake maneno maalumu ikiwa ni moja ya kusawiri mtindo.

#### 4.4.2.8 Misemo

Misemo ni kifungu cha maneno kinachotumiwa na jamii ya watu wenye lugha kwa namna maalumu ili kutoa mafunzo, maadili na kutahadhirisha jamii. Mfano wa misemo ya Kiswahili ambayo imetumiwa na msanii katika tamthiliya ya *Mondlane na Samora* ni ule unaosema " *Vita havina macho*" (uk- 19). Kupitia msemo huu msanii ameonyesha kuwa vita vina athari kubwa katika jamii. Misemo mengine iliyotumiwa na msanii kama vipengele cha kimtindo ni hii ifuatayo:

i) *Ladha ya tunda ni akisi ya mti wake* (uk. 14)

ii) *Kipendach roho dawa* (uk. 18)

iii) *Mapenzi ni uziwi* (uk. 36)

iv) *Mapenzi ni upofu* (uk. 36)

Kwa muongozo wa nadharia ya Umitindo, mtafiti amebaini kuwa matumizi ya mtindo wa kutumia misemo ni msingi mmoja wapo wakuweka wazi umuhimu wa jamii kuwa na maadili mema na kuzingatia mafunzo na maelekezo mengineyo kwa lengo la kuitahadharisha jamii hiyo dhidi ya maovu mbali mbali ambayo huweza kujitokeza katika jamii husika.

#### 4.4.2.9 Kuchanganya ndimi/lugha

Ni hali ambayo hutokea ambapo mzungumzaji au mwandishi anapotumia lugha mbil au zaidi kuwasilisha maoni yake (Wamitila, 2008). Data zilizokusanywa na mtafiti katika tamthiliya ya *Mondlane na Samora* zimeonesha kuwa mtunzi wa tamthiliya hii amechota misamiati ya lugha za kigeni wakati alipoisanii kazi yake.

Muhusika Daligo ametumia maneno ya Kiengereza na Kiswahili alipokuwa akizungumza na Kaulzar wakati wa kupanga namna ya kupambana na Mondlane. Katika mipango hiyo alionyesha kwamba lazima Mondlane afe kwa sababu yeye ndiye“*assimilado*” wa Frelimo. Mazungumzo ya Daligo yalikuwa kama ifuatavyo:

> DALIGO: *Cabral tulimtumia assassin?, lakini Mondlane we will kill him with explosive. Mondlane ndiye assimilado think-tank wa Frelimo, hivyo lazima afe* (uk. 34)

Katika dondoo hili msanii ameonyesha namna ya wale waliokuwa wakiungamkono mashambulizi ya Wareno walivyokuwa wameathiriwa na Umagharibi, msanii amemtumia Daligo ambaye alikuwa akitumia lugha ya Kiengereza katika kazi yake kama ni kiwakilishi cha ukoloni. Mlaga (2017), ameeleza kuwa mtunzi huwasawiri wahusika wake kwa kuwapa mazungumzo ambayo hulenga kuonyesha mtindo wa

mtunzi. Hivyo basi, matumizi haya ya uchotaji wa manenoya Kiengereza katika kazi hii ni mfano wa utabaka uliojengwa na Wareno katika jamii ya Msumbiji.

Tamthiliya ya *Mondlane ya Mondlane na Samora* imetumia lugha ya Kiswahili ipasavyo lakini matumizi ya mchanganyondimi/lugha kama mtindo wa mwandishi umejitokeza. Mchanganyondimi huo umehusisha lugha ya Kiengereza. Mifano mengineya matumizi ya mchanganyondimi ni:

i) *It is simple* (uk.34)
ii) *Yes! You baby Africa: You still need us to civilize you* (uk.36)
iii) *Love is blind* (uk.36)
iv) *Oh! My God! I die!* (uk. 44)
v) *Ilove you woman* (uk. 45)
vi) *Ok, That's fine* (uk.50)

**Jadweli 02: Vipengele vyengine vya Kimtindo katika Mondlane na Samora**

Chanzo: Data kutoka tamthiliya ya Mondlane na Samora.

**Jadweli 03: Muhtasari wa Vipengele vya jumla vya Mtindo katika tamthiliya ya Mondlane na Samora**

| Nambari | Vipengele vya jumla vya Mtindo katika Mondlane na Samora |
|---|---|
| 01 | Vipengele vya Lugha vilivyotumiwa kuwa Mtindo |
| (i) | Tashibiha |
| (ii) | Sitiari |
| (iii) | Tashihisi |
| (iv) | Taswira |
| (v) | Takiriri |
| (vi) | Tanakalisauti |
| (vii) | Mdokezo |
| (viii) | Tafsida |
| (ix) | Mchanganyondimi/lugha |
| 02 | Mtindo wa Nyimbo |
| 03 | Mtindo wa barua |
| 04 | Mtindo wa hotuba |
| 05 | Mtindo wa mawasiliano ya simu |
| 06 | Mtindo wa matangazo ya redio |
| 07 | Misemo |
| 08 | Mtindo wa rejesta ya jeshini |
| 09 | Mtindo wa rejesta ya shuleni |

Chanzo: Data kutoka tamthiliya ya Mondlane na Samora. Septemba, 2018

Kwa ujumla, mtafiti anaamini kuwa amefanikiwa kwa kiasi kikubwa katika uwasilishaji na uchambuzi wa lengo mahsusi la kwanza na swali la kwanza la utafiti huu wenye mada: *Kuchunguza mtindo na Dhamira katika tamthiliya ya Mondlane na Samora*. Kwa misingi hiyo mtafiti amezingatia lengo mahsusi la kwanza lisemalo: Kubainisha vipengele vya mtindo katika tamthiliya ya *Mondlane na Samora*. Lengo mahususi hilo limekwenda sambamba na swali la kwanza la utafiti lisemalo: Ni

vipengele vipi vya mtindo vilivyobainishwa katika tamthiliya ya *Mondlane naSamora?*Uwasilishaji na uchambuzi wa lengo na swali hilo la utafiti umeongozwa na nadharia ya Umitindo kwa ufanisi zaidi. Kwa kuzingatia mada ya utafiti huu, uwasilishaji na uchambuzi wa lengo mahsusi la pili na swali la pili la utafiti umezingatiwa vyema kama ifuatavyo:

### 4.4.3 Ubainishaji wa Dhamira katika Tamthiliya ya Mondlane na Samora

Mada ya utafiti huu imehusu: *Kuchunguza mtindo na Dhamira katika tamthiliya ya Mondlane na Samora.* Kwa msingi huo, lengo mahsusi la pili la utafiti huu lilikuwa ni: Kubainisha dhamira katika tamthiliya ya *Mondlane na Samora.*Lengo hilo limewiana na swali la pili la utafiti lililosema: Ni dhamira zipi zilizobainishwa katika tamthiliya ya *Mondlane na Samora?*Hivyo basi utafiti huu umefanya uwasilishaji na uchambuzi wa kina wadhamira zilizobainishwa katika tamthiliya hiyo kwa kuongozwa na nadharia ya Mwitiko wa Msomaji kama ifuatavyo:

#### 4.4.3.1 Mauaji

Mauaji ni kitendo cha kuondosha uhai wa kuishi wa kiumbe unaotokana na sababu mbalimbali. Mauaji ni moja kati ya dhamira iliyojadiliwa na Mbogo katika tamthiliya ya *Mondlane na Samora.*Msanii ameonesha namna wakoloni walivyofanya mauaji ya kikatili wakati wa harakati za kugombania uhuru. Mauaji hayo yalifanywa na wakoloni ili kuwajenga hofu Waafrika kurudi nyuma katika harakati za ukombozi wa bara la Afrika. Mondlane ameonesha unyama wa Wareno katika nchi ya Msumbiji alipokuwa jukwaani akiwahutubia watu ili kuonesha unyama huo. Mtafiti amelibaini hili pale msanii aliposema:

*"Hii ni damu ya Msumbiji inayotiririka kama maji ya mto Ruvuma"* (uk. 5).

Pia, athari ya mauaji imejitokeza kupitia tukio la Mondlane aliporipukiwa na bomu. Tukio hili limeonesha kwamba Waafrika ambao walikuwa mstari wa mbele katika harakati za mapambano dhidi ya ukoloni walijikuta wakibakia walemavu ama kupoteza maisha yao kutokana na mashambulizi yaliyopangwa na watawala wa kikoloni. Mwandishi amelieleza tukio hili pale Nyerere aliposema:

NYERERE: [*anaongea, anahutubia*]
*Wana wa Afrika*
*Wana wa Msumbiji*
*Vidonda havijapona bado*
*Damu bado inachuruzika*
*Tunalia machozi*
*Kwa haya mengi majonzi*
*Wanapokufa wanamapinduzi*
*Na kuwaacha wao wapenzi.*
*Lakini mioyo haitakufa ganzi*
*Kwani bado tunayokazi*
*Ya kuvitengua vyote vitanzi*…." (uk. 60-61).

Kupitia dondoo hili mtafiti ameona namna wakoloni walivyoimwaga damu ya mashujaa wa bara hili kama vile Mondlane na hata raia wengine wa tabaka la chini. Hussein (1969), katika tamthiliya ya *Kinjeketile* ameonesha namna Wajerumani walivyosababisha umwagaji wa damu za Watanganyika. Hussein anasema ifuatavyo:

"*Watanzania wanavikumbuka sana vita vya Maji Maji baina ya Watanzania na Wajerumani katika mwanzo wa karne hii. Damu ya Watanzania iliyomwagika katika vita hivyo ilikuwa wino ghali ulioandikia kurasa za historia. Watanzania walikufa kwa maelfu. Walikufa kwa sababu Wajerumani walikuwa na silaha bora na walikufa kwa sababu waliamini silaha za Wajerumani hazitawadhuru. Imani hii ilitiwa nyoyoni mwao na mganga aliyekuwa akiitwa Kinjeketile*"

Kwa kurejelea nadharia ya Mwitiko wa Msomaji, mtafiti amebaini kuwa yale aliyoyaeleza msanii kuhusu mauaji yaliyofanywa na wakoloni ndiyo moja ya athari za tawala za wakoloni katika bara la Afrika. Matukio haya ya mauaji ya kikoloni yamebakia kuwa ni kumbukizi za kihistoria ambapo hata baadhi ya nchi hizi zimeweka siku maalumu kukumbuka matukio haya. Kwa mfano, katika visiwa vya Zanzibar kila ifikapo tarehe 12/01/ ya kila mwaka, huwa na maazimisho ya kuyakumbuka Mapinduzi ya Zanzibar ya tarehe 12/01/1964 ambayo yaligharimu maisha ya watu na umwagaji damu mkubwa wa Wazanzibar.

#### 4.4.3.2 Ukoloni

Ukoloni ni hali ya taifa au nchi moja kuitawala nchi nyengine katika fani / sekta zote zikiwemo za kisiasa, kiuchumi na kijamii. Mtafiti kupitia tamthiliya teule amebaini kuwa msanii ameonesha kwamba wakoloni walipokuja Afrika walijenga utabaka ambapo walitengeneza tabaka la mabwana na tabaka la watumwa. Mathalani, Mohamed (2016) katika tamthiliya ya *Mashetani Wamerudi* alionesha namna wakoloni walivyoitawala Afrika wakati wa ukoloni mkongwe na kuwagawa watu na sasa wamerudi tena wakiwa na mbinu ya utandawazi. Hussein (1971), katika tamthiliya ya *Mashetani* ametumia mchezo kati ya Juma na Kitaru ili kuonesha namna wakoloni walivyojenga utabaka katika bara la Afrika. Mbogo ameusawiri utabaka katika tamthiliya ya *Mondlane na Samora* aliposema:

> "*Miungu ya Ulaya ilipodai sadaka ya damu ya mtu mweusi huku udenda ukiwavuja mbweha wale…*" (uk.6).

Dhamira ya Ukoloni imekwenda sambamba na nadharia ya Mwitiko wa Msomaji. Hii ni kwa sababu dhamira hiyo imeweka wazi tabia ya wakoloni ya ukandamizaji na

unyonyaji ambao ulidhoofisha maisha ya wanajamii. Wakoloni walijifanya Miungu watu na kutaka kutiiwa na Waafrika na pindi Waafrika walipopinga walipata adhabu kali ikiwemo ya kifungo na hata kifo. Hali hii iliendelea hadi pale Waafrika walipochoshwa na madhila ya wakoloni na kuamua kupambana nao hadi walipojikomboa katika bara la Afrika.

#### 4.4.3.3 Ubepari na Ujamaa

Ubepari na Ujamaa ni miongoni mwa mifumo miwili tofauti katika maisha ambayo baadhi ya watawala huweza kuitumia kuendesha jamii zao ikiwa ni pamoja na usimamizi wa njia kuu za uchumi na raslimali nyenginezo. Kwa mfano katika Ubepari njia kuu za uchumi humilikiwa na watu wachache, na mfumo wa ujamaa njia kuu za uchumi humilikiwa na umma.Utafiti huu umegundua kuwa, msanii ameonesha namna tapo linalopinga ujamaa linavyokejeliwa na wale wanaopigia debe mfumo wa kibepari. Kwa mfano, msanii ametueleza hivi:

"*Kasuku wote wa Max wamelala saa hizi…*" (uk. 25).

Mawazo haya yameonesha namna wale waliopigia debe ubepari walivyoonekana kufuata mambo kibubusa bila ya kutoelewa kile walichokifanya. Ndio maana msanii ametumia ishara ya "kasuku." Vilevile,Dhamira ya Ubepari na Ujamaa iliendelea kujadiliwa na msanii kupitia mhusika Nungo ambaye aliisema:

"*Afrika imepatwa na degedege la Stalin na wazimu wa Fidel Castro*" (uk.26).

Mawazo haya yaliibua mgogoro miongoni mwa wanajamii. Nungo katika tamthiliya ya*Mondlane na Samora* alionekana kuwa ni msaliti kutokana na kukataa mfumo wa Ujamaa. Kwa upande wa wale waliounga mkono mfumo wa ujamaa wanasema:

*"Ubepari ni jini litakalofyonza damu za Wanamsumbiji"* (uk.14).

Katika dondoo hili Samora ameufananisha mfumo wa kibepari na jini linalofyonza damu ya Wanamsumbiji. Mawazo haya yamepingana na baadhi ya wahakiki kama vile Sengo na Kiango (2012), ambao wanauona mfumo wa Ujamaa ambao ulishadadia Azimio la Arusha -Tanganyika kama mfumo uliokuwa haukuwafaa Watanzania kwa vile ulianza na dhulma ya kunyang`anya mali za watu. Mawazo haya ya Sengo yamesawiriwa na mtunzi kupitia mhusika Nungo aliposema:

> *"Baadhi ya nchi za Kiafrika zimepagawa na huyu kibwengo wa kikoministi"* (uk.15).

Hivyo suala hili la ubepari na ujamaa limewagawa watu katika maeneo mawili ulimwenguni na kila upande ukiona upande mwengine haufai.Ukweli ni kwamba dhamira hii imejadiliwa sana katika jamii za Afrika wakiwemo waandishi wa kazi za fasihi. Kwa mfano, Kezilahabi(1996) ni mmoja wa waandishi waliolijadili suala hili. Katika tamthiliya ya *Kaptula la Marx* Kezilahabi aliwalaumu viongozi wa Afrika waliofuata mfumo huo bila ya kujitambua. Kezilahabi amemtumia Raisi Kapera akifuata mfumo wa Ujamaa ambao ameuona hauna maana kwa maendeleo ya Afrika.

Kwa kuongozwa na nadharia ya Mwitiko wa Msomaji iliyompa uhuru wa kutoa maoni yake kwa mujibu wa alivyoifahamu matin imtafiti ameona kuwa suala la ubepari na ujamaa lilizua mgogoro mkubwa ndani ya jamii ya Tanzania. Harakati za kupigia debe mfumo wa ujamaa ziliibua migogoro hasa kutokana na kulazimishwa baadhi ya Watanzania kuhama mjini na kuhamia vijijini. Mawazo haya yanaenda sambamba na yale ya Omary (2011), anapoeleza kuwa mfumo wa Ujamaa ambao

ulipigiwa mbiu na Mwalimu Nyerere ulilenga kufanya ukombozi wa Watanzania. Hata hivyo mfumo huu ulishindikana kutokana na baadhi ya watu kwenda kinyume na misingi ya mfumo wa Ujamaa.

#### 4.4.3.4 Usaliti

Mdee na wenzake (2011) wanaeleza kuwa, Usaliti ni utoaji wa habari za siri za nchi au mtu kwa adui wake. Data zilizokusanywa na mtafiti zimeonesha kuwa Emmanuel Mbogo amelijadili suala la usaliti katika jamii za Afrika. Mwandishi huyo ameonesha kuwa usaliti ni tatizo ambalo limeikumba Afrika kwa miongo kadhaa. Wakati wa harakati za kupigania uhuru wapo Waafrika ambao waliwasaliti Waafrika wenziwao kwa wakoloni. Kwa mfano, mhusika Samora anasema:

> *"Lakini nasema: iache mifupa ya Wanamsubiji iwe shahidi…." (*uk.11).

Katika dondoo hili msanii ameonesha namna Waafrika walivyosalitiana wakati wa harakati za mapambano dhidi ya ukoloni. Mhusika Samora alimlaumu Nungo kutokana na usaliti alioufanya dhidi ya wanajeshi wa Frelimo.

Kwa upande mwengine, Mondlane ameona dalili za usaliti miongoni mwa Waaafrika. Kutokana na kulibaini hili aliamua kumuandikia barua Janet ili kumueleza suala zima la usaliti ambalo limemzunguka. Barua hiyo ilisema ifuatavyo:

> *"Mpenzi Janet, nahisi kuna kenge*
> *wenye meno ya chuma wanaotamani*
> *kuirarua roho yangu. Nikifa yaache*
> *machozi yatiririke, lakini usikate*
> *tamaa. Tunza watoto wetu:*
> *Eduardo, Jennifer na Nyeleti.*(uk. 29)

Msanii ameonesha kuwa usaliti sijambo lililoanza leo katika jamii za Afrika. Tangu wakati wa mapambano ya kupigania uhuru dhidi ya wakoloni Waafrika kama vile mhusika Nungo na Kavandame walivyo wasaliti Waafrika kutokana na kuweka maslahi yao binafsi mbele badala ya maslahi ya ujenzi wa taifa. Makame (2017), ameeleza kuwa usaliti ni moja kati ya masuala yaliyoibuka katika harakati za mapambano ya kupigania uhuru. Kutokana na tatizo la usaliti uliofanywa na baadhi ya Waafrika ilikuwa ni vigumu kupambana na wakoloni.

Nadharia ya Mwitiko wa Msomaji inayompa fursa msomaji kutoa maoni yake kwa alivyofahamu, mtafiti amekuja na maoni yasemayo kuwa suala la usaliti lilikuwapo kabla ya uhuru na hata baada ya uhuru usaliti umekuwa ukijitokeza katika ngazi mbalimbali za kijamii. Baadhi ya wanandoa husalitiana kwawenza wao kufanya mapenzi ya nje ya ndoa. Hivyo hivyo viongozi wengi walioshika hatamu ya uongozi waliwasaliti Waafrika ambao walikubali kumwaga damu yao ili kukomboa bara hili kwa nia ya kuondoa kabisa unyonywaji na ukandamizwaji. Matarajio haya bado hadi leo hayajafikiwa kutokana na suala la usaliti. Kama wasemavyo Sengo na Kiango (1975), kwamba kabla ya uhuru wa bendera viongozi wengi wa bara la Afrika walitazamia kupata nafasi za uongozi. Hivyo baada ya uhuru waliiga matendo ya kikoloni na kubakia kuwa vibaraka wa kikoloni. Mwafrika akabakia hana lake anaendeshwa kama mashine. Mawazo haya yanayoelezwa na Sengo na Kiango (ktj) ndiyo yanayoshuhudia hadi leo katika jamii za Afrika.

#### 4.4.3.5 Vita

Vita ni aina ya mapigano, mapambano, makabiliano au ukinzani unaohusisha pande mbili za wahusika ambao huweza kutofautiana kwa sababu mbalimbali baina yao.

Katika utafiti huu, Dhamira ya Vita imesimuliwa na msanii/mwandishi hasa katika miktadha ya harakati za ukombozi wa bara la Afrika wakati wa kudai uhuru. Katika kueleza miktadha hiyo msanii ameonesha kuwa mapambano ya kivita yalisababisha Waafrika kupoteza maisha. Kwa mfano, huko Msumbiji Wareno walipambana na jeshi la Frelimo kwa muda wa miaka kumi. Mapambano hayo yaligharimu maisha ya watu wa kila daraja. Viongozi wa harakati hizo kutoka bara la Afrika nao pia walipoteza maisha na wengine kubakia walemavu. Imeelezwa kuwa Mondlane alipoteza maisha kutokana na kuripukiwa na bomu lililokuwa katika paseli kutoka kwa Wareno. Msanii amelieleza hili kwa kusema:

"*Kaburi la Kireno limeumeza uhai wa Baba wa Taifa la Msumbiji*" (uk. 60).

Mbogo (2016), katika tamthiliya ya *Mondlane na Samora* amesema kuwa Mondlane aliuawa kwa bomu ambalo lilifungwa ndani ya paseli na alipoifungua paseli hiyo bomu hilo lilimripukia.Vilevile imeelezwa namna ya mikakati madhubuti ilivyohitajika wakati wa vita dhidi ya wakoloni. Kadri ya athari hasi zilivyojitokeza wakati wa mapambano dhidi ya Wareno kulihitajika Waafrika wapange mikakati madhubuti ili kufikia lengo la ukombozi wa bara hili la Afrika. Vyenginevyo ingekuwa vigumu kufikia lengo la ukombozi. Msanii kupitia mazungumzo kati ya Mondlane na Samora mbele ya wapambanaji wa Frelimo ametueleza ifuatavyo:

MONDLANE: *Yuko wapi Kanali Mahfoudh?*
SAMORA*: Kanali Mahfoudh amechukua*
*batalioni moja, ameelekea*
*Bwawa la Kabora Bassa.*
MONDLANE*: Tunahitaji kupanga mikakati mipya.*
*Wengine toweni maiti. tayarisheni*
*makaburi. tutawazika mashujaa wetu*
*baada ya mkutano huu mfupi.*

ASKARI: *Sawa Afande* (uk 8-9)

Katika nukuu ya hapo juu msanii ameonesha namna vita dhidi ya wakoloni ilivyoondoa maisha ya watu ambao walikuwa msitari wa mbele katika ukombozi wa bara la Afrika. Mondlane ni mfano wa mashujaa hao ambayealipoteza maisha kutokana na vita dhidi ya Wareno. Hii ni kusema kuwa vita havichagui. Kwa hakika athari za vita wakati wa kupigania uhuru wa Afrika kutoka kwa wakoloni zilikuwa ni kubwa na zisizomithilika. Kila tabaka liliathirika. Kwa sababu ya vita kutochagua hata viongozi huweza kuondoka mwanzo kuliko tabaka la chini.

Pamoja na kuwepo kwa athari kubwa ya vita, mtafiti amegundua kuwa msanii ameonesha harakati za mapambano ya kivita wakati wa kupigania uhuru kutoka kwa wakoloni hazikuzuia shughuli nyengine muhimu za kijamii kuendelea. Shughuli kama vile ndoa zilifanyika na huku mapambano yakiendelea. Kwa mfano katika tamthiliya ya *Mondlane na Samora* (uk 39 - 40) imeelezwa namna Josina na Samora walivyofunga ndoa wakiwa msituni wakati wa harakati za mapambano dhidi ya ukoloni wa Wareno.Mwandishi ametueleza ifuatavyo:

WATU: *Vivaa!*
[*Wote wawili wanacheza. Na*
*…wote wanacheza kwa nguvu…Wanatoka.*
*Josina katangulia Samora*
*nyuma…Wanaelekea msituni…Wamepotea.*
[ *Kelele, ngoma na shangwe zinazidi* ]
[ *wakati wakiendelea kucheza, kula na*
*kunywa, ghafla…*]
WARENO*:* [ *Kuna mashambulizi ya ghafla ya ardhni*

*Na ya ndege za kivita angani*]

MONDLANE*:* [ *kwa sauti kali] Wote lala chini! Askari songa mbele! Wakabili maadui!* (uk 39 - 40)

Kwa mnasaba wa nadharia ya Mwitiko wa Msomaji ambayo ni moja kati ya nadharia inayoongoza utafiti huu na inayompa fursa msomaji / mhakiki kutumia uzoefu na taaluma yake kuhakiki kazi ya fasihi inavyostahiki kulingana na taaluma aliyonayo, kama alivyoweka wazi Njogu na Wafula (2007) kwamba nadharia hii imelenga kujalizishia kazi ya fasihi kutegemea uzoefu wa msomaji.Hivyo basi, kutokana na hali hiyo, mtafiti ameshawishika kusema kuwa dhamira ya vita huathiri maisha ya watu wengi. Hali hii pia imethibitishwa na Mbogo (2015), katika tamthiliya ya *Sadaka ya John Okello* ambapo vita vya mapinduzi ya Zanzibar vilisababisha mauaji ya Wazanzibar wengi.

**4.4.3.6 Umuhimu wa Elimu**

Njogu na Chimerah (1999), wanasema kuwa elimu ni kitu muhimu sana na haifai kutumiwa kama nyenzo ya utabaka na ukabila. Kutokana na umuhimu wa elimu ndio maana Josina aliamua kuwasomesha wanajeshi ili wajuwe kusoma na kuandika. Msanii amewataka Waafrika wajuwe kwamba elimu ndio ngao kuu ya ukombozi. Waafrika waliokataa kusoma walifanya sivyo. Elimu inapotumika kama chombo cha ukombozi huwa ni dawa na kinyume chake huwa ni sumu. Hivyo Josina amewafundisha wapambanaji ili kupata elimu ya kuweza kujikomboa. Darasa la Josina lilikuwa hivi:

JOSINA: [Anaonesha na fimbo] Sema:
*a….e…i…o…u. Safi! Sasa mmoja mmoja.*

*Wewe soma!*
*Vizuri: Sema:*
*ba…be…bi…bo…bu. Safi:*
*Sema: baba…babu…*
*Sema: mama…mama…*
*Sasa tungo kamili: baba na mama… baba na mama*
JOSINA: *Nataka kuwakumbusha tena kuwa:kusoma*
*ni muhimu. Kamanda Mondlane, kabla hajatutoka,*
*kila mara alisisitiza kuwa: uhuru wa Msumbiji*
*lazima uende sambamba na vita dhidi ya*
*maadui watatu: ujinga, maradhi na umasikini.*(uk – 67)

Kwa muongozo wa nadharia ya Mwitiko wa Msomaji,mtafiti ameona kwamba suala la elimu lina umuhimu mkubwa katika maisha ya kila siku. Ukombozi wa kisiasa, kiutamaduni, kiuchumi na kifikra, elimu ndio huongoza katika kufanikisha ukombozi huo. Kamwe hatuwezi kukamilisha maswala ya ukombozi iwapo watu watakuwa si watambuzi wa mambo, matukio ya kijamii na ulimwengu kwa jumla. Ndio maana baadhi ya watu husema kwamba "elimu ni nuru au elimu ni ufunguo wa maisha". Kukosekana kwa elimu huwa ni maangamizi makubwa.

**4.4.3.7 Umoja wa Bara la Afrika**

Umoja wa Bara la Afrika ni umoja ambao umelenga kuwaunganisha Waafrika wote kuwa na nia/lengo moja la kusukuma mbele maendeleo ya bara hilo katika sekta zote zikiwemo za kisiasa, kiuchumi na kijamii na kuondokana na kila aina ya maovu kwa Waafrika na jamii nyenginezo nje ya Afrika.

Mtafiti kupitia tamthiliya ya *Mondlane na Samora* amebaini kuwa msanii ameonesha kwamba, suala la umoja na mshikamano kwa bara la Afrika lilikuwa ni ngao katika kupatikana ukombozi wa bara hilo. Mtazamo huu ndio ulioshikiliwa na mashujaa wa Afrika katika kupigania uhuru. Kama wanavyosema Njogu na Chimerah (1999),

kwamba mtu hafanikiwi kwa kutegemea tabaka lake au jamii yake. Kwa kulitambua hili ndio maana kunatiliwa mkazo umuhimu wa umoja na mshikamano katika kufanya ukombozi.

Mwandishi amemtumia muhusika Nyerere wakati akiwa jukwaani akihutubia katika mkutano wa viongozi wa Umoja wa Bara la Afrika huko Addis Ababa. Utafiti huu umegundua kuwa msanii ametumia mbinu ya takriri ili kuibua dhamira ya umuhimu wa Umoja wa Afrika. Kwa mfano, mwishoni mwa hotuba ya Nyerere kuna urudiaji unaojitokeza hivi:

> NYERERE:*Na mintarafu ndugu yangu rais Sekou Toure; Tanganyika tuko tayari kutenga asilimia wahedi ya bajeti ya nchi yetu kwa ajili ya ukombozi wa nchi za kusini mwa Afrika!*
> VIONGOZI: *Viva!*
> NYERERE: *Ndiyo! Na mintarafu ndugu yangu Waziri Mkuu wa Algeria,*
> *Mheshimiwa Ahmed BenBella"tuko tayari kufa kidogo" Ilikung`oa udhalimu wa ukoloni barani Afrika. Asanteni kwa kunisikiliza. Aluta Continua!*
> VIONGOZI: *Aluta Continua!*
> NYERERE: *Viva Afrika!*
> VIONGOZI: *Viva!*

Katika dondoo hili mtafiti aligundua namna msanii alivyomtumia Nyerere akisisitiza juu ya umuhimu wa kuungana kwa nchi za bara la Afrika. Ili kufanikisha muungano huo lazima nchi hizi zikubali kusaidiana kwa hali na mali ikiwa ni pamoja na kujitoa mhanga ili kuhakikisha kwamba bara zima limejikomboa. Katika enzi hizi za Afrika huru ipo haja ya bajeti za nchi kufinywa ili kuhakikisha nchi nyengine za bara la Afrika zimeinuliwa kiuchumi badala ya kutegemea nchi za Kigeni ambazo husababisha kuenea kwa ukoloni.

Pia, msanii amemtumia mhusika Nyerere akitoa mapendekezo yake ya jinsi ya kufanikisha ukombozi wa bara hili. Msanii ameona kwamba ni kwa mbinu ya kuungana pamoja ukombozi wa Afrika unaewza kufikiwa.Mawazo hayo yamejadili ndoto ya mwalimu Nyerere ya kuzitaka nchi za bara la Afrika kuungana ili kuunda nchi moja iliyoimara. Mhusika Nyerere katika tamthiliya ya *Mondlane na Samora* amesema:

"*Lazima Waafrika tuungane! Tuwe nchi moja, tuwe na jeshi moja*..." (uk.7).

Kwa kurejelea nadharia ya Mwitiko wa Msomaji, mtafiti ameona namna mawazo ya kuwepo kwa Umoja wa Afrika yalivyochukuliwa na nchi huru za Afrika na kuunda umoja huo. Kwa bahati mbaya sana yale malengo ya Mwalimu Nyerere, Raisi wa kwanza wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania ya kutaka Afrika iwe nchi moja hadi sasa bado hayajafikiwa na tamaa ya kufikia lengo hilo imekuwa ikififia siku hadi siku. Kukosekana kwa umoja ulioimara katika mataifa ya Afrika kumepelekea nchi hizi kuangukia katika makucha ya ukoloni mamboleo.

#### 4.4.3.8 Mapenzi na Ndoa

Sengo (1985), anasema kwamba ndoa ni asasi muhimu sana katika maisha ya kila siku. Kwa sababu ya umuhimu wa ndoa kila mmoja huwa na kiu ya kutaka kufunga ndoa. Katika maisha ya Uswahilini, mtu hujihisi amekamilika pale anapofanikisha kufanya mapenzi kupitia ndoa. Katika tamthiliya ya *Mondlane na Samora* msanii ameonesha namna taasisi ya ndoa na mapenzi ilivyochukuwa nafasi muhimu katika maisha ya kila siku bila ya kuathiriwa na matukio ya kijamii kama vile vita. Hili

linasawiriwa kupitia Josina na Samora kuhusu suala la mapenzi na ndoa pale aliposema:

> “*Mimi nakuchagua wewe. Nakutaka wewe. Nakupenda wewe…*” (uk.18).

Msanii ametuonesha namna Josina alivyokuwa na mapenzi ya dhati kwa Samora. Kutokana na mapenzi hayo ya dhati ndio maana Josina ameamua kufunga ndoa akiwa msituni ili kukamilisha kiu ya mapenzi. Mapenzi ya kweli hayajifichi wala hayafichiki. Ndio maana watu husema kwamba “mapenzi ukuni wa mkoko usipowaka wafuka.” Mapenzi ya Josina na Samora yalikuwa kiwango cha kuwaka na kila aliyekaribu kuyaona. Hali hio imebainika pale Josina aliposema:

> *“Hata mimi nakupenda [kimya]*
> *Samora…nina hamu…natamani uipande hima mbegu ya pendo lako hapa. Ukamuumbe kiumbe ndani ya tumbo hili la kike ili nikuzalie pacha* [*Samora anacheka*] *Usicheke. Nitakuzalia pacha mvulana na msichana. Kisha tutawaondoa pacha wetu huku vitani”*

Katika nukuu hii mtafiti ameona namna suala la mapenzi linavyoendana na fikra za kupata kizazi. Msanii ameonesha kuwa moja kati ya lengo la ndoa miongoni mwa wanajamii ni kupata watoto ambao hupendelewa wawe wa jinsia ya kike na jinsia ya kiume. Katika jamii ya Afrika mwanamke aliye katika ndoa ambaye ama hajabahatika kujifungua mtoto au amekuwa akijifungua watoto wa kike watupu bila ya kupata watoto wa kiume hujikuta mapenzi katika ndoa yake yakipungua au ndoa hiyo kuwa hatarini kuvunjika kabisa.

Vile vile, msanii amejadili suala la mapenzi kwa kusema “*Kipendacho roho dawa”* (uk.18). Kupitia msemo huu msanii ameonesha kwamba mapenzi huleta kitulizano miongoni mwa wapendanao. Kukosekana kwa mapenzi kunaweza kusababisha

msongo wa mawazo na mtu kukosa kitulizano. Matokeo yake ni kuharibu uhusiano miongoni mwa wapendanao wakiwemo wanandoa. Florence, Buliba na Kamau (2016), waliandika makala yenye anuani "*Vichocheo vya migogoro katika ndoa*." Katika makala hiyo walisema kwamba migogoro katika masuala ya mapenzi haiepukiki hata hivyo ipo haja watu kujiepusha na mambo yanayosababisha migogoro hiyo ili kuendeleza mapenzi yao. Kutokana na kulitambua hilo Samora alikuwa mara kwa mara akimtuliza Josina ili kulinda uhusiano wao. Mbogo (2016) katika tamthiliya ya *Mondlane na Samora* amelilinganisha suala la mapenzi na upofu pale aliposema "*Mapenzi ni upofu*" (uk. 36). Msemo huu umewiyana na msemo maarufu unaosema "mwenye mapenzi haoni ingawa macho anayo." Kwa nini haoni? Jibu ni kwamba ana kiu ya kitu anachotaka kuiondoa.

Kwa kufuata na nadharia ya Mwitiko wa Msomaji,mtafiti ameonakwamba dhamira ya mapenzi na ndoa ndiyoiliyojadiliwa katika jamii na ndicho kitu kinachoshuhudiwa katika jamii zetu. Mapenzi yamekuwa ni sehemu muhimu sana katika maisha ya binadamu. Tatizo moja ambalo limeshuhudiwa ni lile la wanawake kujiona kuwa lazima watimize malengo ya wanaume ili kutunza ndoa zao. Utashi huu mara nyengine hupelekea wanawake kufanya maamuzi ambayo yanakiuka haki zao. Katika kulieleza suala la wanawake kujikuta matatani katika ndoa zao Florence, Buliba na Kamau (ktj), wanamnukuu Greer (1970), ambapo wanasema kwamba wanawake wametenganishwa na ashki yao ya kimapenzi na jamii imeifanya ndoa ni himaya ya wanaume na kazi ya wanawake ni kuwaridhisha wanaume huku wakiachwa wakiumia kihisia. Hali hii ndiyo inayosababisha migogoro katika ndoa. Katika baadhi ya jamii za Afrika wanawake ambao kwa bahati mbaya huwa

hawajabahatika kupata mtoto huzungumzwa vibaya na kusalitiwa na hata na ndugu na jamaa wa mume.

#### 4.4.3.9 Ujasiri na Ushujaa

Ujasiri na ushujaa ni miongoni mwa matendo mema ambayo kila mpenda maendeleo anastahiki kuwa na tabia hizo. Ujasiri na Ushujaa hupelekea kujenga kumbukumbu ya muda mrefu hasa katika kujitolea kwa ajili ya taifa. Tabia hizi hulenga kutenda au kufanya jambo zuri pasi na kutetereka au kuogopa. Ni kitendo cha kujitoa muhanga bila ya woga. Dhamira hizi zimeibuliwa na mtafiti kupitia mtunzi katika tamthiliya ya *Mondlane na Samora* ni dhamira ambazo zinastahiki kuigwa na kila mpenda maendeleo. Msanii ametuonesha namna Ujasiri na Ushujaa ulivyokuwa muhimu sana katika harakati za ukombozi. Kutokana na ujasiri na ushujaa waliokuwanao Waafrika mapambano ya kivita dhidi ya wakoloni yalianzishwa. Pamoja na Wareno kuwa na silaha za kisasa zaidi ukilinganisha na zile za Waafrika.

Mondlane ni mmoja wa wahusika jasiri na mwenye ushujaa mkubwa katika harakati za ukombozi. Sifa hii imejitokeza pale wanajeshi wa Afrika walipojeruhiwa vibaya na majeshi ya Wareno hata hivyo baada ya kukagua majeruhi na wale waliokufa Mondlane alipeleka agizo la kuletwa askari zaidi ili kuendeleza mapambano. Pia, ni katika miktadha hii ambayo Mondalane aliwasiliana na Samora ili alete masanduku ya dawa zaidi. Msanii amelieleza tukio hili hivi:

> MONDLANE:*[baada* ya *kukagua majeruhi na waliokufa anaongea na Ova-ova] Samora..! Samora…Unanisikia? Ova*…*Mondlane*…*Lete askari wengine upande huu. Ova* …*Ova…tunahitaji haraka sanduku la dawa. Ova*. [*anazima ova*] (uk.5)

Kwa kupitia dondoo hili msanii ameonesha namna suala la ujasiri na ushujaa lilivyokuwa muhimu wakati wa mchakato wa kupigania uhuru. Kutokana na ujasiri huo Mondlane alitambua kuwa baadhi ya wanajeshi wa Frelimo wakishirikiana na wale wa Tanzania walipoteza maisha na wengine kujeruhiwa lakini bado aliona ipo haja ya kuendelea na mapambano na si kurudi nyuma. Mondlane alielewa kwamba kurudi nyuma ni kushindwa. Wahusika wengine ambao wametumiwa kama mfano wa watu wenye ujasiri na ushujaa wakati wa vita dhidi ya ukoloni ni Samora na Josina. Ushujaa na ujasiri wa wahusika hawa umejitokeza pale Samora alipozungumza na Josina wakiwa huko msituni ambapo Samora alisema:

*"…nitawamiminia risasi: Titititi! Traaa! Traaa! Traaa! Bumuu!"* (uk.24).

Katika tamthiliya hii mtafiti kupitia msanii ameonesha namna Samora na wanajeshi wengine wa Frelimo walivyoshirikiana bega kwa bega na wanajeshi wa Tanzania kuoneshaujasiri na ushujaa dhidi ya Wareno. Kutokana na ushujaa huo ndio maana Samora aliapa kwamba atapambana na jeshi la Wareno kwa kuwamiminia risasi. Huundio ujasiri na ushujaa unaotakiwa mtu kuwa nao. Ujasiri wa kufanikisha taifa bila kukiuka misingi ya utu.

Nadharia ya Mwitiko wa Msomaji, imempa ujasiri mtafiti kusema kuwa suala la ujasiri na ushujaa lililojadiliwa na Mbogo (2016) katika tamthiliya ya *Mondlanena Samora* limeshabihiana na historia ya jamii za Waafrika. Kupitia nadharia hiyo mtafiti anafikia suluhisho la kusema kwamba"Ukweli ni kwamba Wakoloni walikuwa hawako tayari kuachia madaraka ya uongozi katika bara la Afrika lakini kutokana na ujasiri na ushujaa wa Waafrika kuamua kupinga ukoloni ndani ya bara

hili ndiko kulikowafanya wakoloni kufunga virago na kuachia madaraka hayo. Maamuzi haya ya wakoloni hayakuja tu kwa maneno matupu bali Waafrika waliamua kukamata mtutu wa bunduki ili kupambana na wakoloni bila kujali majeruhi na vifo ambavyo vilikuwa vinaendelea kutokea kila pembe ya bara la Afrika ambavyo vilisababishwa na wakoloni waliokuwa hawako tayari kuliacha bara la Afrika.

#### 4.4.3.1 Mawasiliano

Mawasiliano ni mfumo maalum unaotumiwa na watu kwa lengo la kupeana au kufikisha taarifa/ ujumbe kwa walengwa. Mawasiliano ni njia ambayo hutumika kurahisisha taarifa husika kuweza kutekelezwa inavyostahiki na kwa muda uliokusudiwa. Kawaida mawasiliano huhusisha mtoaji wa taarifa, taarifa husika pamoja na mpokeaji wa taarifa. Katika utafiti huu mtafiti amegundua kuwa msanii ameonesha kuwa vifaa vya mawasiliano vilikuwa muhimu wakati wa harakati za mapambano. Vifaa hivyo vilisaidia wapambanaji kuwasiliana na kupanga mipango ya mashambulizi kwa siri kubwa. Bila vifaa hivi ingekuwa vigumu kwa Waafrika kuwasiliana ili kuwazingira wakoloni. Kutokana na mawasiliano yalivyokuwa mazuri, harakati za kupashana habari kuhususiri ya mapambano zilikuwa rahisi. Kwa mfano, wakati wa vita mawasiliano yaliyotumika yalikuwa ni simu ya upepo (radio call) na yalikuwa kama hivi:

*“Nani?* **...** *Namba ya siri?* **...** *Sawa* **…** *Karibieni”* (uk. 8)

Mtafiti ameona kuwa ili mashambulizi ya Waafrika (Frelimo) dhidi ya wakoloni wa Kireno yaweze kufanikiwa, mawasiliano yalikuwa hayaepukiki. Kwa mantiki hii

palihitajika vifaa vya mawasiliano ambavyo vilikuwa haviwezi kuingiliwa na maadui. Ili kufanikisha suala la mawasiliano Waafrika walitumia nambari za siri katika mfumo wa mawasiliano.

Kwa kurejelea nadharia ya Mwitiko wa Msomaji, mtafiti amekuja na fikra inayoashiria umuhimu wa mawasiliano katika harakati za ukombozi. Mawasiliano yamekuwa yakihitajika katika taasisi yoyote ili kufikia malengo ya taasisi husika. Pia, ni lazima mawasiliano hayo yafanyike katika mfumo uliosalama. Mawasiliano nyeti ya taasisihatakiwi yaingiliwe na watu wengine ambao hawahusiki na kuchukua taarifa hizo. Kutokana na umuhimu huu ndio maana kila taaasisi hujipanga kuhifadhi na kulinda mawasiliano yake ili yasiingiliwe na kuhujumiwa.

#### 4.4.3.11 Uhuru

BAKIZA (2010) wanaeleza kuwa, Uhuru ni hali ya nchi kuwa na maamuzi yake bila ya kuingiliwa na nchi nyengine. AU, uhuru ni hali ya mtu kutoingiliwa mambo yake na mtu mwengine. Katika tamthiliya ya *Mondlane na Samora,* mtafiti amebaini kuwa dhamira ya uhuru imejitokeza kupitia juhudi kubwa zilizofanywa na wanamsumbiji dhidi ya wakoloni wa Kireno. Uhuru huo ulipatikana kutokana na vita vya msituni kati ya jeshi la Wareno na wapambanaji wa Frelimo ambao waliungana na Waafrika wengine toka Tanzania ili kufanikisha kupatikana kwa uhuru wanchi ya Msumbiji. Msanii ameonesha kuwa wapambanaji hao walikuwa na umoja katika mapambano na hawakurudi nyuma. Kama ambavyo msanii anaoeleza

SAMORA: Viva, viva, viva viva Frelimo
Viva, viva, viva viva Frelimo
Viva, viva, viva viva Frelimo

Viva, viva Frelimo!

UMATI: Viva, viva, viva viva Frelimo
Viva, viva, viva viva Frelimo
Viva, viva, viva viva Frelimo
Viva, viva Frelimo! (uk. 105-106)

Kupitia dondoo la hapo juu msanii ameonesha kuwa umoja na mshikamano ndio nyenzo muhimu katika kufanikisha kupatikana kwa uhuru. Waafrika walifanikiwa kupata uhuru wa bara lao kutoka kwa Wakoloni kwa sababu waliungana pamoja. Hatimae umoja na mshikamano ndio ulitoa cheche zilizoanzisha vita vilivyopiganwa dhidi ya utawala wa Wareno.

Pia, msanii ameonesha umuhimu wa kuungana pamoja nchi za bara la Afrika ili kufanikisha kupatikana kwa uhuru katika kila pembe. Msanii amemtumia mhusika Nyerere akiwa Addis Ababa kwenye mkutano wa Umoja wa Nchi Huru za Afrika akihamasisha umuhimu wa umoja na kusaidiana ili kupata uhuru. Hotuba ya Nyerere ilikuwa inasema:

NYERERE: "*Naomba nianze kwa kuwasalimu kwa mtindo wa ndugu zetu wa Frelimo:*
*Viva Frelimo!*
VIONGOZI*: Viva!*
NYERERE: *Aluta Continua!*
VIONGOZI*: Aluta Continua!*
NYERERE*: Mwenyekiti, mwenyeji wetu: Mstahiki Mfalme Haile Salassie.*
*Viongozi wa Nchi huru za Afrika ikiwa ni pamoja na Rais Kwame Nkrumah,Gamal Abdel Nasser, Ahmed Sekou Toure,*
*Ahmed Ben Bella…Itifaki inazingatiwa. Ndugu zangu.*
*Nataka nianze kwa kusema kuwa: hatukuja Adiss Ababa ili*
*kujadili iwapo tunataka Afrika iwe huru au la. Hata maadui*

> *wakubwa wanajua kuwa: lazima tujikomboe toka minyororo ya ukoloni…Hivyo tumekutana hapa Adiss Ababa ili kutafuta mkakati wa pamoja wa kuleta umoja huo…*" (uk 1- 4).

Katika nukuu ya hapo juu imeoneshwa namna Nyererealivyokuwa akitilia mkazo umuhimu waumoja na mshikamano katika kuleta ukombozi wa bara la Afrika. Kwa kutumia hotuba iliyotolewa na mhusika Nyerere, msanii amelenga kutueleza kuwa umoja ni nguvu na utengano ni udhaifu. Katika hotuba hiyo Nyerere ameeleza kwamba kila mmoja kati yetu anahitaji kupambana na wakoloni kwa sababu ya kutaka kuwa huru. Hata hivyo mbinu muhimu ya kuondokana na ukoloni katika bara la Afrika ni kuwa na umoja ili kuhakikisha kila nchi ya Afrika imejikomboa kutoka katika utumwa wa wakoloni. Kutokana na umoja wa Waafrika kuwasaidia Frelimo katika mapambano dhidi ya wanajeshi wa Ureno mwisho nchi hiyo ilipata uhuru wake na Wareno waliondoka. Tukio hili limeelezwa kupitia tangazo la redio ya BBC kupitia ripota wake BBC1 na BBC2. Matangazo haya yalikuwa yanasikika hivi:

> BBC1*: Hii ni BBC London…Karibuni wasikilizaji na wapenzi wa BBC London. Habari zinazogonga vichwa vya habari. Samora Moses Machel ahutubia mkutano mkubwa hukoBeira….Habari kamili.Baada ya makubaliano ya Lusaka, Samora Moses Machel, Rais wa Frelimo atahutubia mkutano mkubwa kwa mara ya kwanza mjini Beira jioni hii.*
> BBC2: *Anaripotimoja kwa moja toka mjini Beira. BBC2 unanisikiliza?*
> BBC2 :*Nakupata vizuri BBC1.*
> BBC1: *Hali ikoje hapo mjini?*
> BBC2: *Ni mjini Beira. Mji ulioko kusini kabisa mwa Msumbiji. Ni katika uwanja Mkubwa wasoka wa Beira. Watu kwa maelfu wanamiminika kuja kumsikiliza Samora Moses Machel* (uk 94 -106)

Katika matangazo haya msanii amedhamiria kuonesha namna Waafrika walivyokuwa na shauku kubwa ya kupatikana kwa uhuru. Watu walifurahia uhuru kutoka mikononi mwa Wareno huku wakiamini kuwa sasa mambo yatakuwa mazuri. Kupitia dondoo hili, mtunzi amewakumbusha viongozi walioshika hatamu baada ya bara la Afrika kupata uhuru wa bendera watambue kuwa watu walipigana na kumwaga damu kwa matarajio ya kupata maendeleo.

Hata hivyo malengo ya Waafrika ya maendeleo hadi sasa yameonekana hayajafikiwa vyakutosha. Kwa mfano Njogu na Chimerah (1999), na Jilala (2016) wanaeleza kwamba pamoja na bara la Afrika kupata uhuru wa bendera, bado wakoloni wamekuwa wakilinyonya bara hili kwa mbinu mpya. Massoud (2017), akiungana na mawazo haya anasema kwamba tamthiliya ya *Mashetani Wamerudi* ni ishara ya ukoloni mamboleo ambao umekuwa ukitumia mbinu mpya ya utandawazi hasa katika sera ya ubinafsishaji ambapo kwa sera hii mataifa tajiri yamendelea kunyonya nchi maskini. Anaendelea kueleza kuwa taswira ya chozi inaashiria mataifa madogo ambayo ni maskini na taswira ya tembo ni mataifa tajiri ulimwenguni. Hivyo Afrika hadi sasa haiwezi kushindana na mataifa tajiri.

Kwa mnasaba wa nadharia ya Mwitiko wa Msomaji ambayo imeongoza katika uchambuzi wa dhamira,mtafiti ameona kuwa mawazo haya ya harakati za uhuru ndiyo yaliyowahi kujitokeza katika maeneo ya bara la Afrika. Waafrika waliungana ili kuhakikisha bara lote limekombolewa toka mikononi mwa wakoloni. Wakati huu walikuwa Waafrika wamechoshwa na madhila, monevu na udhalilifu wa wale ambao walikuja kutoka nchi zao wakakaribishwa wakidhaniwa kwamba ni wema kumbe ni kinyume na dhana ya Waafrika. Kutokana na mawazo haya Sengo na Kiango (1975),

wanasema kwamba mkoloni alipokuja Afrika alikaribishwa kiungwana kwa vile alivyodhaniwa kuwa ni binadamu. Alikaribishwa na akakirimiwa vilivyo. Udhaifu wa binadamu ni kutoridhika na kile apewacho badala ya kushukuru kwamba bado anaendelea kuishi wakati wengine hawakotena duniani ingawa wanapenda waweko. Mkoloni hakuliona hili na akaendeleza ukandamizaji na unyonyaji na hatimae Waafrika wakaanzisha wimbi la mapambano ya kdai uhuru kila pembe ya Afrika.

Kwa ujumla, mtafiti amegundua kuwa tamthiliya ya *Mondlane na Samora* ni tamthiliya iliyoakisi uhalisia wa maisha ya Waafrika wengi katika harakati za kudai uhuru. Bara la Afrika limekuwa katika mfumo wa ukoloni kwa muda mrefu, hali hii ilipelekea Waafrika wachoshwe na tabia mbaya za wakoloni na hatimae kuwa tayari katika kupigania uhuru huo kama ambavyo Msumbiji walivyoshirikiana na mataifa mengine (ikiwemo Tanzania) kupigania uhuru huo. Kupitia tamthiliya hii mtafiti amebainisha dhamira mbalimbali kuzifanyia uchambuzi vyema. Dhamira hizo ni pamoja na: Dhamira ya mauaji, dhamira ya ukoloni, dhamira ya ubepari na ujamaa, dhamira ya usaliti, dhamira ya vita, dhamira ya umuhimu wa elimu, dhamira ya Umoja wa Bara la Afrika, dhamira ya mapenzi na ndoa, dhamira ya uhuru, dhamira ya ujasiri na ushujaa na dhamira ya mawasiliano.

**Jadweli 04: Muhtasari wa Dhamira katika tamthiliya ya Mondlane na Samora**

| Nambari | **Dhamira katika tamthiliya ya Mondlane na Samora** |
|---|---|
| 01 | Dhamira ya Mauaji |
| 02 | Dhamira ya Ukoloni |
| 03 | Dhamira ya Ubepari na Ujamaa |
| 04 | Dhamira ya Usaliti |
| 05 | Dhamira ya Vita |
| 06 | Dhamira ya Umuhimu wa Elimu |
| 07 | Dhamira ya Umoja wa Bara la Afrika |
| 08 | Dhamira ya Mapenzi na Ndoa |
| 09 | Dhamra ya Ujasiri na Ushujaa |
| 10 | Dhamira ya Mawasiliano |
| 11 | Dhamira ya Uhuru |

Chanzo: Data kutoka tamthiliya ya *Mondlane na Samora*.

### 4.5 Hitimisho

Sura imeanza kwa ufafanuzi wa usuli wa mwandshi Profesa Emmanuel Mbogo na Muhtasari wa tamthiliya ya Mondlane na Samora. Baadae surahii imefanya uwasilishaji na uchambuzi wa data kuhusu vipengele vya mitindo na dhamira katika tamthiliya teule ya*Mondlane na Samora*. Data za utafiti zimewasilishwa kwa mkabala wakimaelezo zikiongozwa na nadharia ya Umitindo kwa lengo mahsusi la kwanza na swali la kwanza la utafiti. Nadharia ya Mwitiko wa Msomaji imetumika kwa lengo mahsusi la pili na swali la pili la utafiti huu.

# SURA YA TANO

# MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 5.1 Utangulizi

Sura hii ni ya mwisho katika mpangilio wa tasnifu hii. Hii ni sura muhimu sana ambayo imeonesha kile kilichogunduliwa katika utafiti huu. Vipengele vya msingi vilivyofafanuliwa ni Muhtasari, Hitimisho na Mapendekezo.

## 5.2 Muhtasari

Utafiti huu wenye mada: *Kuchunguza Mtindo na Dhamira katika tamthiliya ya Mondlane na Samora* umegawanywa katika sura kuu tano (5) zifuatazo:

Sura ya Kwanza; Utangulizi wa Jumla: Sura hii imewasilisha vipengele muhimu vifuatavyo: Utangulizi, usuli wa mada, tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti, mipaka ya utafiti na muundo wa tasnifu na hitimisho.

Sura ya Pili; Mapitio ya Kazi Tangulizi na Mkabala wa Kinadharia**:** Sura hii imewasilisha vipengele vifuatavyo: Utangulizi, ufafanuzi wa istilahi mbalimbali, mapitio ya kazi tangulizi na mkabala wa kinadharia: Nadharia ya Umitindo na nadharia ya Mwitiko wa Msomaji na hitimisho.

Sura ya Tatu; Mbinu za Utafiti: Sura hii imewasilisha nakuchambua vipengele vifuatavyo: Utangulizi, eneo la utafiti, kundi lengwa, sampuli na usampulishaji, ukusanyaji wa data, mbinu za ukusanyaji wa data, mbinu za uchambuzi wa data na hitimisho.

Sura ya Nne; Uwasilishaji na Uchambuzi wa Data za Utafiti: Sura hii imejadili vipengele vifuatavyo: Utangulizi, usuli wa mwandishi Emmanuel Mbogo, muhtasari wa tamthiliya ya *Mondane na Samora*. Baadae ni uwasilishaji na uchambuzi wa vipengele vya kimtindo katikatamthiliya ya *Mondlane na Samora*. Pia uwasilishaji na uchambuzi wa dhamira katika tamthiliya ya *Mondlane na Samora* umefanyika.Mwisho sura hii imemalizia kwa kutoa hitimisho.

Sura ya Tano; Muhtasari, Hitimisho na Mapendekezo.Sura hii imezungumzia vipengele vya msingi vifuatavyo: Muhtasari wa kila sura (sura ya kwanza hadi sura ya tano) kwa kuzingatia malengo na maswali ya utafiti husika. Mwisho utafiti huu umetoa mapendekezo kwa watafiti wengineo.

Kwa kutilia mkazo, utafiti huu uliohusu mada: *Kuchunguza mtindo na dhamira katika tamthiliya ya Mondlane na Samora*. Tamthiliya ya *Mondlane na Samora* ni miongoni mwa tamthiliya za karibuni za mwandhishi Emmanuel Mbogo iliyotungwa mwaka (2016). Utafiti huu ulikuwa na malengo mahsusi mawili sambamba na maswali mawili ya utafiti. Lengo mahsusi la kwanza lilikuwa: Kubainisha vipengele vya mtindo katika tamthiliya ya *Mondlane na Samora.* Lengo hilo limewiana na swali la kwanza la utafiti lisemalo: Ni vipengele vipi vya mtindo vilivyobainishwa katika tamthiliya ya *Mondlane na Samora?* Kwa muhtasari uwasilishaji na uchambuzi wa lengo na swali hilo uliongozwa na nadharia ya Umitindo. Kwa upande mwengine, lengo mahsusi la pili lilikuwa: Kubainisha dhamira katika tamthiliya ya *Mondlane na Samora.* Lengo mahsusi hilo limekwenda sambamba na swali la pili la utafiti lisemalo: Nidhamira zipi zilizobainishwa katika tamthiliya ya *Mondlanena Samora?* Lengo na swali hilo liliongozwa na nadharia ya Mwitiko wa Msomaji.

Katika utafiti huu mbinu za utafiti zimejadiliwa kwa kina katika sura ya tatu. Katika sura hiyo, imebainishwa kuwa eneo la utafiti huu ni Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (OUT), Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) na maktaba kuu Zanzibar (zote tawi la Pemba). Walengwa katika utafiti huu ilikuwa ni tamthiliya ya Prof Emmanuel Mbogo ambayo ni *Mondlane na Samora*.Sampuli ya utafiti huu ni Sampuli lengwa. Data za utafiti huu zilikusanywa kwa kutumia mbinu ya usomaji makini kwa data za awali na mbinu ya upitiaji wa nyaraka kwa data za upili.Mbinu hizi zilimsaidia sana mtafiti kuchambua tamthiliya teule na kubaini vipengele vya mtindo na dhamira katika tamthiliya ya *Mondlane na Samora*.  Kwa kuzingatia mada ya utafiti malengo mahsusi mawili na maswali mawili ya utafiti yaliwasilishwa na kuchambuliwa vyema. Kwa muhtasari kulingana na malengo mahsusi na maswali ya utafiti huu matokeo ya uwasilishaji na uchambuzi data ni kama ifuatavyo:

### 5.2.1 Lengo Mahsusi la Kwanza

Katika utafiti huu, lengo mahsusi la kwanza lilikuwa ni: Kubainisha vipengele vya mtindo katika tamthiliya ya *Mondlane na Samora.* Lengo hilo limewiana na swali la kwanza la utafiti lisemalo: Ni vipengele vipi vya mtindo vilivyobainishwa katika tamthiliya ya *Mondlane na Samora?*

Kwa muongozo wa nadharia ya Umitindo,utafiti huu umebaini kwamba tamthiliya ya *Mondlane na Samora* imetumia vipengele vya mtindo vikiwemo: Matumizi ya lugha ambayo yamehusisha tamathali za semi na vipengele vyengine vidogo vidogo vifuatavyo: Tashibiha, tashihisi, sitiari, tafsida, takriri, taswira, mdokezo, mchanganyo ndimi na nidaa.. Pia, kuna matumizi ya vipengele vyengine vya

kimtindo kama vile; matumizi ya nyimbo, hotuba, barua, rejista ya shuleni, rejista ya jeshini, matangazo ya redio na mawasiliano ya simu.

Utafiti huu umebaini kwamba tamthiliya ya *Mondlane na Samora*imefumwa kimtindo kutokana na mapokezi ya kisa cha harakati za kupigania uhuru kutoka katika nchi ya Msumbiji. Vita viliyoongozwa na wanajeshi wa Frelimo wakishirikiana na wanajeshi wa Tanzania dhidi ya jeshi la Wareno.

### 5.2.2 Lengo Mahsusi la Pili

Lengo mahsusi la pili la utafiti huu lilikuwa ni Kubainisha dhamira katika tamthiliya ya *Mondlane na Samora*. Lengo hili liliongozwa na swali la utafiti lisemalo “Ni dhamira zipi zilizobainishwa katika tamthiliya ya *Mondlane na Samora*? Matokeo ya utafiti huu yameonesha kwamba tamthiliya ya *Mondlane na Samora* imeibua dhamira zifuatazo: Dhamira ya mauaji, dhamira ya ukoloni, dhamira ya ubepari na ujamaa, dhamira ya usaliti, dhamira ya vita, dhamira ya umuhimu wa elimu, dhamira ya Umoja wa Bara la Afrika, dhamira ya mapenzi na ndoa, dhamira ya uhuru, dhamira ya ujasiri na ushujaa na dhamira ya mawasiliano

## 5.3 Hitimisho

Utafiti huu umefanikiwa kukamilisha malengo mahususi ambayo yalikuwa mawili. Lengo mahususi la kwanza lilihusu kubainisha vipengele vya mtindo katika tamthiliya ya *Mondlane na Samora*. Matokeo ya utafiti yalionyesha kuwatamthiliya ya Mondlane imetumia vipengele vya mtindo vilivyohusu matumizi ya lugha na vile vilivyohusu sajili mbali mbali kama vile barua, nyimbo,  matangazo ya redio, mawasiliano ya simu, lugha/ rejista ya shuleni na lugha/rejista ya jeshini.

Lengo la pili ambalo lililenga kubainisha dhamira katika tamthiliya ya *Mondlane na Samora*. Kwa ujumla dhamira ambazo mtafiti alizigundua katika tamthiliya hii ni Dhamira ya mauaji, dhamira ya ukoloni, dhamira ya ubepari na ujamaa, dhamira ya usaliti, dhamira ya vita, dhamira ya umuhimu wa elimu, dhamira ya Umoja wa Bara la Afrika, dhamira ya mapenzi na ndoa, dhamira ya uhuru, dhamira ya ujasiri na ushujaa na dhamira ya mawasiliano. Dhamira zote zimelenga kusawiri uhalisia wa maisha ya bara la Afrika wakati wa ukoloni na wakati wa harakati za kutafuta uhuru toka kwa wakoloni.Vile vile mtafiti aligundua kuwa Emmanuel Mbogo amekuwa akichota matukio ya kihistoria ambayo huyafinyanga kisanii kama mawazo makuu ya muongozo wa sanaa yake. Katika kuyaelezea matukio hayo ya kihistoria amejikuta akilazimika kuchota mitindo na dhamira ambazo zilifanikisha kuibua yale aliyoyajadili. Hivyo tamthiliya za Emmanuel Mbogo ni tafiti zilizohusu historia ya jamii ambayo imewasilishwa kwa miktadha ya kifasihi.

## 5.4 Mapendekezo

Utafiti huu umefanywa kwa kutumia tamthiliya moja ya *Mondlane na Samora* ambayo imesawiri matukio ya historia katika bara la Afrika. Hivyo basi, utafiti huu umependekeza kama ifuatavyo:

### 5.4.1 Mapendekezo kwa Watafiti wengine

Utafiti huu unapendekeza kuwa, tafiti zingine zinaweza kufanyika kwa waandishi wengine kwa kutumia kazi zao za fasihi. Tafiti kama hizo zinaweza kutusaidia kuelewa utunzi wa msanii na mbinu zake za utunzi ili kubaini upekee wake katika utunzi. Aidha, utafiti unaweza kufanyika kwa kuchunguza kiulinganishi kazi za E. Mbogo ili kuona mitindo na dhamira inavyolingana ama kutofautiana baina yake na

hata waandishi wengine wa tamthiliya kama vile Said Ahmed Mohamed, Ebrahim Hussein na Penina Mhando

### 5.4.2 Mapendekezo kwa Viongozi

Viongozi wa bara la Afrika wanawajibu wa kuendelea kusoma tafiti mbalimbali pamoja kazi hizi za historia ili kuona namna Waafrika walivyopoteza maisha yao kwa kutaka kuwa huru. Hivyo kila kiongozi anatakiwa atilie maanani lengo la kuleta maendeleo ya taifa badala ya kushughulikia maendeleo yao binafsi. Hii ni kwa sababu kazi ya fasihi ni matokeo ya muktadha na alikokulia mwandishi, dini yake, pamoja na tajriba zake.

### 5.4.3 Mapendekezo kwa Jamii

Jamii za Afrika zinatakiwa zitambue haja ya kuthamini na kutunza tunu ya uhuru wa nchi hizi za Afrika. Wanajamii hao watambue kwamba waasisi wa harakati za ukombozi wa bara la Afrika walifanya juhudi kubwa ya kuhakikisha kwamba uhuru unapatikana bila ya kujali athari zitakazotokea. Kwa mantiki hii ipo haja ya kuwakumbuka, kuwaenzina kuwawekea kumbukumbu maalumu kama sehemu ya heshima yao.

**MAREJELEO**

Babie, E.(1999). *The Basis of Research,* Belmot: Wadsworth Publishing Company.

BAKIZA (2010).*Kamusi ya Kiswahili Fasaha. Oxford University Press, East African Limited, Kenya.*

Cohen, L. et al. (2000). *Research Methods in Education (5th ed). London:Routledge*

Cresswell, J. W. (2009), *Research Design: Qualitative, Quantitative, and Mixed MethodsApproaches. Los Angeles: SAGE Publications.*

Enon, J. C. (2009), *Education Research Statistics and Measurement. Kampala: Makerere University*.

Fadhili, I. (2014*).“Dhima ya Mtindo katika Tamthilia za Kihistoria: Utafiti Linganishi wa Tamthilia ya Morani na Kinjeketile” Tasnifu ya Uzamili ya Kiswahili,Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.*

Florence, N., Buliba, F. A. na Kamau N. G. (2016). Ufafanuzi wa Vichocheo vya Migogoro vya Kindoa kama Vinavyosawiriwa katika iwaya ya Kidagaa

Kimemwozea.Katika jrida la Intenationala Jornal of Advanced Education and Research Toleo Na. 1 uk. 19-27.

Furlong, N. and Lavelace**.** K. (2000). *Research Methods and Statistics: An Intergrated Approach. New York: Hartcourt Colledge Publishers*

Haji, A. A na wenzake. (1982), *“Misingi ya Nadharia ya Fasihi”, Sweden by Berlings, Arlov*

Hussein, I. (1969). *Kinjeketile. Nairobi: Oxford University Press.*

Jilala, H (2014),"Athari za Kiutamaduni katika Tafsiri: Mifano kutoka Matini za Kitalii Katika Makumbusho za Tanzania" Tasnifu ya shahada ya Uzamivu, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Jilala, H(2016). *Misingi ya Fasihi Linganishi: Nadharia, Mbinu na Matumizi. Dar - es - Salam: Daudi Publishing Company*

Kombo, D. K. and Tromp, D. L. A. (2006). Proposal and Thesis Writing: Pauliness Publications.

Kothari, C. R (1990). *Research Methods: Methods and Techniques. New Delhi:Wiley Eastern Ltd.*

Kothari, C. R (2008). *Research Methodology: Methods and Techniques. New Delhi:New Age International Publishing Ltd*

Kothari, C. R (2004). *Research Methodology: Methods and Techniques. New Delhi:New Age International Publishing Ltd*

Kothari, C. R (2013). *Research Methodology.Methods and Techniques, 2nd Ed, New Age International (P) Ltd, New Delhi.*

Leech, G. N. and Short, M. H. (1981). *Style in Fiction: A Linguistics Introduction to English Prose. New York: Longman Group inc.*

Madumulla, J. S. (2009). *"Riwaya ya Kiswahili: Nadharia Historia na Misingi yaUchambuzi". Nairobi:Phoenix Publishers Limited*

Makame, K (2017). *Kuchunguza Dhamira Za Kihistoria na Kisiasa Katika Tamthilia ya Kinjeketile na Sadaka ya John Okello. Shahada ya Uzamili ya Kiswahili Chuo Kikuu Huria Cha Dar - es - salaam*

Mbogo, E. (1980). *Ngoma ya Ng'wanamalundi. Dar es salaam: Tanzania Publishing House.*

Mbogo, E.(2016) *Mondlane na Samora.Dar-es salaam: Tanzania*

Mbonde, J. P. (2002). *Uhakiki na Uchambuzi wa Tamthilia, Riwaya na Ushairi. Dar es Salam: Mkuki na Nyota Publishers*

Mkuwili, O. (2014). "Fani na Maudhui katika Tamthilia ya Ngoma ya Ng`wanamalundi na Kivuli Kinaishi: Utafiti Linganishi.*"*Tasnifu ya Shahada ya Uzamili katika Kiswahili Chuo Kikuu Huria cha Tanzania

Mlama. P.O. (2003). *"Utunzi wa Tamthiliya Katika Mazingira ya Tanzania." Katika Makala za Semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili 111 FASIHI. TUKI: Dar  es Salam*

Mningo, R. (2015). "Mwingiliano matini katika Utunzi wa Emmanuel Mbogo: Utafiti

Linganishi wa Tamthilia ya Ngoma yaNg`wanamalundi na Fumo

Liongo."Tasnifu ya Shahada ya Uzamili Katika Kiswahili, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania

Mnenuka, A. (2018). *Fomula ya Tamthiliya Ndani ya Tamthiliya. Katika TamthiliyaTeule za Kiswahili. Imepakuliwa leo 10/11/2018 2.00 asubuhi katika Journals. udsm. ac. tz*

Mulokozi, M. M. (1996). *Fasihi. Dar es salaam: Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.*

Murumba, J. B. (2013). Mtindo katika Watu wa Gehenna. Tasnifu ya M. A Kiswahilia katika   Chuo Kikuu cha Nairobi (haijachapwa).

Ndungo, C. W. na Wafula, R. M. (1993). *Tanzu za Fasihi Simulizi. Nairobi: University of Nairobi.*

Njogu, K. na Chimerah, R.M. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi. Nairobi: Jomokenyatta Foundation*

Nogu, K. na Wafula, R. M. (2007). *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi. Nairobi: Jomokenyatta Foundation.*

Oiko, A. (2017). Uhakiki wa Mtindo katika Tamthiliya za Arege. Tasnifu ya M.A Kiswahili ya Chuo Kikuu cha Maasai Mara.

Onchangu, R. N. (2013). Mtindo katika Riwaya na Hadithi Fupi za Clara Momanyi. (Tasnifu ya M.A- Kiswahili). Chuo Kikuu cha Nairobi

Ramadhani, D. (2005). The Uses of Metaphors in Mbogo`s Ngoma ya Ng`wanamalundi. (1988) and Husein`s Mashetani (1971). Astylistics Comparison.Tasnifu ya Umahiri (Haijachapwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salam

Massoud, S. (2013). "Maudhui na Fani katika Tamthilia za Kiswahili: Utafiti Linganishi wa Tamthilia ya Mashetani na Kivuli Kinaishi." Tasnifu ya Uzamivu katika Kiswahili Chuo Kikuu Huria cha Dar es Salam

Sengo, T.S.Y na Kiango, S. D, (2012). *Hisiya Zetu. Dar es Salam: Taasisi ya Taaluma za Kiswahili ChuoKikuu cha Dar es Salam*

Sengo, T.S.Y (2009). *Sengo na Fasihi za Kinchi. Dar es salaam:Aera Kiswahili Researched Products.*

Sengo, T. S. Y. na Kiango, D. S. (1975). *Hisi Zetu.Dar es Salam: Chuo cha Uchunguuzi Wa Kiswahili Chuo Kikuu Dar es Salam.*

Senkoro, F.E. M. K. (1982). *Fasihi. Dar es Salaam: Press and Publicity Centre.*

Senkoro, F.E. M. K. (1987). *Fasihi na Jamii. Dar es salaam: PPC.*

Senkoro, F.E. M. K.(2011). *Fashi. Dar es Salam: KAUTTU LTD*

Shimweta, G (2015). "Itikadi katika Tamthiliya za E. Mbogo. Utafiti Linganishi katika Tamthilya ya Ngoma ya Ng`wanamalundi na Fumoliongo." Tasnifu ya Shahada ya Uzamili Katika Kiswahili Chuo Kikuu Huria cha Tanzania

TUKI, (2013) Kamusi ya Kiswahili Sanifu (toleo la 3) Oxford University Press Nairobi.

Wafula, R. M. (2002). *Uhakiki wa Tamthiliya: Historia na Maendeleo Yake. Kenya: Jomo Kenyatta Foundation.*

Wamitila K.W. (2002). *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele Vyake. Nairobi: Phoenix Publishers.*

Wamitila K.W. (2003).*Kamusi ya Fasihi: Istilahi na Nadharia. Nairobi: Focus Publications*

Wamitila K.W. (2008). *Misingi ya Uchambuzi wa Fasihi. Nairobi: Vide-Muwa Publishers Ltd*

Wamitila K.W. (2010). *Kanzi ya Fasihi: Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi.Nairobi: Vide muwa*

Young, P. V. (1984). *Scientific Social Survices and Research. Englewood Chiffs: Prentice Hall. Inc.*

Walliman, N. (2011).*Research Methods: The Basic. New York: Routdige Taylor and Francis Group.*

Wanjala, F. S. (2013*). Kitovu cha Fasihi Simulizi. Mwanza: Serengeti Book shop.*